Nipashe
Ijumaa Novemba 15, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580076
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



# Mbunge aomba msamaha mvuto wafanyakazi ATCL

UKURASA 3


Ukurasa 14
Mkurugenzi Ewura: Hawatuelewi tu, kigezo cha bei ya petroli hiki
Ukurasa 18
Waume waliotelekeza warudi kusikia 'nyumbani kumenoga'
BUFE
Ijumaa Novemba 15, 2019
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Mkurugenzi anayeacha ofisi IMF 'atiririka' pesa mtandao kukubalika
Ukurasa 19
Bosi Latra afunguka kuikabili bodaboda ni 'pasua kichwa'
NA ANTHONY GERVAS
BARABARA ni nyenzo muhimu katika maendeleo ya umma, ikishika sehemu ya tafsiri ya uchumi.
Ili iwe na manufaa, inapaswa kutumika kwa usalama. Hapo ndipo wataalamu wa usalama barabarani wanaitafsiri kwamba: "Ni mwingiliano salama kati ya watumiaji barabara, watembea kwa miguu na vyombo vya moto."
Vilevile kuna suala la kuwapo mazingira ya barabarani kwa maelewano, mfano taa nyekundu inapowaka inamsimamisha mtumiaji, kwani asiposi-
mama, inaunda chanzo cha ajali kinachoishia katika madhara.
Hivyo, katika mfumo wa utumiaji wa barabara, unapaswa kuangukia katika maana 'salama.' Katika kuliangalia hilo na mengineyo, ndiyo serikali ikaunda chombo Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini (Latra).
Hata hivyo, kihistoria hilo ni zao jipya la iliyokuwa Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (Sumatra), iliyoanza baada ya serikali kujitoa katika utoaji huduma za kibiashara kuanzia
INAENDELEA UK.16
UCHUMI
Habari katika picha
Ukurasa 17

UKURASA 13

# Mkapa: Niliruhusu mawaziri kunikosoa




Distributed via ippmedia

• **Asema** aliyekosea alimtaka ajipime na kujitumbua, aeleza alivyopata taabu kuteua Gavana BoT... *Endelea uk. 2*

# Neema ajira walimu 16,000

UKURASA 3


Sabaya Lema

# Mbunge Lema mbaroni kwa amri ya DC Ole Sabaya

UKURASA 2



Scan Hapa
Fungua App ya QR code Reader kisha scan kupakua APP yetu
GET IT ON Google Play
Download on the App Store

MICHEZO STARS: NJOONI, E' GUINEA HAWATOKI UK.32
MAONI, KATUNI UK.6

# JKCI yaokoa bil. 89/- matibabu moyo ndani

**Na Joseph Mwendapole**

KATIKA kipindi cha miaka minne, Serikali imeokoa zaidi ya Sh. bilioni 89 kwa wagonjwa 5,954 wenye matatizo makubwa ya moyo ambao walifanyiwa upasuaji wa kufungua na bila kufungua kifua katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI).

Iwapo wagonjwa hao wangetibiwa nje ya nchi, serikali ingetumia zaidi ya Sh. bilioni 178 kulipia gharama za matibabu hayo.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Prof. Mohamed Janabi, alisema hayo jana wakati akielezea mafanikio ya miaka minne ya serikali ya awamu ya tano kwa upande wa matibabu ya moyo, katika kikao cha Bodi ya Wadhamani ya taasisi hiyo.

Prof. Janabi alisema kwa wagonjwa hao kutibiwa nchini matibabu yao yamegharimu cha Sh. bilioni 89 fedha ambazo zimelipwa kupitia bima zao za matibu, misaada ya wafadhili mbalimbali wa nje, wagonjwa wenyewe kujilipia na serikali kugharamia matibabu ya wagonjwa wasio na uwezo wa kumudu gharama hizo.

"Gharama ya mgonjwa mmoja aliyefanyiwa upasuaji nje ya nchi ni zaidi ya Sh. milioni 30. Lakini kwa mgonjwa mmoja kutibiwa hapa nchini gharama zake hazizidi Sh. milioni 15.

'Kwa kutibiwa hapa nchini fedha anazolipa mgonjwa zinatumika kununua vifaa tunavyomwekea katika moyo wake kama vile

INAENDELEA UK. 8

# Mkapa: Niliruhusu mawaziri wanikosoe

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS mstaafu Benjamin Mkapa amesema aliruhusu mawaziri wake kumkosoa na kutoa nafasi kwa mawaziri wake kujitafakari na kujiuzulu nafasi zao pale walipofanya makosa.

Katika sura ya 10 ya kitabu chake kilichozinduliwa Jumanne na Rais John Magufuli, Mkapa aliyeongoza Tanzania kwa miaka 10 kuanzia mwaka 1995, anaeleza jambo hilo.

Mkapa (81), anasema alilazimika kutoa fursa hiyo kwa wasaidizi wake hao ili kufuata nyayo za Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere ambaye Rais huyo wa awamu ya tatu anakiri kujifunza uvumilivu kutoka kwake.

Katika ukurasa wa 118 wa kitabu chake hicho, Mkapa anasema alijifunza kwa Mwalimu Nyerere kuwa mtulivu, mvumilivu na kuwa tayari kusikiliza mawazo ya wengine na kutafuta makubaliano ya pamoja katika kujenga mazingira mazuri ya kazi.

"Kwa wote tuliofanya kazi na Mwalimu (Nyerere), kuna nyakati tuliona alifanya uamuzi kwenye jambo fulani lakini bado tulifanya jitihada za kulijadili, akitaka na sisi pia tulielewe.

"Nilijitahidi kuendeleza utamaduni huo wa kutafuta ushauri kutoka kwa baraza langu. Niligundua utaratibu huo ulifanya vizuri sana kutokana na uhalisia kwa kuwa hatukutofautiana umri kwa kiasi kikubwa, hivyo majadiliano yalikuwa ya wazi," Mkapa anasema.

Anakiri kulikuwa na ugumu katika kuyaweka pamoja baadhi ya maoni ya mawaziri, lakini mara nyingi alijitahidi kupata ushauri wao kwenye masuala ya sera na mara chache alifanya uamuzi wa haraka.

"Mwishowe wajumbe wa Baraza la Mawaziri walitofautiana na uamuzi wangu na kulikuwa na utamaduni imara kuwa ndiyo wenye jukumu la kumshauri Rais, naye akakubali.

"Rais anaweza kupuuza ushauri wowote aliopewa, lakini wana njia mbadala ya kujiuzulu kama hawakubaliani naye kwenye jambo fulani.

"Nashukuru katika wakati wa uongozi wangu hakuna waziri aliyejiuzulu kwa sababu hiyo kwa kipindi chote cha uongozi kuanzia mwaka 1995 hadi 2005," Mkapa anasema.

INAENDELEA UK. 8




Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani, akiwavusha barabarani wanafunzi wa shule ya msingi katika eneo la Kamata, Kata ya Gerezani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz
In replay please quote:

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,

NOTICE TO THE PUBLIC

1. The general public is hereby notified that there will be a movement of special loads from **MPANDA to HANDENI, TANGA** by vehicles with registration number(s) **T864CVX/T473CVG and T192DQV/T805DQV of PMM ESTATES (2001) LTD.** The journey is schedule to start on **15/11/2019**

2. Special load dimensions:
   **Length - 17.5m**
   **Width - 3.2m**
   **Height - 4.7m5**

3. **Route:** from **MPANDA to HANDENI via MBEYA** Travelling time will be only day time ***(06:30 am -06:00pm)***

115517702

***We regret for any inconvenience caused***

# Mbunge Lema mbaroni amri ya DC

**Na Mwandishi Wetu, HAI**

MBUNGE wa Arusha Mjini, Godbless Lema (Chadema) na watu wengine watano, akiwamo Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Helga Mchomvu, jana walikamatwa na kushikiliwa na Jeshi la Polisi wakidaiwa kukusanyika isivyo halali.

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, alithibitisha viongozi hao wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kukamatwa majira ya saa 6:30 mchana.

Alisema alipata taarifa za kuwapo kwa Lema na kundi lake wilayani Hai kwa kazi maalum aliyodai ni kupanga mikakati ya kumbeba mbunge huyo katika uchaguzi wa viongozi wa Chadema ambao Msajili wa Vyama vya Siasa ameagiza ufanyike.

"Hai haiwezi kuwa sehemu ya makutano ya magenge yanayopanga mipango ya kupotosha wananchi au kutumika kumbeba Lema kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chadema wa Kanda," alisema.

Kwa mujibu wa Ole Sabaya, Lema na wenzake hao wanadaiwa kukutwa kwenye ofisi ya Chadema iliyoko eneo la Gezaulole, Kata ya Bomang'ombe wilayani Hai, wakipanga mikakati ya kuandaa mkutano wa kisiasa isivyo halali.

Ingawa kiongozi huyo wa wilaya hakuwataja watu wengine wanne waliokamatwa na kushikiliwa na Jeshi la hilo wakiwa na Lema na Mchomvu, Ole Sabaya viongozi hao kuhojiwa na jeshi hilo.

"Ni kweli Jeshi la Polisi Wilaya ya Hai linamshikilia Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema, pamoja na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Hai kwa kukusanyika na kufanya mkutano usio halali.

"Lema amekamatwa muda mfupi baada ya Mwenyekiti wa Halmashauri ya Hai kukamatwa katika eneo hilo la Gezaulole ilipo ofisi ndogo ya Chadema," alisema.

Nipashe ilimtafuta Katibu wa Chadema Mkoa wa Kilimanjaro, Basil Lema, kuzungumzia suala hilo na alisema:

"Na mimi nimepata hizo taarifa muda si mrefu kutoka kwa Katibu wa Chadema Wilaya ya Hai, akinitaarifu kwamba Mbunge wa Arusha Mjini na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Hai, Helga Mchomvu, wamekamatwa na polisi na wanashikiliwa."

Kiongozi huyo wa Chadema alisema chama kilikuwa kinafuatilia taarifa hizo na kufuata taratibu za kuwawekea dhamana.

Mkutano wa 17 wa Bunge la 11 unahitimisha leo bungeni bila uwapo wa Lema kutokana na mbunge huyo kufungiwa kushiriki mikutano ya chombo hicho kwa kuunga mkono kauli ya aliyekuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, kwamba anafikiri 'Bunge ni dhaifu'.

## HABARI KITAIFA



Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga (wa pili kushoto), akikata utepe kuzindua vitabu vyenye ripoti ya haki za binadamu na viwango vya kazi katika biashara, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Ujengaji wa Uwezo na Uwajibikaji wa kituo hicho, Felista Mauya, Mwenyekiti wa Bodi wa kituo hicho, Prof. Geofrey Mmari (kulia) na Naibu Ofisa Mipango wa Ubalozi wa Sweden, Anders Winberg. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbunge aomba msamaha mvuto wafanyakazi ATCL

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

MBUNGE wa Uvinza, Hasna Mwilima (CCM), amewaomba radhi wanawake kwa kauli yake ya wiki iliyopita bungeni kuwa 'wahudumu wa Shirika la Ndege (ATCL) hawana mvuto'.

Amedai aliitoa kauli hiyo kwa nia nzuri ya kuboresha utendaji wa shirika na si kuwadhalilisha wanawake, husu-sani wahudumu wa ndege za ATCL.

Kabla ya kuanza kwa kipindi cha 'Maswali' bungeni jana, mbunge huyo alisimama na kuomba radhi kutokana na kauli yake hiyo, jambo ambalo lilionekana kuwagusa wabunge wengi walioamua kumshangilia.

"Nilifanya vile kwa dhumuni la kuboresha shirika letu la ATCL, lakini inawezekana kwa namna moja au nyingine nikawa nimewakwaza Watanzania, hasa wanawake wenzangu. Naomba nichukue nafasi hii Mheshimiwa Spika kuomba radhi kwa kauli yangu niliyoitoa mbele yenu," alisema.

Kutokana na kauli hiyo, Spika Job Ndugai alisema: "Kabla hujaendelea, nilitaka kusema, waheshimiwa wabunge, huo ndiyo uungwana, tumeipokea radhi hiyo."

Wiki iliyopita, Mwilima wakati akichangia mapendekezo ya serikali kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha, alizua gumzo kwenye mitandao ya kijamii na hata bungeni baada ya kulitaka shirika hilo kuajiri wahudumu wenye mvuto.

Alisema wahudumu wa shirika hilo hawana mvuto na ni wafupi kiasi cha kusababisha ndege za shirika hilo kutokuwa na mvuto kwa wateja.

"Wahudumu wetu kwenye shirika letu la ndege hawana mvuto, utakuta Air hostess mfupi, hana mvuto, mhudumu nyuma yupo kawaida, hata mimi na miaka yangu ni 50 nimeshazeeka, nilivyo ninavutia.

"Tunapoajiri 'ma-Air hostess', akiwa ndani ya ndege inatakiwa ukimwita, akigeuka abiria anaona kweli..." alisema Mwilima.

Hata hivyo, kauli ya mbunge huyo ilimlazimu Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye, kuitisha mkutano na waandishi wa habari na kuijibu kuwa serikali haitumii kigezo cha mvuto katika kuajiri watumishi wa ATCL.

# Neema ya ajira 16,000 za walimu

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SERIKALI imesema inatarajia kuajiri walimu 16,000 wa shule za msingi na sekondari muda wowote kuanzia sasa.

Waziri Mkuu Kasim Majaliwa, alitangaza neema hiyo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Mlalo, Abdallah Shangazi (CCM), aliyetaka kufahamu mkakati wa serikali kuhakikisha sekta za elimu na afya zinakuwa na watumishi wengi.

"Sekta za elimu na afya zina upungufu mkubwa sana wa watumishi. Sasa, ni upi mkakati wa serikali kuhakikisha tunapata watumishi wa kutosha kwenda kuwahudumia Watanzania?" mbunge huyo alihoji. Katika majibu yake, Waziri Mkuu alikiri sekta hizo mbili zina uhitaji wa watumishi kutokana na serikali kutanua huduma zake hadi ngazi ya vitongoji.

"Serikali imeanza kutoa vibali vya ajira katika sekta hizi mbili za afya na elimu, hata kwenye kilimo. Mwaka jana, tuliajiri watumishi 6,000 na sasa tuna kibali ambacho kitatoka hivi karibuni cha watumishi 16,000 kwa upande wa sekondari na msingi. "Tunaamini baada ya ajira hizi kwenye sekondari na elimu msingi, tutakuwa tumepunguza kwa kiasi kikubwa uhaba wa walimu, hivyo hivyo kwenye sekta ya afya, tunataka kuhakikisha tunapeleka wataalamu. Mkakati wa kujenga miundombinu utakwenda sambamba na kuajiri wataalamu," alisema.

Aliongeza kuwa serikali imefanya maboresho makubwa na sera inaeleza kuwa kila kata kuwe na kituo cha afya na kila wilaya iwe na hospitali. Alisema kinachoendelea kwa sasa ni ujenzi wa zahanati na vituo vya afya vyenye uhitaji wa madaktari. Mei 22, 2017, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, ililiambia Bunge kuwa, imebaini Tanzania inakabiliwa na uhaba wa walimu 182,899 wa shule za msingi na 69,794 wa shule za sekondari.

### UHABA WA CHAKULA

Katika hatua nyingine, Majaliwa amewaagiza wakuu wa wilaya na mikoa nchini, ambao maeneo yao yana upungufu wa chakula, kukutana na wafanyabiashara ili kupata chakula kwa kununua kutoka mikoa yenye chakula kingi.

Waziri Mkuu alitoa agizo hilo alipojibu swali la Mbunge wa Chemba, Juma Nkamia (CCM), aliyetaka kupata kauli ya serikali kuhusu maeneo yenye uhaba wa chakula. Alisema upungufu wa chakula upo katika baadhi ya wilaya na maeneo kadhaa kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

"Ni jukumu la wafanyabiashara wetu kufanya biashara, kuhamisha chakula kutoka maeneo yenye chakula cha kutosha na kupekeka maeneo ambayo hayana chakula ili kujipatia kipato," alisema. "Wakuu wa wilaya na mikoa pindi wanapokutana na hali hii, wakutane na wafanyabiashara, wawashawishi kuchukua chakula kutoka maeneo yenye chakula na kuwaletea."

Alisema serikali ina chombo cha kununua na kuhifadhi chakula (NFRA) na baada ya kununua, hupeleka katika maeneo ambayo yana upungufu wa chakula na kuyauzia.

Kwa sasa, alisema serikali inachosubiri ni viongozi wa maeneo hayo, wakiwamo wakuu wa wilaya, kuandika na kuonyesha maeneo yao yana upungufu wa chakula ili Wizara ya Kilimo ianze kuratibu na kuona namna ya kuwafikishia chakula.





HAIUZWI KWA WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 18. TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU.

# Afariki akijiandaa mtihani kidato 4

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

MWANAFUNZI aliyekuwa akiendelea na mtihani wa taifa wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Mwemage Kata Ibwera Bukoba Vijijini, Pasficus Medichades, amefariki dunia kutokana na kukosa hewa ya Oksijeni katika chumba alimokuwa akiishi.

Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Revocatus Malimi, alisema kuwa mwanafunzi huyo alikutwa na mauti usiku wa kuamkia Jumamosi, na kwamba alikuwa amejifungia ndani akiendelea kujisomea ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya mtihani .

Kamanda Malimi alisema inahofiwa wakati akiendelea kujisomea alipitiwa na usingizi na wakati huo kulikuwa na jiko la mkaa ndani likiwaka.

"Kwa bahati mbaya alifunga mlango na madirisha, kwa hiyo alikosa hewa akawa amefariki," alisema.

Mkuu wa shule hiyo, Leonard Ndyakowa, alisema mwanafunzi wake aliyekuwa akiendelea na mtihani wa kuhitimu kidato cha nne, na kueleza kuwa alikuwa akiishi na mama yake mzazi, ambaye siku ya tukio aliondoka kwenda katika makazi yake mengine na kumwacha mtoto wake peke yake.

"Ni tukio la kweli, lakini limetokea nje ya mazingira ya shule, inaonekana mwanafunzi huyo alikuwa akipika ndani, akajilaza pembeni na inaonekana alikuwa akijikumbushia masomo kwa kujisomea akapitiwa na usingizi, na ndo kikawa kifo chake," na kuongeza:

"Alikuwa amebakiza mtihani mmoja tu Biolojia paper 2, lakini Mungu akamchukua, tulishtushwa sana na taarifa za kifo chake, lakini hatuna la kufanya, ni mapenzi ya Mungu."

"Ni tukio la kwanza kutokea katika mtihani huu, limetusikitisha lakini baada ya kutokea mwanafunzi walipata mshtuko na baadae walirejea katika vyumba vya mtihani na kuendelea na mitihani yao, alisema Ofisa Elimu (sekondari) Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, Deo Chacha.

# Chadema wamganda Jafo kujiuzulu

**Na Waandishi Wetu**

BARAZA la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), limemtaka Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, kujiuzulu kwa kile kinachodai kushindwa kutimiza wajibu wake katika mchakato wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa baraza, Patrick Ole Sosopi, alidai kitendo cha waziri huyo kutoa kauli zinazotofautiana kuhusiana na uchaguzi huo, kimeonyesha hana nia njema na uchaguzi wenyewe.

"Waziri Jafo ameonyesha sura nne tofauti, kitu kinachothibitisha ameshindwa kazi yake. Sisi kama baraza la vijana tunamtaka ajiuzulu," Sosopi alisema.

Jumapili, Jafo aliagiza wagombea wote walioenguliwa katika mchakato wa uchaguzi huo, kurejeshwa. Kauli hiyo iliibua mjadala mzito na siku iliyofuata, waziri huyo alijitokeza tena na kusema ilikuwa imetafsiriwa vibaya. Alidai aliowalenga ni waliorejesha fomu na kuteuliwa na wasimamizi wa uchaguzi ndiyo wanaotakiwa kugombea nafasi hizo.

Vyama vingine vya upinzani vinavyomtaka Jafo kujiuzulu ni pamoja na ACT-Wazalendo na National League for Democracy (NLD), ambavyo pia vinataka mchakato wa uchaguzi huo uanze upya.

**KAULI YA WAZIRI MKUU**

Bungeni jijini Dodoma, jana Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kusikiliza sera za wagombea wa nafasi mbalimbali katika uchaguzi huo uliopangwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu.

Waziri Mkuu alitoa rai hiyo alipojibu swali la Mbunge wa Iramba Mashariki, Allan Kiula (CCM), aliyetaka kauli ya serikali baada ya kuwapo kwa malalamiko kutoka kwa wananchi wakihofu kukosa haki zao za msingi za kupiga kura na kupigiwa kura.

Majaliwa alisema katika uchaguzi huo kulikuwa na maandalizi ya kujiandikisha, kuchukua na kurudisha fomu na kinachosubiriwa kuanza kwa kampeni za wagombea Novemba 17.

"Nitoe wito kwa Watanzania, kipindi kinachokuja watu waende kusikiliza sera za wagombea hao na nia thabiti ya kuwaletea maendeleo katika maeneo yao. Na kila Mtanzania apate nafasi ya kumchagua kiongozi anayemtaka," alisema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Abel & Fernandes, Fatma Fernandes, akizungumza katika uzinduzi wa kampeni dhidi ya ugonjwa wa kisukari, jijini Dar es Salaam jana, ambayo imelenga kuboresha huduma za afya na maisha ya watu wanaoishi na ugonjwa huo nchini. **MPIGAPICHA WETU**

# Wadau waunganisha nguvu dhidi ya kisukari

**Na Mwandishi Wetu**

TISHIO la ugonjwa wa kisukari limewaibua wadau kadhaa kuunganisha nguvu kuendesha mapambano.

Kampuni ya Mawasiliano ya Abel & Fernandes imeungana na Kampuni ya Afya ya AAR na wadau wengine kwa lengo la kushirikiana katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo ambao umeelezwa kusababisha zaidi ya watu 40,000 kukatwa miguu kwa mwaka.

Akizungumza katika uzinduzi wa kampeni hiyo jana, jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa Abel & Fernandes, Fatma Fernandes, alisema kampeni hiyo dhidi ya kisukari imelenga kuboresha huduma za afya na maisha ya watu wanaoishi na ugonjwa huo.

Alisema kampeni hiyo iliyopewa kaulimbiu ya 'Tenda Leo, Mabadiliko ya Kesho ...tuungane kutokomeza kisukari' imelenga kuwaunganisha wadau mbalimbali kuboresha huduma za kinga, tiba ili kudhibiti ugonjwa wa kisukari.

Alisema watatoa huduma kwa mamia ya jamii iliyokumbwa na kisukari, kutoa taarifa muhimu kuhusu kisukari na kupaza sauti kwa wale waliokosa haki zao dhidi ya ugonjwa wa sukari.

"Ugonjwa wa kisukari nchini unakua, kwa sababu hadi sasa watu zaidi ya milioni 4.2 wamebainika kuwa na ugonjwa huo. Abel & Fernandes tunaelewa tatizo hili, ndio maana tumeamua kuungana kuelimisha watu juu ya ugonjwa huo ili waweze kupata matibabu sahihi na kujua namna ya kujitunza," alisema.

Alisema ili kufikia malengo hayo ya uhamasishaji, Abel & Fernandes inakusudia kufanya kazi na madaktari na wataalamu ili kuhakikisha kuwa huduma sahihi zinatolewa katika hospitali mbalimbali kwa walioathirika na ugonjwa huo.

"Tunapaswa kuanza kwa vitendo sasa, ambapo hatua ya kwanza ni kuunga juhudi ya serikali kuboresha huduma zinazotolewa dhidi ya waathirika wa ugonjwa huo kwa kuanzisha mikakati ya kitaifa ya kuudhibiti na kuwa na ufuatiliaji wa mara kwa mara. Hii itaruhusu matumizi bora ya rasilimali, ambayo ni muhimu ikiwa mkoa utaandaa mikakati thabiti ya kudhibiti janga hilo,"alisema.

Aidha, naye Dk. Akil Msei kutoka AAR, alisema kwa mujibu wa ripoti za Shirika la Afya Duniani (WHO) takwimu zinaonyesha kila sekunde 10 mtu mmoja mwenye kisukari hufariki duniani na zaidi ya watu 40,000 wenye kisukari Tanzania hukatwa miguu.

Alisema pia zaidi ya watu milioni 422 wana kisukari duniani hivyo kupelekea ugonjwa huu kushika nafasi ya 5 kama kisababishi cha vifo.

"Tutakuwa na kampeni za barabara ambazo zitatembelea maeneo ya Tegeta na Kariakoo kwa kutoa huduma katika magari maalumu ya kidijitali.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni lazima kila mtu asajili simu

**WATANZANIA** wanalazimika kusajili simu licha ya Wizara ya Mambo ya Ndani kueleza kuwa hakuna atakayefungiwa simu ifikapo Desemba 31, 2019.

Mwisho wa mwezi ujao ndiyo siku ya mwisho ya kusajili namba za simu na kwa mujibu wa Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA), ambaye hatasajili laini atafungiwa.

Licha ya hakikisho hilo la serikali ni vyema Watanzania wakafahamu kuwa suala la kusajili simu ni muhimu kwa sababu kuna uovu mwingi unaofanyika kupitia simu za mkononi.

Itakumbukwa kwamba simu hizo zimetumiwa mara kadhaa kuiba fedha za watu kwa utaratibu wa kuandika ujumbe wa kuomba kutumia pesa na kudanganya kuwa jina litakalokuja ni la fulani.

Wizi huo maarufu kama 'tuma kwa namba hii' umesababisha watu wengi kupoteza fedha zao na matapeli kuendelea kushere-hekea kujinufaisha na uovu bila hofu.

Tunasema haya kwa sababu ilikuwa ni kawaidakwa baadhi ya vijana mtaani kulala maskini na kuamka matajiri na hakuna mtu aliyeweza kuwauliza wamefanyaje au kutumia miujiza gani kufanikiwa kiasi hicho. Kumbe wengi walikuwa wanatumia njia hiyo ya wizi wa kusema 'tuma kwa namba hii.'

Lakini, si hivyo pia wapo baadhi ya vijana walikuwa wanatumia simu za mkononi kurubuni mabinti. Walikuwa wanatumia simu zisizosajiliwa kuwaandikia ujumbe wa kuwalaghai na kufanya nao ngono na pale ujumbe wa mapenzi ulipofikishwa mahakamani waliruka kwa vile hazikuwa simu zao, kwani hazijasajiliwa kwa majina yao.

Yote haya yanakoma kwa kusajili simu hizo ili hata mazoea ya kuishi bila maadili nayo yakomeshwe pia.

Tunapenda kusema kuwa mahali popote ambapo vitendo vya matumizi ya simu kiholela hayatadhibitiwa ni wazi kuwa kutakosekana amani na kama una amani hiyo, haitakuwa na manufaa kwa vile kuna wajanja wanaoivuruga.

Lakini, pia tukumbushane kuwa mahali popote ambapo mtu anaweza kujichumia mali iwe kwa kuiba kwa kutumia simu iwe kubaka na kuhadaa wanafunzi kwa kutumia simu, kutapeli fedha za watu kwa kutumia majina ya watu wenye heshima kwenye jamii kwa kuanzisha akaunti za Twitter, WhatsApp na Instagram yatakoma kwa kusajili namba hizo kwa alama za vidole.

Kwa kusajili simu zetu wezi na wahalifu mbalimbali watakamatwa. Aidha, hata matumizi ya simu yatakuwa ni kwa njia ya uwajibikaji si kutuma picha za ngono, chafu, za kutisha wala kusambaza ujumbe wa kashfa na chuki mitandaoni.

Wananchi wajue kwamba simu zikisajiliwa hata kupanga 'madili' ya kupora na kuua watu yatapungua. Upangaji huo wa wizi unaweza kutumiwa na wafanyakazi ndani ya taasisi fulani hasa za fedha. Hawa wanaweza kushiriki kuhujumu benki au shirika na kusaidiana na majambazi kuiba.

Watuhumiwa hao ambao huitwa 'internal criminals' ambao pamoja na kuajiriwa hutumia nafasi hizo kusuka 'dili' na majambawazi mfano kuwajulisha ni lini, wapi na fedha nyingi zitaletwa kwenye matawi yao au kuchukuliwa wanadhibitiwa kwa kusajili namba za simu kwa vidole.

Ndiyo maana tunataka kusikia kuwa wenye simu wote wawe wamezisajili ifikapo Desemba 31. Aidha ni vyema taifa liwe na sheria kutangaza kuwa ni lazima kusajili simu kwa alama za vidole na ambaye hatafanya hivyo anakutana na adhabu kali iwe mteja ama kampuni inayohusika.

Aidha, sheria isisitize kuwa watakaoshindwa kusajili simu kutokana na ama kukosekana kitambulisho cha taifa au sababu nyingine wachukuliwe hatua na kuhakikisha kuwa usajili unakamilishwa na kuondoa ujanja na uhalifu unasababisha watu kukwepa kusajili simu.

Ndiyo maana tunaendelea kusema kuwa pamoja na maelezo ya wizara ni lazima Watanzania wasajili simu zao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



# Mnaouza dawa bandia, nini hiyo kwa jamii ?

Na Yasmine Protace

Distributed via ippmedia

**DAWA** bandia ni tabu kubwa. Zinamuathiri mtumiaji pale, atakapozitumia na zina madhara makubwa kwa watumiaji.

Pia, zinapotumika hata kwa wanyama kama mifugo na mimea, napo ni changamoto, hasa pale mmea ukuaji wake hauwi mzuri na hata mfugo unapowekewa nao uweza kufariki.

Inasikitisha kuona watu wanaofanya biashara za kuuza dawa wanakuwa, sio waaminifu kwa kuuza visivyofaa kwa walaji na hata mimea.

Inakuwaje mtu apate utajiri mkubwa kupitia kuuza kitu kinachomletea madhara mtumiaji. Ikumbukwe kwamba, binadamu tuna matatizo ya kiafya na tunapokula dawa, malengo ni kupona, ili kuendelea na majukumu mengine.

Lakini, kinachotusikitisha unakula dawa tena ni feki ambazo nazo anachangia mtu kuendelea kulala kitandani.

Serikali imekuwa ikipambana na hata kuwachukulia hatua watu wote wanaokamatwa, wakijihusisha na uuzaji wa dawa bandia.

Tumekuwa tukiona misako katika maduka ya dawa ikiwamo maabara za watu binafsi, lengo ni kupambana na watu wanaojihusisha na uuzaji dawa bandia na kutoa matibabu kwa dawa zizisofaa.

> **Tumekuwa tukiona misako katika maduka ya dawa ikiwamo maabara za watu binafsi, lengo ni kupambana na watu wanaojihusisha na uuzaji dawa bandia na kutoa matibabu kwa dawa zizisofaa.**

Katika misako hiyo, baadhi ya maduka ya kuuza dawa na maabara za watu binafsi zilibainika kutoa huduma zisizofaa kwa kutumia vifaa vilivyo chini ya kiwango.

Hivi karibuni, mikoa ya pembezoni ya Kigoma, Arusha na Kilimanjaro imeonekana kuwa kinara wa uingizaji dawa nchi ikiwamo ya Kanda ya Magharibi, Kanda ya Ziwa na Kaskazini imeripotiwa kuwa kinara wa dawa duni za binadamu na mifugo, vifaa tiba na vitendanishi ambavyo havikusajiliwa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA).

Akitangaza matokeo ya operesheni maalum ya dawa, vifaa tiba, vitenganishi, dawa asili na tiba mbadala mbele ya waandishi wa habari jijini Dar e Salaam, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Akida Khea, anasema hilo wilaya zaidi ya 33 katika mikoa 20 wameweza kukamata dawa bandia aina saba zenye thamani ya fedha za kitanzania Sh. 12,495,500.

"Katika dawa hizo, uchunguzi wetu baada ya kuzibaini tuliweza kuwasiliana na wamiliki wa dawa husika ambapo walituthibitishia kuwa ni bandia na zingine zimegushiwa maandishi" anasema.

"Tumebaini mikoa iliyo pembezoni ikiwemo Kigoma kubainika kuwa na dawa nyingi bandia pamoja na Mwanza. Pia, mikoa ya Kaskazini ikiwamo Arusha na Kilimanjaro, nayo imebainika kuwa na wingi wa dawa hizo" anasema.

Katika tukio hilo, TMDA waliwashirikisha mamlaka mbalimbali wakiwamo Jeshi la Polisi, Msajili wa Baraza la dawa asili na tiba mbadala pamoja na Tamisemi.

Mrakibu wa Jeshi la Polisi kutoka makao makuu ya upelelezi kitengo cha Interpol, anasema jeshi hilo linafuatilia kwa karibu, wahusika waliobainika katika kuingiza au kusambaza watachukuliwa hatua.

"Wajibu wa jeshi la Polisi ni kulinda usalama wa raia na mali zao. Usalama wa raia ni pamoja na afya za wananchi sisi kama Jeshi la Polisi kwa pamoja tunahakikisha usalama wa raia, unalindwa na wahusika watafikishwa kwenye vyombo vya sheria uchunguzi ukikamilika" anasema.

# Mameneja maji washushwa vyeo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMENEJA 14 wa mikoa na wilaya wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa) wametenguliwa kwenye nafasi zao kutokana na utendaji wao kutoridhisha.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema viongozi hao waliteuliwa Julai mwaka huu na wamefanyiwa tathmini kwa miezi mitatu kulingana na majukumu waliyokuwa wamepewa.

"Tulisema tutawapima kila robo ya mwaka na kutokana na tathmini tuliyofanya, tumeamua kufanya mabadiliko katika ngazi za mikoa na wilaya. Tumefanya mabadiliko ya vituo vya kazi kwa wahandisi na mameneja na kuteua wengine wapya," alisema.

Katibu mkuu huyo alisema viongozi hao wametenguliwa kutokana na kasi yao ya kiutendaji kutoendana na kasi ya Wizara, Ruwasa na sekta yenyewe inavyotaka.

"Tunataka kasi na matokeo ya haraka na tunapoona hayaendi vizuri tunafanya uamuzi,"alisema.

Aliwataja waliotenguliwa kuwa ni Genes Kimaro, Sylivester Paulin, Fredrick Magige, Renatus Gumba, Emmanuel Alexandar, Frank Elisa, Grace Mukulasi, Joseph Ntellya, Michael Ndunguru, Bahati Haule, Daudi Amlima, Crispin John, Aaron Swai na Renard Baseki.

Alisema watapangiwa vituo vyao vya kazi baadaye kuendelea na kazi ya uhandisi.

Akizungumzia utendaji kazi wa wakala huo kwa kipindi cha miezi mitatu, Prof. Mkumbo alisema Ruwasa imekabidhiwa kuendelea kusimamia jumla ya miradi 652 vijijini ambayo ipo katika wilaya nchini.

Alisema kwa kipindi cha Julai hadi Oktoba mwaka huu, miradi ya maji 69 imekamilika yenye vituo vya kuchotea maji 1549 na ambayo inahudumia watu 412,250. Pia alisema katika kipindi hicho, kwa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2019/20, miradi 108 imelipwa Sh. Bilioni 14.2 na inatarajiwa kuhudumia wananchi 1,120,623 katika maeneo ya vijijini.

# Ndugai asema Mbowe mtoro Bungeni

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema utoro wa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Freeman Mbowe, umekuwa ukisababisha nafasi ya maswali ya moja kwa moja kutoka upinzani kwenda kwa Waziri Mkuu kupotea kila mara.

Aliyasema hayo jana asubuhi bungeni mjini hapa wakati wa kipindi cha 'Maswali kwa Waziri Mkuu' kutoka kwa wabunge.

Ndugai alisema kwa mujibu wa utaratibu wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola, upinzani hupewa nafasi ya kwanza kuiuliza swali serikali, lakini kwa hapa nchini nafasi hiyo hupotea kila wakati kutokana na utoro wa kiongozi huyo.

"Waheshimiwa wabunge, niwataarifu tu kwamba utaratibu wetu wa kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu, swali la kwanza kabisa huwa linakuwa akiba kwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, lakini kwa leo (jana) kama mnavyoona kiongozi huyo hayupo," alisema Ndugai.

Alisema Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani anaweza siku zote asiwepo bungeni lakini siku ya Alhamisi ni muhimu awepo kutokana Waziri Mkuu kuwapo na anatakiwa awe wa kwanza kuuliza swali.

"Huwa ni fursa pekee ambayo upinzani wanapata nafasi kwa hiyo kiongozi wa upinzani anaweza asiwepo bungeni siku yoyote, lakini siku ya Alhamisi ambayo ni ya Maswali kwa Waziri Mkuu ni lazima awepo," alisema Spika.

Alisema hata hivyo hana taarifa zozote za udhuru kutoka kwa kiongozi huyo (Mbowe) na wala hajui yuko wapi.

"Kwa hiyo hatujapata swali lile kwa kuwa kiongozi wa upinzani bungeni hayupo, uwe wapi, uwe wapi kama Spika hana taarifa zako ni mtoro tu kwa hiyo, ni mtoro na ndiyo maana leo unaona kwamba hiyo fursa ambayo imewekwa kwenye kanuni haitekelezwa.

"Na ndio maana mnaona kwamba nafasi inapotea sababu ya utoro," alisema Spika Ndugai.

Nipashe ilimtafuta Mbowe ili kupata taarifa za yeye kutokuwapo katika kipindi hicho cha Maswali kwa Waziri Mkuu, lakini simu yake haikupatikana.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mafuta ya Total, Jean Francois Schoepp, akisafisha kioo cha gari ya mteja, kwenye kituo cha Total cha Mlimani city, jijini Dar es Salaam, jana, wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Huduma kwa Wateja iliyozinduliwa mwanzoni mwa wiki. Menejimenti na wafanyakazi wa kampuni hiyo, wamejiunga na wafanyakazi wa vituo vya mafuta kuhudumia wateja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaonya biashara vyuma chakavu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, ameagiza waliobainika kusafirisha vyuma chakavu ambavyo ni miundombinu ya majitaka na majisafi, wachunguzwe kujua walikovitoa ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

Pia, ametahadharisha kuwa yeyote atakayekutwa amebeba, kuhifadhi, kuuza au kusafirisha vyuma chakavu bila kibali, atachukuliwa hatua za kisheria.

Simbachawene alitoa agizo hilo jana ofisini kwake jijini Dodoma alipoliagiza Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (Nemc) kuichukulia hatua Kampuni ya Press Freight Tanzania Ltd (Wakala wa Usafirishaji) kwa kusafirisha makontena ya vyuma chakavu, mali ya kampuni ya Eco Steel ambayo hayakuwa na kibali na iliyasafirisha licha ya katazo lake.

Alisema katika kampuni nane zilizokuwa zinamiliki makontena 147 yaliyokuwa Dar es Salaam, baada ya ukaguzi kampuni nne zilisema uongo kwa kuwa ziliweka vitu visivyoruhusiwa kwa mujibu wa sheria.

Alisema kuna haja kufanya uchunguzi kubaini walikovitoa vitu hivyo visivyoruhusiwa kusafirishwa kwenda nje ya nchi.

"Kwa kampuni ya Eco Steel Limited na Mahavir Implex Tanzania Limited ambazo zilikiuka agizo langu la kusafirisha taka hatarishi kwenda nje ya nchi, naagiza taasisi zilizowapa leseni, yaani Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) wazifutie leseni kwani zimekiuka sheria ya mazingira ya vibali vya kukusanya na kusafirisha taka hatarishi ndani ya nchi.

Waziri huyo pia alizitaka kampuni nne zilizodanganya na zilizoonekana kuwa na upungufu mdogo, kwenda Nemc kwa ajili ya kufuata utaratibu kwa kulipa faini na kuanza upya mchakato wa kupata kibali cha waziri cha kusafirisha kwenda nje ya nchi taka hatarishi.

Simbachawene alisema kampuni nne zilizokutwa na makosa, zinapaswa kulipa faini ya Sh. 460,000 kwa kila kontena lililokaguliwa na wataalamu na makosa mengine yatozwe faini kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004.

Alisema biashara zote zinazohusiana na ukusanyaji wa vyuma chakavu kwa mtu mmoja mmoja, kwa ngazi za chini, zitasimamiwa na serikali za mitaa huku akiagiza utekelezaji huo kuanza mara moja.

Oktoba 16, mwaka huu, makontena 142 yanayomilikiwa na kampuni mbalimbali yalifanyiwa ukaguzi na taarifa kuwasilishwa na timu ya kitaifa ya ukaguzi na taarifa kuonyesha uwapo wa ukiukwaji wa sheria na kanuni zinazosimamia na kudhibiti taka zenye madhara nchini.



Meneja wa Kiwanda cha Tanzania Distilleries Ltd (TDL), Aranyaeli Ayo (kushoto), akikabidhi msaada wa printa kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Kichanga ya wilayani Temeke, Mariam Mushikwa, kwa ajili ya kusaidia shughuli za ofisini katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Meneja Mauzo na Usambazaji wa TDL, Mwesige Mchuruza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bunduki yafyatuka, risasi yaua mtuhumiwa ujambazi

**Na Gurian Adolf, KATAVI**

MKAZI wa Kijiji cha Magula, Kata ya Machimboni, Tarafa ya Nsimbo wilayani Mpanda Mkoa wa Katavi, Masoud Mtegitwe (27), anayedaiwa ni jambazi, amekufa papo hapo baada ya risasi kufyatuka kutoka kwenye bunduki aliyokuwa ameibeba mwenzake.

Mwenzake ambaye anadaiwa kuwa ni jambazi, inadaiwa kutokuwa na utaalamu wa kubeba silaha.

Tukio hilo lilitokea Novemba 11 saa 3 :00 za usiku wakati watu hao wakiwa wanatembea kijijini wakiwa na mfuko wa aina ya sulphate uliokuwa na bunduki ndani yake aina ya AK 47 namba TX 4039, magazini moja yenye risasi tisa, ganda moja la risasi na kofia ngumu ya pikipiki.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Benjamin Kuzaga, watu hao walikuwa wanakwenda kusikojulikana wakiwa wamebeba bunduki hiyo kwenye mfuko, ndipo risasi zilipofyatuka na kumuua Mtegitwe kisha aliyekuwa amebeba mzigo kutokomea kusikojulikana.

Kamanda huyo alisema kuwa chanzo cha tukio hilo bado kinachunguzwa, na kuwa katika upelelezi wa awali inaonyesha watu hao walikuwa majambazi.

Alisema msako mkali unaendelea kwa kushirikiana na wananchi pamoja na viongozi wa eneo husika ili kuhakikisha kuwa mtu aliyekimbia anapatikana.

Distributed via ippmedia




# JKCI yaokoa bil. 89/- matibabu moyo ndani

INATOKA UK. 2

'pacemaker', 'high power device', 'stent', 'device closure' na valvu. Vifaa hivi tunaviagiza nje ya nchi kwani havipatikani nchini", alisema Prof. Janabi.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa kwa kipindi cha miaka minne, wamewaona wagonjwa 300,836 kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani na nchi jirani kama vile Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Malawi, Ethiopia, Zambia, Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda na Visiwa vya Comoro.

"Jambo la kufurahia ni kuwa tumefanikiwa kuokoa maisha ya watu ambao tumewatibu na hivi sasa wanaendelea na majukumu yao ya kazi za kila siku. Kwa kipindi cha miaka minne tulilaza wagonjwa 14,960, tumefanya upasuaji wa bila kufungua kifua kwa kutumia mtambo wa Cathlab kwa wagonjwa 4,207 na upasuaji wa kufungua kifua na kusimamisha moyo kwa wagonjwa 1,747," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ambayo inamaliza muda wake Prof. William Mahalu, alipongeza uongozi wa taasisi hiyo pamoja na wafanyakazi kutokana na huduma za matibabu ya moyo wanazozitoa kwa wagonjwa wanaowatibu.

Prof. Mahalu ambaye ni mmoja wa madaktari bingwa wa upasuaji wa moyo na mishipa ya damu wa kwanza nchini, alisema anamaliza muda wa mwenyekiti wa bodi hiyo huku ndoto yake ya kuona Tanzania inakuwa na hospitali ya matibabu ya moyo ikiwa imetimia.

# Mkapa: Niliruhusu mawaziri wanikosoe

INATOKA UK. 2

**MAWAZIRI KUJITUMBUA**

Katika ukurasa wa 119, Mkapa anaeleza namna alivyowalazimisha mawaziri wake wanne kujiuzulu nafasi zao, lakini baadaye alimrejesha kazini mmoja wao baada ya uchunguzi wa kina kubaini hakuhusika na jambo lililomlazimu kuachia madaraka.

Alisema mawaziri watatu walijiuzulu wakati wa kipindi cha kwanza cha urais wake ambao ni pamoja na aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Juma Ngasongwa, ambaye baadaye alirejeshwa kazini baada ya uchunguzi kuonyesha hakuwa na makosa.

"Nilimtaka Waziri wa Fedha, Simon Mbilinyi na naibu wake, Kilonsi Mporogomi, kuachia madaraka kutokana na mgogoro wa mara kwa mara baina yao, jambo ambalo sikuruhusu lijitokeze katika kipindi tulichokuwa tunajenga uchumi imara wa nchi," anasema Mkapa.

Anabainisha kuwa Waziri wa Viwanda na Uchumi, Iddi Simba, alijiuzulu mwenyewe katika kipindi cha pili cha uongozi wake, kutokana na masuala ya biashara ambayo alikuwa na maslahi binafsi na yaligongana na uongozi wake.

Anamtaja waziri mwingine aliyelazimika 'kujitumbua' kuwa ni aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Hassy Kitine, aliyeachia madaraka baada ya kubainika kuwa mkewe alifanya udanganyifu wa gharama za matibabu alizotumia akiwa Marekani.

**UTEUZI WA GAVANA**

Katika kitabu chake hicho alichokipa jina la 'My Life, My Purpose' (Maisha Yangu, Kusudi Langu), Mkapa pia anaeleza namna ilivyokuwa ngumu kwake kuteua Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

"Ilibidi nimuulize Mwalimu (Nyerere). Nilimfikiria mtu ambaye hakumfikiria kwa angekuwa ni gavana. (Mwalimu) aliniuliza 'natambua unataka kuteua mtu mwingine kushika nafasi ya gavana, unaweza kunipa jina lake?' Nilijibu kuwa ni Daudi Balali, ndiye ninayemtaka.

"(Mwalimu) alinijibu 'afadhali maana nilielezwa ulikuwa unamteua mtu mwingine', na huo ukawa mwisho wa mazungumzo yetu siku hiyo," Mkapa anasema.

**MISHAHARA SERIKALINI**

Mkapa pia anaeleza namna uongozi wake ulivyokumbana na vikwazo katika kulipa mishahara ya watumishi wa umma, akibainisha kuwa wakati anaingia madarakani, mishahara ilikuwa hailipwi kwa wakati na mara nyingi watumishi walikuwa wanapewa stahiki zao hizo wiki la kwanza la mwezi uliofuata.

Anaeleza zaidi kuwa baada ya kuapishwa Novemba 23, 1995, siku iliyofuata, Katibu Mkuu Kiongozi, Matern Lumbanga, walikutana kwa mazungumzo naye na kuelezwa ukweli ambao anakiri ulimshtua kutokana na kubaini kwamba nchi ilikuwa katika hali mbaya kiuchumi.

Mkapa anaeleza katika kitabu chake hicho kuwa 'huwezi kujua ukubwa wa tatizo linaloikabili nchi hadi unaposhika madaraka makubwa ya kufanya uamuzi'.

"Muda mfupi baada ya kuwauliza baadhi ya wafanyakazi wa Ikulu kama watumishi wa umma wamelipwa mishahara, waliniangalia kwa mshangao, 'unauliza kama mishahara imeshalipwa? Wakati mwingine hatuwalipi hadi wiki ya kwanza ya mwezi unafuata," anaeleza Mkapa.

Anasema aliwaambia watendaji wake hao kuwa jambo hilo ni fedheha na walipaswa kujipanga kulirekebisha kwa kuwa nchi ilikuwa inakwenda kuwa na vyanzo vipya vya mapato.

"Nataka tuanze kulipa mishahara kwa wakati, tunawezaje kuwa na serikali inayofanya kazi kama wafanyakazi hawalipwi mishahara kwa wakati?

"Kwa wakati huo, mfumuko wa bei ulikuwa wa asilimia 27.4. Nilibaini kulikuwa na tatizo kubwa uchumi kiasi cha ukusanyaji wa mapato kuwa mgumu," anasema Mkapa.

# Programu ubia kilimo ilivyoongeza mavuno

**Na Mwandishi Wetu**

PROGRAMU ya Ubia wa Kilimo (TAP II) imewesha wakulima kuongeza mazao hasa ya mpunga katika mikoa ya Katavi na Rukwa.

Imeelezwa kuwa kwa Wilaya ya Mpanda mkoani Katavi, mavuno ya zao hilo yameongezeka.

Mavuno hayo yameongezeka kutoka gunia 18 kwa hekari moja hadi gunia 28 kwa hekari, huku kwa Sumbawanga mkulima wa mpunga akiwa na uhakika wa kuvuna gunia 25 kwa ekari moja tofauti na gunia 15 za awali.

Hayo yalibainishwa na Juma Mkumba, mkulima kutoka kijiji cha Ng'ongo wilayani Sumbawanga mkoani Rukwa. "Nimeshangazwa sana na uzuri wa teknolojia ya kilimo shadidi kwa sababu inakuwezesha ufanye kilimo kwa misimu yote ya kilimo katika mwaka na huongeza Kipato cha kaya kwa ukubwa sana kwa sababu inaweza kufanyika wakati wote" alisema.

Alisema kuwa kabla ya 2014 wakulima wengi hawakuwa na muamko kuhusu matumizi sahihi ya mbolea, lakini serikali ilileta mbolea ya ruzuku ambayo ilipatikana kupitia mawakala.

Baada ya kuanza kwa utekelezaji wa awamu ya pili ya TAP, msisitizo mkubwa uliwekwa kwenye matumizi sahihi ya pembejeo na wakulima walipata nguvu ya pamoja katika ununuzi wa mbolea kupitia vikundi vyao vya kilimo (AMCOS).

"Kulikuwa na changamoto ya upatikanaji wa pembejeo ikiwamo mbolea, kwa sababu iliyokuwa ikipatikana ilikuwa ikiuzwa kwa gharama kubwa sana, hivyo kusababisha matumizi kuwa madogo licha ya uelewa wa wakulima kuhusu matumizi ya mbolea kuwa juu" alisema Mkumba.

"Tulifanya zoezi la kuandaa mashamba darasa kwanza, na hii ilihusisha wakulima viongozi katika kila kijiji tuliamini wao wakielewa vizuri itakuwa rahisi kufikisha teknolojia hii kwa wakulima wenzao katika kila kijiji na tuliamini hi ndo itakuwa njia bora zaidi ya kufisha teknlojia hii kwa wakulima wote," alisema msimamizi wa TAP Awamu ya Pili katika mikoa wa Rukwa na Katavi, Wilison Erenest Loth. "Vijiji vya Msia, Ng'ongo, Mfinga, Kisa, Mpanda, Uruwila, Kilida na Nankanga vilikuwa vya kwanza kujifunza teknolojia hii na lengo letu kuu ilikuwa kuitumia elimu hiyo kwa ajili ya kuendeleza na kukuza vipato vyao kutokana na zao la Kilimo cha mpunga," alisema Loth.

"Mashamba hayo yamekua na mafanikio makubwa kwani yameonyesha waziwazi namna Kilimo shadidi cha mpunga kinaweza kuongeza kiwango cha mavuno na kuwafanya wakulima wasitegemee sana misimu ya mvua tu bali wawe na uwezo wa kulima mpunga hata kipindi cha kiangazi kwa sababu teknolojia hii inaweza kuhimili vipindi vyote," alisema.

Baraza la kilimo Tanzania (ACT) kama chombo kilele cha wadau wa Sekta Binafsi ya Kilimo Tanzania lilisaini makubaliano ya kushirikiana kuendeleza Sekta ya Kilimo nchini kwa kutekeleza Programu ya Ubia wa Kilimo Tanzania na Shirika la Maendeleo la nchini Norway (NORAD) kwa vipindi viwili tofauti,

Makubaliano ya kwanza yalikuwa ni utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazohusisha mfumo wa usambazaji wa Pembejeo vijijini huku makubaliano ya pili yakilenga kusaidia teknolojia mbalimbali za Kilimo ikiwamo kilimo shadidi kwa zao la mpunga ikiwa ni pamoja na teknolojia ya kilimo hifadhi kwa zao la mahindi ambapo teknolojia zote zililenga kutekelezwa katika Wilaya 29 nchini. Dhumuni la Programu ilikuwa ni kusukuma maendeleo ya Kilimo katika maeneo ambayo Program hii inafanya kazi kwa kuhusianisha na maendeleo yaliyofikiwa katika Mpango wa kwanza wa TAP I.



Kijana akipepeta mchele na kutoa uchafu ili kuuweka kwenye hali ya usafi wakati akisubiri wateja, katika eneo la Mburahati, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# DC aifagilia TRA elimu ya mlipakodi

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani, Juma Njwayo, amepongeza juhudi zinazofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) za kutoa elimu ya kodi kwa kuwafuata wafanyabiashara katika maeneo yao.

Amesema aina hiyo ya utoaji elimu ya kodi kwa kuwafuata wafanyabiashara kutaongeza ari ya ulipaji kodi miongoni mwa wafanyabiashara na walipakodi wengine siyo tu katika Wilaya ya Rufiji bali hata kwa Watanzania wote.

"Niwapongeze sana TRA kwa kuamua kufanya wiki ya elimu na huduma kwa walipakodi katika wilaya yetu, naamini wana-Rufiji tutafaidika na elimu hii na mapato yataongezeka," alisema Njwayo.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara na wananchi wa Wilaya ya Rufiji kutumia fursa hiyo kufahamu mambo yanayohusu ulipaji kodi ili walipe kodi kwa hiari na kwa wakati, na kuiwezesha serikali kutekeleza miradi mikubwa yenye tija kwa Taifa.

"Sote tunashuhudia jinsi Rais John Magufuli anavyotekeleza miradi mikubwa kama huu wa kufua umeme wa Nyerere tena upo wilayani kwetu, kwa hiyo tutumie fursa ya elimu ya kodi na kila mmoja aone ana wajibu wa kulipa kodi kwa hiari ili tupate maendeleo zaidi," alisema Njwayo.

Naye Meneja wa Huduma kwa Mlipakodi wa TRA, Honesta Ndunguru, aliushukuru uongozi wa Wilaya ya Rufiji kwa ushirikiano walioonyesha, na kueleza kuwa TRA itahakikisha inafika katika sehemu zote muhimu zenye wafanyabiashara na kuwasajili kuwa walipakodi na kuwapatia cheti cha utambulisho wa mlipakodi (TIN).

"Tutatoa TIN kwa kila anayestahili kupata kwa ajili kufanya biashara au kupata huduma zingine kama vile leseni ya udereva," alisema Ndunguru.

# Wanufaika Tasaf kuingia viwanda

**Na Elizabeth Zaya**

HALMASHAURI ya Ludewa mkoani Njombe, imeanza mpango wa kuwawezesha wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya masikini wanaowezeshwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) kuanzisha viwanda vidogo

Akizungumza mbele ya maofisa wa Tasaf, Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Sunday Deogratius, alisema wameamua kuanza kuwapa elimu ya kuanzisha viwanda hivyo kutokana na mwitiko mkubwa walionao katika kuanzisha miradi mbalimbali

Alisema wanufaika wa Tasaf tangu waanze kuwezeshwa na kupatiwa elimu ya kuanzisha vikundi vidogo vya kujiwekea akiba na kukopa wameanzisha miradi mingi ambayo imefikia wakati wanatakiwa kuwezeshwa zaidi kuingia katika uchumi wa viwanda

"Sisi hapa kwetu Ludewa tumepata manufaa makubwa sana kupitia mpango huu wa Tasaf, familia nyingi zilizokuwa zinakabiliwa na umasikini na wakati mwingine watoto kushindwa kwenda shuleni kwa ajili ya njaa sasa hivi wanakwenda vizuri, wana afya njema na wanafanya vizuri kwenye masomo, kwa kweli tunaishukuru sana serikali kupitia mpango wake huu," alisema Deogratius

"Ukienda kuwatembelea unashuhudia mifugo mingi waliyofuga, wanalima, kwa hiyo tumeona kwamba na wao kupitia vikundi vyao hivyo na miradi yao hiyo, waanze kupanua mawazo ya kuanzisha viwanda vidogo, wanunue mashine ndogo za kutengeneza juisi za matunda mbalimbali na kuzifungasha vizuri na kusambaza katika masoko, maduka makubwa na madogo."

Alisema katika halmashauri hiyo jumla ya kaya 232 zinazowezeshwa na Tasaf zimeanzisha miradi ya ufugaji huku vikundi 100 vya kuweka akiba vimeanzishwa.

Pia alisema kaya 1,543 kati ya 3146 zimekarabatiwa makazi yao, huku kaya 1086 zimejengewa nyumba mpya na kwamba kaya 2736 kati ya 3146 zimejiunga na bima ya afya

Deogratous alisema jumla ya miradi 35 ya Tasaf katika Halmashauri hiyo imetekelezwa ikiwamo katika sekta ya afya, elimu, miundombinu na ufugaji

## Serikali yatambua shida maji Kilindi

WIZARA ya Maji imekiri kutambua tatizo kubwa la huduma ya maji linaloikabili wilaya ya Kilindi kutokana na kutokuwa na mito wala maziwa yanayotumika kwa ajili ya shughuli za binadamu na wanyama kwa kipindi cha mwaka mzima.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Jumaa Aweso, alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kilindi (CCM), Omary Kigua.

Katika swali lake, Kigua alisema Wilaya ya Kilindi yenye Vitongoji 611 na Vijiji 102 haina mto wala ziwa na kuhoji serikali haioni umuhimu wa kupatia wilaya hiyo mradi mkubwa wa maji kutoka Mto Pangani ili kutatua changamoto ya maji.

Akijibu swali hilo, Aweso alikiri serikali kutambua tatizo hilo na kwamba vyanzo vikuu vya maji katika Halmashauri hiyo ni maji yaliyopo chini ya ardhi.

Hata hivyo, alisema katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali ilichimba visima vinne katika Miji ya Songe na Bokwa ambapo katika Mji wa Bokwa tayari huduma ya maji inapatikana kwa wananchi waishio maeneo hayo.

Aidha, alisema katika Mji wa Songe tayari usanifu umekamilika ili kujenga miundombinu ya usambazaji maji.

"Kwa upande wa huduma ya maji vijijini kuna visima vifupi 67 na visima virefu 13 vinavyotoa huduma ya maji kwa maeneo mbalimbali ya vijiji pamoja na malambo 12 ya maji,"alisema.

Alisema kwa sasa serikali inakarabati mradi mkubwa wa Kitaifa wa HTM unaotoa maji Mto Pangani ili kuendelea kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa Wilaya ya Handeni na baadhi ya vijiji vya Wilaya ya Korogwe.

"Serikali itafanya tathmini ya kina kuangalia uwezekano wa ukarabati wa mradi huo endapo baadaye utaweza kuwanufaisha wananchi wanaoishi Wilaya ya Kilindi," alisema.

# Waliolipwa fidia Geita 2013 kupisha mgodi kuhamishwa

OFISI ya Mkuu wa Mkoa wa Geita imeagizwa kuwahamisha wananchi 155 walio karibu na mgodi wa GGM waliolipwa fidia mwaka 2013 ili kupisha shughuli za uchimbaji.

Agizo hilo lilitolewa jana na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Upendo Peneza.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema wananchi wa maeneo ya Katoma Kompaundi, Nyakabale wameathirika sana na shughuli za mgodi na serikali ilikwishatoa maelekezo kwamba wananchi wa maeneo hayo wahamishwe. "Je, ni lini sasa wananchi hao watahamishwa?" alihoji Akijibu, Waitara alisema Ofisi hiyo iwahamishe wananchi hao kwa kuwa wanapaswa kuachia maeneo hayo yaliyofidiwa ili kupisha shughuli za uchimbaji. "Naielekeza Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Geita kusimamia zoezi la kuwahamisha wananchi hao," alisema.

Awali, Waitara alifafanua kuwa kwa mujibu wa Kifungu cha 95(b) cha Sheria ya Madini, mgodi unapaswa kulipa fidia kwa wananchi wanaomiliki maeneo yanayozunguka eneo la uchimbaji lenye umbali wa mita 200.

"Hata hivyo, mwaka 2013 Mgodi wa GGM ulilipa fidia kwa wananchi walioko katika eneo lenye kipenyo cha mita 500 katika mitaa ya Katoma Kompaundi na Nyamalembo ambapo wananchi 155 walilipwa kiasi cha Sh. bilioni 6.83," alisema.

Aidha, alisema kwa upande wa Nyakabale, Mgodi haukuwalipa wananchi fidia kwa kuwa maeneo yao yapo zaidi ya umbali wa mita 200 kutoka eneo la Mgodi.



Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge Rafiki wa Mazingira (TAPAFE), Jitu Soni, akitoa maelezo ya utangulizi, kuhusiana na mpango kazi wa chama hicho, kwa Spika wa Bunge, Job Ndugai (kulia kwake), kabla ya kuuzindua rasmi mpango huo katika mkutano uliofanyika kwenye ukumbi wa Msekwa, Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: BUNGE**

# Sekta ya viwanda yapaisha ajira

BUNGE limeelezwa kuwa ajira katika Sekta ya viwanda imeongezeka kutoka watu 254,786 mwaka 2015 hadi kufikia watu 306,180 mwaka 2018.

Hayo yalielezwa jana na Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CUF), Rukia Kassim Ahmed.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema Rais alisema kwamba ifikapo 2020 asilimia 40 ya watu wawe wameajiriwa katika sekta ya Viwanda na sasa hivi ni mwaka 2019.

"Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza kauli hiyo kwa wakati?" alihoji.

Akijibu, Waziri Bashungwa alisema idadi hiyo ni kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwenye Kitabu cha Hali ya Uchumi cha mwaka 2018 zinaonyesha kuwa ni ongezeko la watu 51,395 sawa na asilimia 20.17.

"Ajira hizo ni za moja kwa moja mbali na zile zinazotokana na mnyororo mzima wa thamani kama vile usafirishaji, huduma za vyakula na malazi, ni imani yangu kuwa ajira zitaendelea kuongezeka kama ilivyokusudiwa," alisema.

Aidha, alisema ili kuweza kuongeza kasi ya ajira kutokana na mchango wa Sekta ya Viwanda, Wizara hiyo imeelekeza nguvu kubwa katika uhamasishaji wa uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa katika mnyororo wa thamani.

"Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi pamoja na kubuni mikakati mbalimbali ili kuwezesha wajasiliamali wa ngazi zote na hivyo kuchangia ipasavyo katika kuongeza ajira," alisema.

Vile vile, Bashungwa alisema katika mwaka 2018, kasi ya ukuaji wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani ilikuwa asilimia 8.3 ikilinganishwa na asilimia 8.2 mwaka 2017.

"Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa baadhi ya bidhaa zikiwemo bidhaa za vyakula, vinywaji baridi, saruji, unga wa ngano, chuma, na rangi sambamba na kuongezeka kwa hamasa ya matumizi ya bidhaa za ndani," alisema.

Waziri huyo alisema mchango wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani katika Pato la Taifa uliongezeka na kuwa asilimia 8.1 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 7.7 mwaka 2017.

"Mipango iliyowekwa na Serikali katika kuhakikisha kuwa mchango wa sekta ya viwanda katika ajira unaongezeka kama iliyokusudiwa ni pamoja na kuvutia wawekezaji na kuhamasisha Sekta Binafsi kuanzisha na kuendeleza viwanda vinavyotumia malighafi za hapa nchini," alisema.

Pia alisema kuhamasisha uanzishaji na maendeleo ya viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati, kuendeleza maeneo yaliyobainishwa ya viwanda katika mikoa yote na

kuendeleza maeneo maalumu ya uwekezaji (EPZ & SEZ) pamoja na kongano za viwanda (industrial clusters), kuendeleza eneo la viwanda la TAMCO Kibaha, kuendeleza mitaa/maeneo ya viwanda vya Sido.

"Kadhalika, kuendeleza Kanda Kuu za Uchumi (Ruvuma, Tanga, Kigoma na Manyoni); Bagamoyo SEZ & BMSEZ; Kurasini Logistic Centre na Kigamboni Industrial Park; na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji," alisema.

Bashungwa alisema wizara imeweka msukumo wa pekee katika kuhamasisha ujenzi wa sekta Binafsi ya Kitanzania iliyo imara ili iweze kushiriki na kuchangia ipasavyo katika ujenzi wa uchumi wa viwanda na hatimaye kushiriki ipasavyo katika kutoa ajira.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

## HABARI ARUSHA



Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Longido, Ezekiel Mollel, akiongea na wanachama wa chama hicho, katika kijiji cha Ngoswak, wilayani humo, mkoani Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Tanzania, Uganda zatakiwa NIT

**Na Allan Isack,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, amezitaka Mamlaka za Anga za nchi ya Tanzania na Uganda kukiimarisha Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), ili kupunguza gharama za kuwapeleka marubani wataalamu kujifunza nchi za nje.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa safari ya ndege ya shirika la ndege la Uganda kutoka Entebbe kwenda Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro (KIA), Nditiye alisema endapo nchi hizo mbili zitaimarisha chuo cha mafunzo ya urubani watapunguza gharama za kuwapeleka wataalamu hao kujifunza nje ya nchi.

Alisema chuo hicho, kikikamilika kitatoa fursa kwa wataalamu na wanafunzi kutoka nchi za ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kujifunza badala ya kwenda katika nchi za Ulaya na Marekani.

"Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekuwa zikiingia gharama kubwa ya kuwapeleka wataalamu na wanafunzi kujifunza nje ya Bara la Afrika," alisema Nditiye. "Tumekuwa tukipata changamoto kubwa ya kuwapeleka marubani wetu nje ya Afrika kupata mafunzo, lakini tukiimarisha chuo chetu cha taifa cha usafirishaji kwa kushirikiana na mamlaka hizi mbili na wadau mbalimbali tutawapata wataalamu bora wanaotakiwa kwa maslahi ya nchi zetu," alisema Nditiye.

Alisema serikali inakihitaji chuo hicho, kifanye vizuri ili kuharakisha maendeleo kwa haraka na kupunguza gharama za uendeshaji kwa mashirika ya ndege.

Waziri wa Usafiri, Mawasiliano na Uchukuzi, Aggrey Bagire, alisema shirika hilo halijaja Tanzania kwa ajili ya kushindana na mashirika yaliyopo bali ni kuungana nayo kutoa huduma za usafiri wa anga ambazo ni muhimu," alisema Bagire.

Balozi wa Uganda nchini, Richard Kabonero, alisema kuzinduliwa kwa safari hiyo, kutaongeza ushirikiano wa mataifa haya mawili kwa kurahisisha na kukuza uchumi wa nchi zote mbili.

Mwenyekiti wa Bodi wa Shirika la Ndege la Uganda, Pereza Ahabwe, alisema shirika hilo, limetengeneza sera ambazo zitakuwa rafiki katika ushindani wa kibiashara, lengo likiwa ni kutoa huduma bora katika usafiri wa anga.

# Biteko amtumbua ofisa madini

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, amemtumbua aliyekuwa Ofisa Mfawidhi wa Madini Mkoa wa Arusha, Robert Erick, kwa kushindwa kusimamia ipasavyo majukumu yake ya kazi.

Ofisa madini huyo, anadaiwa kuwaachia wafanyabiashara wakubwa wa madini mkoani Arusha kufanya biashara maofisini mwao tofauti na maelekezo ya serikali iliyowataka wafanye biashara hiyo kwenye soko la madini.

Biteko alisema hayo katika mkutano wa hadhara wa wafanyabiashara wakubwa na wadogo wa madini katika ziara yake ya kushtukiza kufika jijini Arusha na kutembelea soko hilo, lililopo eneo la Uzunguni.

Biteko alikuta ofisi kumi zikiwa wazi bila kufanya biashara wakati soko hilo, likiwa na idadi ya ofisi za wafanyabiashara wakubwa 40, lakini kwa zaidi ya miezi minne hawajahamia katika ofisi hizo.

Alisema jukumu la kusimamia biashara ndani ya soko hilo, na kuchukuwa hatua kwa wafanyabiashara wenye madini majumbani lilitakiwa kufanywa na ofisa huyo, lakini ameshangaa kuona kazi hiyo inafanywa na waziri hatua ambayo haikubaliki kabisa.

Waziri alisema biashara ya madini ya Tanzanite mkoani Arusha, imeshuka kwa asilimia kubwa na wanaofanya biashara hiyo, kushuka wako lakini hawajachukuliwi hatua.

Alisema kutokana na hali hiyo, alimwagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Prof. Saimoni Msangila, kumwondoa kazini ofisa huyo kwani kwa kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kila siku. Alisema hakuna sababu za msingi kwa wafanyabiashara wakubwa wa madini humo, kushindwa kufanya biashara katika soko la madini lililotengwa na serikali na badala yake wafanyabiashara hao wanafanya biashara katika ofisi zao.

Alisema yeye anasimamia sheria na kanuni za madini ili kuhakikisha sheria hizo, zinatekelezwa kwa wafanyabiashara wote nchini.

Alisema wafanyabiashara wakubwa waliomba mwezi mmoja kufanya biashara ndani ya soko hilo na wizara iliwaongeza muda waliohitaji lakini hadi sasa ni zaidi ya miezi minne hakuna mfanyabiashara aliyefika kufika kufanya biashara katika soko hilo.

Biteko alisema ana taarifa za uhakika baadhi ya wafanyabiashara wakubwa 97, wana ofisi za madini Arusha na Jiji la Nairobi, na wanafanya ujanja ili wafanye biashara hiyo kwa njia haramu na kuikosesha serikali mapato.

"Nataka kuanzia Novemba 18, mwaka huu siku ya Jumatatu wafanyabiashara wa madini wakubwa kwa wadogo kila mmoja afanye biashara ndani ya soko la madini na sio mtaani," alisema Biteko.

Akizungumzia suala hilo, wafanyabiashara wadogo wa madini (Broker's), alisema ofisi yao ina idadi ya wafanyabiashara wenye leseni 263, lakini wanaofanya biashara hiyo mtaani 1,300, lakini zaidi ya wafanyabiashara 1037, wanafanya biashara bila ya leseni na ofisa madini Mkoa wa Arusha anawafahamu na alishindwa kusimamia majukumu yake ya kazi.

## Ombi kwa serikali kandarasi kwa wazawa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SERIKALI imeshauriwa kuwapatia kazi za ukandarasi wazawa kutekeleza miradi mbalimbali badala ya kutoa kandarasi hizo, kwa makandarasi kutoka nje ya nchi.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Macleo Electrical Contractors Ltd, Elineema Kileo, wakati akizungumza kwa niaba ya Mbunge wa Arumeru Mashariki, John Pallagyo, wakati wa mahafali ya 22, ya Chuo cha Ufundi cha Shirika la Mapadri wa Roho Mtakatifu Tengeru Arusha, ambapo jumla ya wanafunzi 27 walihitimu.


Alisema serikali inapaswa kutoa fursa ya tenda za miradi mbalimbali kwa makandarasi wazawa ili fedha hizo ziweze kubaki hapa nchini ambapo itaongeza kiwango cha ulipaji wa kodi. Aliongeza kuwa kitendo cha kuwapatia kazi makandarasi wa nje fedha hizo zinaendelea kuwanufaisha wao, wakati zingeachwa hapa nchini zikiendeleza dhana ya uchumi wa viwanda, kwani kuna asilimia kubwa ya makandarasi wenye uwezo wa kutekeleza miradi hiyo na sio wale kutoka nje ya nchi tu.

"Tunaiomba serikali wawape miradi makandarasi wazawa, kwani hata sisi tuna uwezo mkubwa sana wa kutekeleza miradi tena wapo makini wanauwezo kutoa ajira kwa wazawa wengine tena kwa kiwango kikubwa," alisema.

Mkurugenzi wa chuo hicho, Padri Emmanuel Kway, alisema chuo kilianzishwa mwaka 1994, kwa lengo la kuwatayarisha vijana katika fani mbalimbali za ufundi na kukuza vipaji vyao vya ufundi ili waweze kujiajiri badala ya kusubiri kuajiriwa na serikali na kampuni binafsi.

Alisema chuo kinakabiliwa na tatizo la majisafi na salama kwa matumizi ya binadamu, kwa kuwa sasa chuo hicho, kinatumia maji ya kisima.

Alisema pia wanakabiliwa na tatizo la eneo la kusaga na kukoboa nafaka kwa chakula cha wanachuo jambo ambalo linawapoteza muda wanafunzi kwenda mashine nje ya chuo.





## Ustawi wa Jamii wataka ushirikiano

**Na Mary Mosha,** KILIMANJARO

OFISA Ustawi wa Jamii wa Manispaa ya Moshi, amesema ili kutokomeza vitendo vya kikatili kwa wanawake na watoto, serikali inashirikiana na mashirika na taasisi mbalimbali ngazi ya kata hadi taifa kukabiliana na janga hilo.

"Serikali ikiwa ni mwangalizi inafanyakazi kuanzia ngazi za mtaa, kata, wilaya, mkoa, mpaka taifa na mashirika au taasisi zisizo za serikali kwani hawa ndiyo wamekuwa viunganishi kati ya wananchi na sisi katika utekelezaji wa mkakati yetu ya kutokomeza ukatili kwa wanawake na watoto vinatokomezwa," alisema, Mohammed Seif, na wadau wengine walipozungumza na Nipashe.

Alisema kuwa kwa Mkoa wa Kilimanjaro, Shirika la NAFGEM kwa kushirikiana na wadau wengine limekuwa mstari wa mbele kuhamasisha wananchi kuwafichua wale wanaofanya vitendo vya ukatili na ukandamizaji. Seif alionya kuwa kutokana na vitendo hivyo kuhusisha zaidi ndugu wa damu inakuwa ni vigumu kupata taarifa hizo kwa kuwa watu huogopa kuwaripoti ndugu zao kwenye vyombo vya usalama.

Alisema, "mtu anafikiria labda ni bibi au shangazi yake amemkeketa binti, hawezi akaenda kumripoti kwa sababu atakuwa anafikiri kuwa anamfunga bibi yake, shangazi yake, kwa hiyo vimekuwa ni vya kulindana sana." Alitoa rai kwa jamii, wazazi na familia kutoa ushirikiano kwa serikali na mashirika hayo inapotokea kitendo cha kikatili kimeripotiwa. Aidha, Daktari Lengarivo Losari kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mawenzi, alisema kuwa mtu akifanyiwa ukeketaji kuna madhara mbalimbali ambayo anaweza kuyapata ikiwamo kupoteza damu nyingi na hata kupoteza maisha wakati wanapokeketwa.

Alisema kutokana na vitendo hivyo kutokufanyika kitaalamu kwa kuwa mangariba hutumia vifaa ambavyo havina usafi wala havijatasishwa upo uwezekano wa kupata Ukimwi na VVU hata homa ya ini.

"Wengine wanapata fistula kwa maana inawaathiri kwenye njia za mkojo na haja kubwa. Wanaumizwa na matatizo ya kisaikolojia na wakati mwingine wanapata vidonda, majipu kwa maana vifaa hivyo si visafi, lakini pia maumbile yao yanaharibiwa kwani wakati mwingine inahusisha kutoa baadhi ya sehemu za siri, "alisema Dk. Losari.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya NAFGEM (Network Against Female Genital Mutilation) Francis Roman, alisema kuwa ili kutokomeza vitendo vya kikatili kwa wanawake na watoto jamii inatakiwa kutoa ushirikiano kwa mashirika, taasisi na serikali.

Aidha, alisema kuwa ili kuhakikisha kuwa vitendo hivyo vinakwisha wamekuwa wakitoa elimu, ikiwamo kuwawezesha baadhi ya wanawake wanaokeketa kupata elimu ya ujasiriamali.



Mkurugenzi wa Uhusiano kwa Umma wa kampuni ya Bia ya Serengeti, John Wanyancha (kushoto), akizungumza na waendesha bodaboda mjini Moshi jana, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya 'Usinywe na Kuendesha' inayolenga kupambana na ajali za barabarani. Wengine ni Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Kilimanjaro, Zauda Mohamed (katikati) na Mratibu wa Mafunzo Ofisi ya Kikosi cha Usalama Barabarani mkoa huo, Inspekta Hamadi Hoza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Skimu umwagiliaji zakosa matunzo

Distributed via ippmedia

**Na Mary Mosha,** MOSHI

LICHA ya kuwapo kwa mabadiliko ya tabianchi na serikali kuhimiza kilimo cha umwagiliaji, imeelezwa kuwa pamoja na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kujenga miundombinu ya kilimo hicho, skimu zinazojengwa hazitunzwi na wananchi.

Baadhi ya miradi hiyo iliyojengwa kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA), imeshuhudia skimu hizo zikibomoka hivyo kukosa tija kwa wakulima na taifa.

Hayo yalisemwa jana mjini Moshi na Mhandisi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Kilimanjaro, Japheth Senyinah, alipozungumza na wanahabari.

Alisema uendeshaji na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji umekuwa hauridhishi kutokana na uelewa mdogo wa wakulima juu ya uendeshaji na matunzo yake.

Hali hiyo imepelekea skimu za umwagiliaji kukosa tija kutodumu muda mrefu licha ya kutumia gharama kubwa wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo.

"Wadau wote wanaohusika wanatakiwa kutoa elimu kwa wakulima mara kwa mara ili skimu hizo ziwe endelevu na kuleta tija, kuwa na uhakika wa chakula na kupunguza umaskini kuanzia ngazi ya familia hata taifa kwa," alisema.

Alieleza kuwa ni wajibu wa kila umoja wa umwagiliaji kuhakikisha unasimamia ukusanywaji wa asilimia tano ya mapato kwa kila mwanachama katika skimu kwa ajili ya shughuli za uendeshaji na matunzo ya miundombinu ili skimu ziwe endelevu kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Umwagiliaji Namba 5 ya Mwaka 2013.

"Wataalamu wa kilimo kuanzia ngazi ya skimu, kijiji, kata, wilaya na mkoa wana wajibu wa kuhakikisha utekelezaji wa sheria hii unazingatiwa ili kuleta tija kwenye skimu hizo ikiwa ni pamoja na matengenezo madogo na ya mara kwa mara," alisema. "Katika kutekeleza majukumu ya uendelezaji na utunzaji wa skimu za umwagiliaji ili ziwe endelevu, wataalamu kwa kushirikiana na wakulima wanatakiwa kufuata "Mwongozo wa Umwagiliaji au Comprehensive Guide Line (CGL)."

Aidha, mwanakijiji anayetumia skimu ya Mtambo, Jumanne Idd, alisema hakuna elimu ya kutosha juu ya utunzaji wa miundombinu inayotengwa na tume hiyo ya umwagiliaji.

"Wengi hatuna elimu ya kutosha juu ya matengenezo madogo yanayotakiwa kwenye skimu zetu. Kumbe yanatakiwa kufanywa na sisi kwa mujibu wa sheria. Tunahitaji elimu zaidi ili kuleta mabadiliko," alisema. Ofsa Umwagiliaji wa Wilaya ya Hai, John Chuwa, alisema mbali na kuwapo kwa changamoto hizo wanaendelea kutoa elimu kwa wakulima ili kuleta mabadiliko katika sekta ya kilimo.

## Wajumbe wa Bodi ya Ushirika watumbuliwa

**Na Mary Mosha,** HAI

BODI ya Ushirika ya Shamba la Lambo Estate, inayojumuisha vyama vya msingi vitatu Foo, Nronga na Machame Wari, imesimamishwa kazi baada ya kushindwa kuendeleza shamba hilo. Aidha, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, amemtaka Mrajisi wa Vyama vya Ushirika, kuteua bodi ya mpito kutoka miongoni mwa viongozi wa vyama hivyo vitatu.

Akitoa maagizo hayo jana, baada ya kufanya ziara katika shamba hilo, Mghwira alisema amelazimika kuvunja bodi na kuwataka kuunda nyingine ya mpito ambayo itasimamia hadi mkutano mkuu utakapofanyika.

"Tumefikia maamuzi hayo baada ya kubaini kuwa bodi hiyo ilishindwa kusimamia maendeleo ya shamba hilo na serikali ya mkoa imelihakiki na kubaini kuwa kuna kaya 65, ambazo tumezigawia ekari mbili kila moja ili ziendelea kulima," alisema.

Alisema, jumla ya kaya 64 zilizomo ndani ya shamba la Lambo Estate zilipewe ekari mbili kila kaya moja ambazo ni sawa na jumla ya kaya 130 ili wazitumie katika kilimo cha kujikimu kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2019/2020 na ugawaji huu utafanyika kila mwaka hadi hapo utaratibu wa uendeshaji wa shamba hilo utakapokamilika.

"Jumla ya ekari 26 kati ya 156 ambazo zitabaki baada ya mgao wa ekari mbili kwa kila kaya zilimwe na kaya hizo 65 kama shamba lao la ushirika hadi hapo utaratibu wa uwendeshaji wa shamba hilo utakapokamilika.

Wakati huo huo, Mkuu wa Mkoa alisitisha ukodishwaji wa shamba la ekari 656, kwa kampuni ya EPK mpaka ushahidi wa uridhishwaji juu ya uwepo wa kampuni hiyo inayotaka kuingia mkataba wa uendeshaji wa sehemu hiyo.

"Tumesitisha kwanza ili kujiridhishe kama hiyo EPK ni kampuni na kama ina uwezo wa kuendesha eneo hilo, pia ni chukue fursa hii kuwataka wataalamu wa ushirika ngazi ya wilaya na mkoa kufuata sheria na taratibu ili kuhakikisha tunajenga ushirika imara," alisema Dk. Mghwira.




Ukurasa 14

Mkurugenzi Ewura: Hawatuelewi tu, kigezo cha bei ya petroli hiki



Ukurasa 18

Waume waliotelekeza warudi kusikia 'nyumbani kumenoga'


# BUFE

Ijumaa Novemba 15, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




## Mkurugenzi anayeacha ofisi IMF 'atiririka' pesa mtandao kukubalika

Ukurasa 19



# Bosi Latra afunguka kuikabili bodaboda ni 'pasua kichwa'

**NA ANTHONY GERVAS**

BARABARA ni nyenzo muhimu katika maendeleo ya umma, ikishika sehemu ya tafsiri ya uchumi.

Ili iwe na manufaa, inapaswa kutumika kwa usalama. Hapo ndipo wataalamu wa usalama barabarani wanaitafsiri kwamba: "Ni mwingiliano salama kati ya watumiaji barabara, watembea kwa miguu na vyombo vya moto."

Vilevile kuna suala la kuwapo mazingira ya barabarani kwa maelewano, mfano taa nyekundu inapowaka inamsimamisha mtumiaji, kwani asipositmama, inaunda chanzo cha ajali kinachoishia katika madhara.

Hivyo, katika mfumo wa utumiaji wa barabara, unapaswa kuangukia katika maana 'salama.' Katika kuliangalia hilo na mengineyo, ndiyo serikali ikaunda chombo Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini (Latra).

Hata hivyo, kihistoria hilo ni zao jipya la iliyokuwa Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (Sumatra), iliyoanza baada ya serikali kujitoa katika utoaji huduma za kibiashara kuanzia

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

## Bandari Tanga katika safari ya kupanda na kushuka mapato

Ukurasa 20

BIASHARA

# Mkurugenzi Ewura: Hawatu tu, kigezo cha bei ya petrol

• Atangaza ushindi uchakachuaji mafuta • Waba kutoka 78% hadi 4% • Gharama uagizaji chini, ko




Kituo cha mafuta ambacho kimejengwa maeneo ya vijijini. **PICHA ZOTE: AUGUSTA NJOJI.**

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KWA muda mrefu kulikuwa na kilio cha uchakachuaji mafuta, hivyo kuhatarisha vyombo vya moto hususani magari.

Wamiliki wa magari wamekuwa wakipata hasara, ikiwamo injini za magari kuharibika kutokana na mikasa hiyo ya uchakachuaji mafuta.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji(EWURA), katika kuitafutia majibu, ilikuja na programu ya kuweka vinasaba kwenye mafuta, ikitajwa inapunguza uchakachuaji mafuta ya petroli na dizeli kutoka asilimia 78 kwa mwaka 2007 hadi asilimia nne mwaka huu

**MKURUGENZI**

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Ewura, Nzinyangwa Mchany, anasema walianzisha programu ya kuweka vinasaba kwenye mafuta yanayotumika nchini, ili kudhibiti uchakachuaji na ukwepaji kodi, ikiwamo kuweka mazingira ya ushindani na haki.

"Uchakachuaji wa mafuta ni changamoto kubwa hapa nchini na Ewura kwa kuliona hilo imepambana na kufanikiwa kupunguza uchakachuaji," anasema.

> **Madhara makubwa sana yanaweza kusababishwa na mlipuko wa gari linalobeba mafuta. Wananchi wanaombwa wasisogelee gari la mafuta, hasa linapopata ajali.**

Mchany anasema mwaka 2010 Chuo Kikuu Cha Dar-es-Salaam (UDSM), ilifanya utafiti kuhusu matumizi ya vinasaba na kubaini mwaka 2010 hadi 2013, kulikuwapo na ongezeko la mapato ya serikali kwa njia ya kodi, kiasi cha Sh. bilioni 466.50, manufaa yanayoendelea kupatikana.

**UTOAJI LESENI**

Kaimu Mkurugenzi huyo, anasema Ewura imetoa leseni 1,561 za biashara ya mafuta, zikiwamo za biashara ya mafuta 66, biashara ya mafuta rejareja 1,397 na leseni 19 kwa gesi ya kupika na vilainishi vya mitambo ni 56.

"Pamoja na mafanikio hayo, zipo changamoto mbalimbali ikiwamo kuchelewa kwa utoaji wa leseni za ujenzi wa vituo vya mafuta, wawekezaji kutokamilisha masharti ya leseni, hususan kibali cha matumizi ya ardhi na kibali cha mazingira,"anasema na kuongeza Ewura, inaendelea kutoa elimu ya vigezo vya kupata leseni.

**UAGIZAJI MAFUTA (BPS)**

Mchany anasema, Ewura kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati




Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Ewura, Nzinyangwa Mchany.

# uelewi i hiki

## na hujuma odi kibao






na Madini, iliandaa mfumo wa uagizaji wa pamoja (BPS) wa mafuta nchini, ambao utafiti uliofanywa na UDSM mwaka 2014, ulibaini kuokolewa Sh. bilioni 121.6 mwaka 2012 na 2013.

Pia, anasema utafiti ulibaini kupungua gharama za usafirishaji na mafuta kiwango cha 'premium' kiasi cha Sh. bilioni 81.9 katika kipindi cha miaka miwili.

Anaweka bayana faida iliyopatikana kwa kutumia mfumo wa pamoja wa BPS ni kurahisisha upatikanaji takwimu sahihi za ujazo wa mafuta yanayoingizwa nchini.

"Pia umerahisisha ukokotoaji wa bei za mafuta kwa mtindo ulio wazi zaidi na kurahisisha udhibiti wa ubora wa mafuta yanayoingizwa nchini kwa mfumo huo," anasema.

**UDHIBITI BEI**

Anasema Ewura ilianza kupanga bei mnamo Januari mwaka huu na utaratibu uliopo, bei hurekebishwa kila Jumatano ya kwanza ya mwezi.

"Matangazo ya bei mpya hufanywa kupitia kampuni ya mafuta, mamlaka mikoani na wilayani, magazeti na ukaguzi wa bei hufanywa mara kwa mara,"anasema

Ahadi ya mkurugenzi huyo ni kwamba, Ewura itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo, kwa ufafanuzi:

"Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi sahihi kuhusu ununuzi ya bidhaa za mafuta. Vituo vya mafuta vinahimizwa kuweka mabango ya bei yanayoonekana bayana na wateja wanahimizwa kununua mafuta kwenye bei ndogo kuchochea ushindani."

Kuhusu dai kutoka kwa umma, bei ya mafuta kutoshuka kwa bei yenye uwiano na ushukaji katika soko la dunia, anafafanua kuwa zinazotangazwa bei ya mafuta ghafi.

Anasema, bei za mafuta nchini hutegemea bei za mafuta masafi katika soko la dunia na gharama nyingine zisizoshuka, kama vile usafirishaji, faida za waagizaji mafuta, kodi za serikali, gharama za bandari na tozo za mamlaka mbalimbali.

**VITUO VIPYA VIJIJINI**

Anasema Ewura imeunda kanuni za ujenzi wa vituo vijijini na maeneo ya pembezoni na zilianza kutumika Julai mwaka 2015, zikiainisha masharti ya ujenzi wa vituo yaliyo nafuu, pia kwa kuzingatia matakwa ya usalama wa watu na mazingira.

Mchany anaahidi Ewura itaendelea kubuni njia za kuhakikisha biashara ya mafuta inaendeshwa kwa usalama, pasipo kukiuka matakwa ya ubora na usalama.

**TAHADHARI YAKE**

Kaimu Mkurugenzi huyo anasema, shughuli zote zinazohusu mafuta ya petrol, ni lazima zifanyike kwa umakini na uangalifu mkubwa, ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea.

"Ni muhimu kuzingatia na kufuata sheria, kanuni, viwango vya ubora na masharti ya leseni wakati wote. Tahadhari kubwa zinatakiwa kuchukuliwa katika shughuli za utunzaji, usafirishaji na utumiaji na uuzaji bidhaa za petroli.

" Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa maeneo yanayotumika yameruhusiwa kwa matumizi ya shughuli za mafuta, miundombinu kama vile magari ya kubebea bidhaa za petroli, vituo vya mafuta, maghala makubwa ya kuhifadhia, vijengwe au kuundwa kwa ubora unaotakiwa na kuendeshwa kwa kufuata kanuni za kiusalama, kiafya na kimazingira," anasisitiza

Pia, anakumbusha kwamba miundombinu yote inatakiwa kila wakati iwe na vifaa vya kuzima moto viwe vinavyofanya kazi, wafanyakazi wafundishwe kuvitumia vifaa hivyo, katika dharura ya moto.

"Madhara makubwa sana yanaweza kusababishwa na mlipuko wa gari linalobeba mafuta. Wananchi wanaombwa wasisogelee gari la mafuta, hasa linapopata ajali," anasema.

Lingine anasema magari ya kubebea mafuta yasiegeshwe au kulazwa pasipohusika, yaegeshwe na kulazwa sehemu maalumu zilizotengwa.

"Kwa wakati wote vifaa vya kuhifadhia, kubebea na kusafirishia mafuta vikaguliwe na kuwekwa katika viwango bora na kuweka alama za tahadhari katika maeneo yanayohusika na shughuli za mafuta," anasema.

Anatoa mfano husika ni kama "usivute sigara; zima injini; zima simu;, vaa vifaa vya usalama uingiapo mahali hapa."

**CHIMBUKO LA EWURA**

Kaimu Mkurugenzi huyo, anasema Ewura ilianzishwa kisheria na ilianza kufanya kazi, Septemba mwaka 2006.

"Inadhibiti huduma za nishati (umeme, petroli na gesi asilia) na maji na usafi wa mazingira.

"Udhibiti wa sekta hizi kwa pamoja, unapunguza gharama za udhibiti na kuwezesha mapato ya tozo ya sekta ya nishati kugharamia sehemu ya gharama za udhibiti wa sekta ya maji," anasema.

Anataja majukumu yake ni kutoa leseni na kusimamia utekelezaji wake, kudhibiti ubora, usalama na tija ya watoa huduma, kutathmini na kupitisha marekebisho ya bei za huduma, kusikiliza malalamiko na kutatua migogoro na kuelimisha umma shughuli zake.

Ili kufanikisha majukumu yake, Ewura inatumia sheria za za sekta husika, ikiwamo ya umeme, mafuta, maji na mikataba mbalimbali kama ya leseni, viwango vya ubora (TBS), pia viwango vya ubora na miongozo.

# Mambo hayo! Nigeria Mahari mtindo wa kodi



Shughuli za harusi zikiendelea nchini Nigeria. **PICHA: BBC**

NI takribani miezi minne sasa hakuna ndoa iliyofungwa katika kijiji kimoja la jimbo la Kano, nchini Nigeria tangu chifu wa eneo hilo kuanzisha malipo ya kodi ya harusi.

Ado Sa'id, ni chifu wa kijiji cha Kera, Kaskazini Magharibi mwa nchi hiyo, amewataka mabwana harusi kulipa kodi ya kiasi cha dola 377 (sawa na Sh. 878, 400).

Hiyo ni mbadala wa utamaduni uliopo wa kulipa samani, vyombo vya jikoni na vitu vingine vya thamani, kwa familia ya bibi harusi watakapofunga ndoa.

Kiongozi huyo anasema kuwa, kulipa kodi ni rahisi zaidi kuliko mahari na itawafanya watu wengi kufunga ndoa kirahisi na utekelezaji wake, utaanza baada ya kushauriana na wanakijiji, jambo ambalo lilipingwa vikali.

Wanakijiji wanadai utaratibu wa zamani ulikuwa mzuri na waliweza kununua zawadi wanavyotaka.

Mwanakijiji, Isah Kera, anasema sheria mpya inawalazimisha wapenzi kwenda kufunga ndoa sehemu nyingine, ili kukwepa kodi hiyo na mwenzake, Sani Kera, anasema ana watoto watano ambao wako tayari kuoa, lakini mipango yao imebidi ihairishwe.

Wakati Nigeria wanalalamikia kodi kwenye harusi, vijana wa kwingineko Afrika, wanalalamikia gharama kubwa ya mahari katika jamii zao.

Nchini Uganda, utamaduni huo ni wa kawaida kwa jamii zilizopo katika maeneo ya mashinani, pia hutolewa katika maeneo ya mijini. Mahari nchini humu hufuata msingi ambao umekuwapo kutoa kitu ili upewe mke.

Lakini sasa, kuna mtindo wa baadhi ya familia kuandikishana mikataba na bwana harusi kama ithibati ya kulipa mahari anayoitishwa.

Inaaminika, iwapo mke anamtoroka mumewe, familia yake inawajibika kulipa mahari.

Mwaka 2010, mahakama nchini humo iliamua utoaji mahari ni halali, lakini majaji walipiga marufuku mtindo wa kurudishwa wakati ndoa inapovunjika.

Nchini Kenya, sheria haishurutishi ulipwaji mahari, lakini ni jambo linalofahamika rasmi katika jamii.

Baadhi ya jamii, kwa mfano za wafugaji husisitiza mahari ya mifugo na jamii nyinginezo pesa taslimu na hata madini hupokewa kama mahari.

Utamaduni wa kutoa mahari upo katika nchi nyingi, ikiwamo barani Asia, pia Mashariki ya Kati

**MAANA YA MAHARI**

Kiwango kinachotolewa kumposa binti, hutofautiana kuanzia zawadi ndogo tu za kuendeleza utamaduni huo hadi maelfu na mamilioni ya shilingi.

Tangu jadi, utoaji mahari umekuwa utamaduni unaoheshimiwa na kuenziwa pakubwa hata miongoni mwa jamii za watu waliosoma na kuishi maisha ya kisasa.

Kwa kawaida mahari ni kama mkataba wa makubaliano kabla ya ndoa ambapo mali kama ng'ombe, ngamia, mbuzi au hata pesa taslimu hulipwa na bwana harusi kwa familia ya bibi harusi ili apewe mke.

Iwapo mume hatotimiza mahari iliyokubaliwa kwa muda uliotolewa, kuna jamii ambazo zinamrudisha mke nyumbani mpaka mume akamilishe kulipa mahari. **BBC**

BIASHARA

# Bosi Latra afunguka kuikabili bodaboda ni 'pasua kichwa'

## • Kila kukicha mpya kibao kila mahali • Neno usalama barabarani kwao 'sifuri' • Wajipanga 'chamoto' matajiri, madereva





Distributed via ippmedia

Picha halisi ya maisha ya barabarani yanayozaa kilio kutoka kwa madereva na abiria wa boda boda. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**INATOKA UK.13**

mwaka 1985 na utekekezaji zaidi kuonekana katika miaka ya 1990. Awali ilimiliki mashirika ya usafiri kama vile Kampuni ya Mabasi ya Taifa (Kamata), shirika la Kauma na mengine.

Kahatano anasema, serikali ilibaki kuwa mkusanyaji wa kodi baada kubinafisisha biashara, ikaamua kuanzisha jicho lake la kusimamia ufanisi wa shughuli hizo. Hapo ndipo ilipojitokeza Sumatra.

Hata hivyo, kutokana na kuelemewa na majukumu, hivi klaribu serikali imeigawanya kwa kuanzishwa Latra na Mamlaka ya Wakala wa Usafiri wa Meli Majini (Tasac).

Tayari katika maisha yake mapya, Latra ina angalizo lake la awali kimajukumu, tayari inapiga mayowe ya udhibiti wa huduma za usafiri wa bodaboda nchini ikizitaja kuwa 'pasua kichwa.'

Mkurugenzi wa Udhibiti wa Usafiri wa Barabara (Latra), Johansen Kahatano, katika mazungumzo maalum na Nipashe ofisini kwake hivi karibuni jijini Dar es Salaam, anakiri kuna kazi ngumu ya kukabili matatizo ya barabarani, bodaboda ikiwa na nafasi ya kipekee.

Kahatano ambaye ni mzoefu wa masuala ya usimamizi barabarani, analalamika kuwapo ongezeko la bodaboda mpya barabarani kila kukicha, sambamba na madereva wengi wenye nidhamu duni, jambo linalowapa tabu.

> **"Sisi tunadhibiti magari ya abiria na mizigo na Polisi wanadhibiti na kukamata katika sehemu yao barabarani na kutoza faini. Vilevile TRA nao wanafanya kazi katika sehemu yao.**

Anasema, majumuisho ya mustakabali huo yanaiweka Latra, katika wakati mgumu, pia Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani na wadau wengine, wakiangukia mtihani mgumu wa kutoa elimu ya kudhibiti matumizi ya barabara na usalama wake, kwa kufuata sheria na kanuni.

Kahatano anasema, madereva wengi wa bodaboda, hawana uelewa sahihi wa sheria na kanuni za usalama barabarani. Analifafanua hilo akisema:

"Udhibiti wa huduma za usafiri wa bodaboda barabarani bado ni mgumu katika Mamlaka yetu ya Latra, kutokana na wahusika kutokuwa na uelewa juu ya usalama barabarani, tabia zao, elimu zao, utumiaji wa vyombo hivyo pamoja na utambuzi wao."

"Kila siku bodaboda mpya zinaongezeka, hivyo madereva wengi hawajui sheria na kanuni za usalama barabarani," anafafanua Kahatano.

Anasema, waendesha bodaboda wengi nchini hawaizingatii sheria na kanuni za usalama barabarani, hivyo kusababisha ajali na madhara kwa abiria yasiyokuwa ya lazima.

Ni mazingira anayoyasema inaifikisha serikali kuchukua hatua kali kisheria, ikiwamo kutoza faini na wengine wanafikishwa katika



vyombo vya dola.

Kahatano anasema, Latra inafanya kazi kubwa ya kutambua bodaboda kwa kushirikiana na halmashauri za wilaya, miji na Polisi wa Usalama Barabarani, kwa kuwapatia madereva elimu ya usalama barabarani, wadau wa watumiaji barabara.

Anasema, mamlaka imeshaanza mikakati ya kuhakikisha wanaomiliki bodaboda wanatambuliwa na kusajiliwa na vyombo vyao, kwa kutumia mfumo wa kisasa, ili makosa ya madereva wao yanapotokea, iwe rahisi kuwajibishana kisheria.

### TAA NYEKUNDU

Kahatano anasema, madereva wa bodaboda wanatumia vibaya sheria na kanuni za usalama barabarani, wakikaidi kusimama taa nyekundu zinapowaka, pia katika alama za pundamilia kwa watembeaji kwa miguu.

Anasema, kuna bodaboda zinazoendesha kwa kasi kubwa zikipita taa nyekundu, bila ya kusimama, huku wakiwa na abiria. Mkurugenzi huyo wa Udhibiti wa Usafiri wa Barabara wa Latra, anasema ni hali inayochangia ajali na madhara kwa abiria watembeao kwa miguu.

"Bodaboda wamekuwa wakihatarisha maisha ya watembea kwa miguu na abiria pindi wanapokaidi kusimama katika eneo la taa nyekundu, ambazo huzuia asipite hadi atakaporuhusiwa na taa za kijani.

"Lakini wao hupita, hivyo kusababisha ajali na madhara kwa abiria au watembea kwa miguu wanapovuka alama za pundamilia," anasema Kahatano.

### KAZI ZA LATRA

Kahatano anaeleza majukumu ya Latra, ni kudhibiti huduma za kiuchumi kuhusu viwango vya nauli, ubora wa huduma kwa wadau katika kiwango kinachotakiwa, kukagua uzima wa magari na kupitia upya viwango vya nauli katika huduma ya usafiri wa magari madogo ya abiria na mabasi makubwa ya abiria nchini.

Anasema, mamlaka hiyo inasimamia mazingira ya huduma zinazotolewa kwa wananchi kuhakikisha zinakuwa salama na kudhibiti asinyonywe, kukagua gari la mizigo na abiria kama liko salama ili abiria asipatwe na hofu wakati akisafiri na kuchukua hatua linapobainika kuwa bovu.

Lingine analotaja Kahatano, wajibu wa Latra upande wa pili wa shilingi ni kulinda maslahi ya wanaomiliki magari ya abiria, wasipate hasara katika uendeshaji biashara zao. Aidha, anasema jukumu walilo nalo ni kudhibiti faida katika biashara za mabasi ya abiria isizidi asilimia 25, lengo ni kutowaumiza walengwa watoa huduma.

Kahatano anasema, wamepokea malalamiko ya wadau na kuyatolea ufafanuzi, kisha wanachukua hatua, kadri hoja zilivyo, ikiwamo adhabu na makosa mbalimbali.

Anasema, Latra imekuwa ikitoa elimu kwa wadau wake kupitia njia mbalimbali katika vyombo vya habari na wana utaratibu wa kukagua magari ya mizigo na abiria ambao ni wa kisheria hata kama gari sio bovu.

### SHERIA MPYA

Kahatano anasema sheria mpya ya Latra ya mwaka huu, inafafanua kazi yake kuratibu usalama wa barabarani, kwa kuhaikikisha mhusika anayajua majukumu yake matumizi ya barabara.

Anayataja, kupanga mfumo mzima wa kudhibiti usafiri ardhini, kutoa elimu na mafunzo ya ukaguzi wa magari na makosa mengine kupitia Polisi wa Usalama Barabarani.

"Sheria hiyo mpya imekuja na mfumo mpya wa magari yote ya abiria lazima yakaguliwe hata kama ni zima au bovu, ili kupunguza ajali nyingi barabarani na madhara yasiyokuwa ya lazima kwa abiria na madereva watasoma vyuo vya Veta (Vyuo vya Maendeleo ya Ufundi na kupewa vyeti rasmi," anasema.

Kahatano anafafanua kwamba, mwongozo wa kisheria ni dereva wa magari ya mizigo na abiria wanadhibitiwa kwa kufanya mitihani ya uendeshaji magari na kupewa cheti, ambazo utoaji wake unaratibiwa kupitia mitihani maalum, Latra ikishirikiana na Polisi Usalama Barabarani.

### MWENDOKASI JE?

Kahatano anaeleza kiwapo mabasi 3,400 ya abiria yanayofanya safari za mikoa mbalimbali nchini, yamefungiwa vidhibiti mwendo vinavyosaidia kupunguza ajali na madhara kwa abiria.

Anaongeza, Latra kwa kutumia vifaa hivyo inaangalia na kudhibiti madereva wasikiuke sheria na kanuni. Ni vifaa vinavyoonyesha alama na mlio kudhibiti mwendokasi unaomtaarifu dereva apunguze mwendo katika kiwango anachoruhusiwa.

### WANAVYOSHIRIKIANA

Kahatano anasema makosa ya kisheria kuhusu mwendokasi kupitia teknolojia ya kisasa ya kutumia tochi barabarani, inaona mabasi ya abiria yanayokimbia mwendokasi, ikiwa na mwongozo maalum ya utozaji huo.

"Pia, mipaka yetu Latra,TRA na Polisi inajulikana, hatuingiliani. Kila mtu ana sehemu yake, ila shughuli zetu kwa pamoja zinafanana.

"Sisi tunadhibiti magari ya abiria na mizigo na Polisi wanadhibiti na kukamata katika sehemu yao barabarani na kutoza faini. Vilevile TRA nao wanafanya kazi katika sehemu yao," anaeleza Kahatano.

Anataja baadhi ya makosa na adhabu zake za faini:Uendeshaji gari bila leseni ya mamlaka husika, Sh. 250,000; kukatisha 'ruti' Sh.100,000; osa dogo barabarani Sh.30,000; na makosa makubwa yanayosimamiwa na latra, shilingi milioni moja.

Latra inaiomba serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kuanzisha muhtasari wa mafunzo katika shule za msingi nchini, wanafunzi waanze kufundishwa somo la usalama barabarani.

"Usalama barabarani ni suala mtambuka linahitaji elimu zaidi kwa jamii," anasistiza.

Pia, anazitaka asasi za kiraia kwa kushirikiana na serikali, zishiriki kutoa elimu hiyo, akitoa mfano wa Wakala wa Ujenzi wa Barabara Vijijini na Mijini (Tarura) Tarura, Wakala wa BarabaraTanzania (Tanroads) na Polisi Usalama Barabarani.

### CHANGAMOTO

Anasema Latra ina upungufu wa wafanyakazi baada ya kugawanyika kutoka Sumatra, pia inakabiliwa na shida ya uelewa mdogo wa wadau wanaosimamiwa na chombo hicho.

Lingime analitaja, wananchi kutojua sheria na kanuni kuhusu za usalama barabarani na huduma zake za msingi, hivyo kuwapo hali ya umma kupotoshana.

***Mwandishi wa makala hii anapatikana kwa barua pepe: anthonygervas@yahoo.com na simu (+255) 0682 86 92 44.***

# Biashara katika picha



Mchuuzi akitembeza bidhaa zake, katika eneo la Mabibo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**



Machinga akinadi kofia katikati ya Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, eneo la Daraja la Selander, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mama mkaanga samaki akiandaa kitoweo hicho, kwaajili ya wateja wake, kando ya Barabara ya Mabibo, eneo la Urafiki, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

BIASHARA

MAISHA MAZURI HAYAONGOPI

# Waume walioteIekeza warudi kusikia 'nyumbani kumenoga'

• Tasaf hiyo; aliyetoweka 2008 aonekana, wa 2014 arudi kwa 'magoti' ya msamaha • Safari zote zilianzia giliba 'wee mzigo tu'

**Na Elizabeth Zaya,**

Wanging'ombe

"HAKUNA kama Tasaf. Imenisaidia kurudisha mume wangu ambaye alikimbia na kunitelekeza na watoto wangu kwa sababu ya ugumu wa maisha," ni kauli ya mnufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) Salome Mpogole.

Huyo ni mkazi wa kjiji cha Lyamkena katika Halmashauri ya Wanging'ombe, anayesimulia kwamba kabla ya kuingizwa katika mpango huo, maisha yake yalikuwa magumu na hata kukawapo ugomvi usioisha na mume wake.

Anaeleza chanzo cha malalamiko hayo ni kwamba yeye ni 'mzigo' kwa mume kwa kutofanya shughuli yoyote ya kumuingizia kipato

Salome anasema, aliendelea kuvumilia aliyoambiwa na mume wake ambaye baadae litoweka, akimtelekezea watoto wanne

Mama huyo anasema ilikuwa kama ndoto kwake kutelekezwa na watoto na mume wake aliyempenda, katika mkasa ulioanzia mume kumuaga anasafiri kwenda kutafuta shughuli ya kuongezea kipato, ili kuikomboa familia dhidi ya umasikini, naye alikubali.

"Mambo yalibadilika, miezi ilipita bila mume wangu kunipigia simu wala hakutaka kujua maisha niliyokuwa naishi na watoto, "anasimulia Salome

"Tuliishi maisha ya tabu sana, ilibidi niingie kwenye vibarua katika mashamba ya watu ili angalau nipate pesa hata kidogo kwa ajili ya chakula, nilijitahidi kufanya hivyo japo bado maisha yalikuwa magumu sana, kwa sababu nikiugua nilikuwa siwezi kwenda.

"Hata watoto wakiugua, nilikuwa sina uwezo wa kupata pesa ya kuwauguza. Ilifika wakati mpaka majirani walikuwa wananionea huruma na kunisaidia walichokuwa wakijaliwa," anasema.

### TASAF YAJA

Salome anasema, mwaka 2014 kwenye mkutano wa kijiji baada ya kufika ugeni wa Tasaf na Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini, alipendekezwa kuingizwa katika mpango na alianza kupatiwa Sh. 40,000, aliyotumia kwa ajili ya mahitaji ya watoto shuleni, chakula na huduma za tiba.

"Hali ya maisha ilianza kubadilika kidogo, mawazo hasa niliyokuwa napata juu ya chakula cha watoto yaliisha. Kabla ya hapo,


Distributed via ippmedia

Auleliya akitoa mifugo kwenye banda. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

> **"Mpaka sasa tangu nianze kufuga kuku, nimeuza mara nne na pesa hizo zimenisaidia kujenga nyumba ya tofali za kuchoma ya vyumba viwili.**

tulikuwa tunapata tabu hata kupata mlo mmoja kwa siku tulikuwa hatuna uhakika, lakini tulipata uhakika wa kula miwili mpaka mitatu baada ya kufikiwa na Tasaf," anasema Salome

Anasimulia kwamba mwaka 2015 walengwa wote wa Tasaf walishauriwa kuanzisha vikundi vya watu 10 vya kuwekea akiba pamoja na kuanzisha miradi midogo

Salome anasema, katika kikundi chao walijipanga kuanza na akiba ya shilingi 2000 kila wiki na mwisho wa mwaka wakopeshana, wakiwa na malengo kila mwaka kutumia pesa hizo kuanzisha mradi binafsi na mengine ya maendeleo

Anasema, ilipofika mwisho wa mwaka huo 2015 alipata zaidi ya Sh.100,000 aliyowekeza na akaanza kununua kuku watano wa kufuga pamoja na bati mbili.

"Kuku hao walizaliana hadi kufikia 30, kwa awamu ya kwanza, nikauza 20 nikabakiza 10 ambao niliendelea kufuga," anasema na kuongeza:

"Mpaka sasa tangu nianze kufuga kuku, nimeuza mara nne na pesa hizo zimenisaidia kujenga nyumba ya tofali za kuchoma ya vyumba viwili."

"Watoto wangu wanaishi vizuri kwa sasa na maendeleo yao kwenye masomo ni mazuri sana, wanakula na kulala vizuri," anaeleza.

### MUME AREJEA

Salome anasema mwaka 2017, mume wake alirudi nyumbani na kumuomba msamaha kwa kumkimbia na kumtelekeza watoto. Aliamua kumsamehe

"Licha ya mateso aliyokuwa akinipatia mwanzoni na baadae kunitelekeza na wanangu, lakini alivyorudi na kwa namna alivyokuwa amekonda, niliamua kumsamehe ili tulee watoto wetu.

"Huwezi 'amini' mume wangu amebadilika, hanitukani wala kunigombeza kama zamani na tunashirikiana kuendesha shughuli zetu, "anasema Salome.

"Yote haya yametokana na mimi kuanza kujiunga na vikundi vya ujasiriamali kwa walengwa wa Tasaf, kuanza kujiwekea akiba na kufanya shughuli za kujiongezea kipato, bila hivyo sidhani kama angerudi," anasema.

### MKASA ULEULE

Auleliya Kiwale wa kjiji cha Usetule katika Halmashauri ya Mji wa Makambako, naye anasimulia namna alivyokuwa na migogoro katika ndoa yake na baadae kutelekezwa na mume, akiangukia kuishi kwa tabu.

Kama alivyo mtangulizi wake, naye anasimulia kwamba baada ya kuishi kwa tabu kipindi kirefu ,wananchi waliamua kumpendekeza aingizwe katika 'kaya masikini' wa Tasaf na baadaye alianza kujishughulisha na miradi wa uzalishaji, ikiwamo ufugaji.

Anasema, mume aliyemtelekeza na watoto watatu, baadae baada ya kufanikiwa kwa kuwezeshwa na Tasaf, aliomba kurudi nyumbani.

"Mimi nilitelekezwa na mume wangu miaka mingi sana tangu mwaka 2008 na alisema anakwenda kutafuta eneo kwa shughuli za kilimo, lakini alipoondoka hakurudi tena na kutuachia mateso makubwa, mimi na watoto wangu," anasema.

Kiwale anasema, baada ya kuingizwa katika mpango wa kunusuru kaya masikini, alianza kujishughulisha na ufugaji kuku na mbuzi, pia kilimo na alifikia hatua ya kujenga nyumba iliyoezekwa ikiwa na vyumba vitatu

"Kama unavyoona sina shida tena, Tasaf imenikomboa, ninaishi kwenye nyumba ya kisasa na hatunyeshewi mvua tena kama ilivyokuwa zamani. Naishukuru sana Tasaf," anasema mama huyo

Anasema, kwa sasa ana mbuzi zaidi ya 10, kuku wa nyama na kuza mazao ya kutosha

### MRATIBU TASAF

Kaimu Mratibu wa Tasaf, katika Halmashauri ya Mji wa Makambako, Veronica Simwanza, anawasifu wanawake wengi walio katika mpango wa kunusuru kaya masikini wamepambana kujiunga na vikundi vya uzalishaji na vimewaongezea kipato na kuwapunguza shida nyingi za kifamilia.

"Nikiri kwamba ni kweli wanawake, hususani katika familia za walengwa, wamefanya kazi kubwa. Sisi tunaowasimamia na kuwafuatilia mara kwa mara tunashuhudia hili.

" Wapo baadhi yao walikuwa na maisha magumu baada ya kutelekezwa na waume zao, lakini baada ya kuingizwa kwenye mpango na kufundishwa mbinu za ujasiriamali, wanawake wengi wamefanya makubwa na baadhi yao waume zao wamerudi na kuwaomba msamaha," anasema Veronica

BIASHARA

UNAIJUA SARAFU MTANDAONI?

# Mkurugenzi anayeacha ofisi IMF 'atiririka' inavyokubalika zaidi

**Na Nimi Mweta**

ULE mwelekeo wa awali kuwa sarafu mtandao ni nyenzo haribifu katika soko la fedha na amana la kimataifa, huku baadhi ya wataalamu wakisema ni homa ya uwekezaji bahatisha ambayo itafikia mlipuko na hasara kwa walanguzi wa sarafu mtandao sasa unaanza kupauka.

Kuna wakati wasimamizi wa masuala ya fedha wa Marekani, hasa Kamati ya Bunge kuhusu sekta ya fedha, waliangalia kwa karibu uwapo wa sarafu mtandao na utitiri wake ambao sasa ziko zaidi ya 1,600 kote duniani.

Waliposhindwa kufikia tamati ya kuzizuia au kuweka vizingiti halisi, wasiwasi ukaondoka.

Wasiwasi huo ulifikia kilele chake pale Kamati ya Fedha ya Bunge, ilipomhoji Mkurugenzi Mtendaji na mwanzilishi wa mtandao wa Facebook, ulitoa azimio la kuanzisha sarafu mpya ya jina la Libra, Mark Zuckerberg.

Mpango huo uliishtua Marekani, kwa vile Libra ilikuwa na wadhamini zaidi ya 100, yaani kampuni kubwa zinayoingiza fedha za awali (hisa au mitaji) kuanzisha operesheni za Libya kama sarafu mtandao nzito kuanzia mwanzo.

Baadhi walianza kuwa na wasiwasi, itakuwa mshindani wa haja kwa sarafu ya Marekani, dola inayotolewa na Benki Kuu ya Marekani haraka.

Wakati suala la kuundwa Libra bado liko mezani na sarafu hiyo haijaanza kusikika ikitikisa masoko, kwani bado masoko ya fedha yanaifuatilia zaidi Bitcoin, iliyofikia ngazi ya sarafu mtandao kiongozi zaidi ya miaka miwili sasa, kuna mabadiliko zaidi.

Kuanza kwa sarafu shirika badala ya wajasiriamali tofauti kuunda sarafu zao za mtandao, kumefanya suala hilo katika ngazi tofauti, kiasi serikali za nchi tofauti zinanza kufikiria kuunda sarafu zao.

### IMF YAINGILIA

Ni katika hali hiyo. Benki ya Dunia na Shirika la Fedha lal Kimataifa (IMF) imeanza kuangalia sarafu mtandao katika mazingira tofauti hivi karibuni.

Akiandika katika blogu ya IMF, Christine Lagarde, mkurugenzi mtendaji anayeondoka, alizilinganisha na 'homa' ya kulima maua (tulip) Uholanzi katika karne ya 17 na kusambaa halafu kuporomoka kwa 'dot.com' (kampuni, biashara zilizojikita mtandaoni) mwanzo wa muongo uliopita.

Alithibitisha kuwa kati ya sarafu mtandao 1,600 zilizokuwa sokoni tayari, nyingi tu zitayeyuka katika mchakato wa kuchuja pale sarafu kubwa na muhimu zikianza kujithibitisha katika soko.



Christine Lagarde; Mkurugenzi Mtendaji wa IMF anayeondoka. **PICHA: MTANDAO.**

> **"Ukiangalia alichosema Lagarde katika blogu yake, anasema kwamba ugunduzi wa upande bora au wezeshi tija wa sarafu mtandao ndiyo unaanza kufahamika.**

Christine Lagarde, kabla alikuwa Waziri wa Fedha wa Ufaransa na sasa anaenda kuchukua nafasi ya Gavana wa Benki Kuu ya Umoja wa Ulaya, mwanzoni mwa mwaka. Bado alikuwa na wasiwasi kuhusu 'kizunguzungu' kinacholetwa na sarafu mtandao.

Hata hivyo alikumbushia kuwa teknolojia kadhaa zilizoibuka kipindi cha 'dot.com' tayari zimekuwa na athari kubwa katika maisha ya kila siku, kwa mfano katika maeneo ya kuweka akiba, kuwekeza na kulipa bili.

Alisisitiza kuwa mtazamo sahihi kuhusu sarafu mtandao ulenge siyo katika kulaani sarafu hizo na siyo kuzitumainia kupita kiasi, ila kuangalia kwa makini fursa zinazoweza kupatikana kwa kutumia sarafu hizo kwa umakini na uadilifu.

Mwanzoni, mkazo ulikuwa unawekwa katika upande hasi wa sarafu mtandao, kuwa ni njia inayoibuka ya kukwepa sheria katika uhamishaji fedha, kutakasa pesa za madawa ya kulevya na uwezeshaji wa ugaidi.

Ukiangalia alichosema Lagarde katika blogu yake, anasema kwamba ugunduzi wa upande bora au wezeshi tija wa sarafu mtandao ndiyo unaanza kufahamika.

Lagarde anakumbushia jinsi teknolojia za 'dot.com,' pamoja na kukwama kwa wimbi hilo la uwekezaji, zimesaidia kubadili mitindo ya maisha kote duniani. Inabidi wasimamizi fedha wasijihami, wajifunze zaidi.

### ZINAKOFAA

Akigusia maeneo bora ya sarafu mtandano inakofaa, Lagarde anataja amana za mtandao kwa jumla zinawezesha ubadilishaji haraka wa amana au fedha bila ya gharama, huku zikiwa na baadhi ya sifa za fedha za kawaida.

Anasema, iwapo zinatolewa na wajasiriamali au kampuni binafsi, amana hizo zinakuwa hatarishi na thamani yake 'inarukaruka', hivyo kuna haja ya benki kuu za nchi tofauti kuanza kutoa aina mpya za fedha, sarafu za mtandaoni.

Mtaaluma huyo wa fedha, anasema teknolojia kuu ya sarafu mtandao, ambayo wataalamu wanaita 'teknolojia ya kitabu hifadhi cha wote' (distributed ledger technology) inaweza kusaidia masoko ya fedha kufanya kazi kwa ufanisi zaidi, akitoa mfano wa mikataba inayoingia na kusimamiwa mtandaoni moja kwa moja.

Uwezo wa kutumia mfumo huo wa kiteknolojia unaweza kupunguza baadhi ya shughuli za uwakala wa fedha au hisa (amana za kuuza mtandaoni), akatoa mfano kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Soko la Hisa nchini Australia inapanga kutumia mfumo wa DLT kukamilisha na kufanya malipo ya ununuzi wa hisa.

Anataja pia ubora wa DLT katika utunzaji nyaraka, akitoa mfano wa kampuni za tiba kutaka kuanza kutumia mfumo huo kuhifadhi takwimu nyeti za tiba na wakati huo huo kuzitoa kwa kampuni za bima na watumiaji wengine walioruhusiwa.

Nchi zinazoendelea zimeanza kuona umuhimu wa kutumia mfumo huo kujenga haki miliki ya mali isiyohamishika, kuongeza kuaminika sokoni, kwa kupunguza nguvu za mamlaka za usimamizi na kupanua wigo la uwekezaji, kuondoa tatizo la kuhifadhi taarifa mauzo ya ardhi.

### MAPINDUZI YA FEDHA

Lagarde ananena kuangalia sarafu mtandao kama mwanzo wa kinachoitwa 'mapinduzi ya teknolojia ya fedha' akisema kuwa mapinduzi hayo hayataondoa hitaji la mawakala wanaoaminika,katika bima au mabenki.

Anataja matumaini ya matumizi kwa njia za wazi, zinazotokana na uwapo wa kabrasha la pamoja la taarifa husika bila watu wa nje (wasio wadau wa amana au mtiririko wa mauzo) hawawezi kuziingilia.

Pia, anasema wanaohusika na hivyo kuzipata kama nyaraka jumla za wazi kuhusu eneo hili au lile biashara ya amana, hisa, fedha au bidhaa hawawezi kubadili nyaraka, takwimu baada ya kuingia katika nyaraka jumla husika.

Takriban uaamuzi wote unatolewa mikononi mwa watawala na kuwekwa katika soko, ambako nyaraka za matukio (mauzo, manunuzi) zinasambazwa kwa pamoja, haraka.

Mkurugenzi huyo anayeondoka IMF, anasema kutokana na uchache wake katika soko hivi sasa ukilinganisha na mifumo rasmi ya fedha na hisa katika masoko ya kimataifa, sarafu mtandao bado hazileti wasiwasi wa uthabiti wa mfumo wa fedha au mabenki kimataifa.

Anasema hata hivyo sarafu mtandao zina uwezo bayana wa kufikisha katika ngazi ya kushangaza au ya kutisha vihatarishi vya biashara wekeza inayotegemea thamani nyeti mahali fulani, halafu ikiporomoka ni mfumo wote unaathirika.

Kwa upande mwingine mabenki na taasisi nyinginezo za kifedha zitakuwa na wakati mgumu wa kutetea mifumo yao ya biashara (inayojifundia katika amana chache zinazohusishwa na taasisi hizo) pindi mifumo kama DLT ikipanuka kitaifa, kimataifa.

BIASHARA

# Bandari Tanga katika safari ya kupanda na kushuka mapato

- Meneja alia kina kinamuangusha



Mandhari ya Bandari ya Tanga. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Mary Geofrey,** aliyekuwa Tanga

***IJUMAA iliyopita, ilikuwapo makala kuhusu maendeleo ya bandari ya Mtwara. Mwandishi anaendelea na simulizi za bandari nyingine kubwa ya Tanga. Endelea.***

BANDARI ya Tanga ipo chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) na ni ya pili kwa ukubwa katika mwambao wa bahari ya Hindi, ikitanguliwa na Bandari ya Dar es Salaam.

Meneja wa Bandari hiyo, Ajuaye Msese, anasema imekuwa ikihudumia sehemu kubwa ya mizigo ya nchini na nchi jirani kutokana na nafasi yake kijiografia, kwa upande wa Tanzania imekuwa ikihudumia upande wa Kaskazini na Mashariki katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Singida.

Anasema katika bandari hiyo ambayo barabara ya reli imepita ina fursa ya kurahisisha mizigo itakayoshuka na kupelekwa moja kwa moja katika mikoa ya Kigoma,Tabora na Mwanza na kuhudumia shehena za nchi ambazo hazina bandari kama Uganda, Rwanda, Burundi na Congo, Zambia, Malawi kwa urahisi kabisa kupitia njia hiyo ya reli.

Msese anasema, katika kuhakikisha inaleta chachu katika sera ya taifa ya uchumi wa viwanda, Serikali kupitia TPA inatekeleza miradi mbalimbali yenye lengo la kuifanya bandari ya Tanga kuchangia kwa sehemu kubwa uchumi wa Taifa.

Anasema TPA imeona vyema kuijengea uwezo bandari ya Tanga ili ihudumie meli nyingi na kubwa pamoja na shehena kubwa kwa ufanisi zaidi.

> Kwa sababu ya changamoto ya kina cha bandari ya Tanga inayofanya meli kubwa kufunga nje ya gati na baadaye kutumia vifaa vingine katika kusogeza mzigo katika na kuvitoa.

"Ili kufanikisha azma hiyo miradi mbalimbali imekuwa inatekelezwa katika bandari hiyo ikiwamo ya muda mfupi, kama vile ununuzi ya vifaa, miradi ya muda mrefu kama ujenzi wa sehemu ya kuhifadhia makasha na uboreshaji wa gati namba mbili kwa ajili ya kuhudumia meli na mizigo kwa ufanisi wenye tija kubwa," alisema Msese.

**UINGIZAJI SHEHENA**

Msese anasema shehena zinazohudumiwa katika bandari hiyo zinaongezeka na kushuka katika vipindi mbalimbali kutokana na sababu zilizopo ndani ya bandari hiyo.

Anasema katika miaka mitano ya nyuma kutoka mwaka wa fedha 2014/15 takribani shehena zilizohudumiwa katika bandari hiyo ni tani 800,000 za mzigo huku kwa mwaka 2015/16 zilihudumiwa tani 843,000.

Meneja huyo anasema, katika mwaka wa fedha 2016/17 shehena zilizohudumiwa katika bandari hiyo zilishuka kwa kiasi kikubwa na kuhudumia tani 589,000 na kwa mwaka 2017/18 zilipanda tani 646,000 .

"Kwa mwaka wa fedha 2018/19 zimehudumiwa tani 690,000 matarajio yetu katika mwaka huu wa fedha tutarudi katika tani 800,000 kabla ya kufikia tani milioni 1.2,"anasema Msese.

Anasema miongoni mwa shehena zinazopita katika bandari hiyo ni pamoja na mazao ya kilimo, malighafi zinazotumika katika kuzalisha bidhaa katika viwanda vilivyopo Tanga na mikoa jirani Moshi na Arusha.

Msese anasema, mbali na bidhaa hizo bandari inapitisha shehena ya makasha ambayo shehena zake zinaongezeka na kupungua kwa namna tofauti tofauti kulingana na meli zinazoingia.

Anasema, mwaka wa fedha uliopita bandari yao iliweza kuhudumia makasha takribani 6,259 sawa na asilimia 32 ya malengo waliojiwekea na kwamba mwaka uliiopo wa fedha,wanatarajia kuhudumia makasha 11,000.

Msese anasema, ili kufikia malengo hayo, uongozi wa bandari umeanza mazungumzo na wateja wa makasha hayo walioacha kupitisha katika bandari hiyo na wale ambao ni wageni.

**UINGIAJI WA MELI**

Msese anasema shehena katika bandari uletwa na meli, kwa miaka mitano iliyopita meli zilizohudumiwa katika ukubwa tofauti katika bandari hiyo na kwa mwaka wa fedha 2018/19 takribani meli 677 zilihudumiwa.

Anasema, meli zinazoingia katika bandari hiyo ni zile ndogondogo ambazo zinatumika kuchukua mzigo katika bandari ya Tanga na kupeleka katika maeneo ya bandari za karibu, ikiwamo Dar es Salaam ambazo hupeleka shehena katika meli kubwa na kwenda nchi mbalimbali.

"Sababu za kuja kwa meli ndogo katika bandari yetu ya Tanga ni kutokana na miundombinu iliyopo sasa kutoweza kupokea meli kubwa katika gati,"anasema Msese na kuongeza

"Kwa sababu ya changamoto ya kina cha bandari ya Tanga inayofanya meli kubwa kufunga nje ya gati na baadaye kutumia vifaa vingine katika kusogeza mzigo katika na kuvitoa ," anasema Msese.

**MRADI WA KUONGEZA KINA**

Msese anasema Serikali kupitia TPA imekuja na mradi mkubwa wa kuongeza kina katika mlango wa kuingilia bandari ya Tanga .

Anasema upanuzi wa kuongeza kina cha maji hadi kufikia mita 13 katika bandari ya Tanga na inagharimu Sh. bilioni 170 na itayozifanya meli kubwa kufika, kushusha na kupakia mzigo karibu na gati umbali wa mita 200 kutoka umbali wa kilomita 1.7 za sasa.

"Upanuzi na Uongezwaji wa kina katika gati hilo utafanya meli kubwa kufika katika bandari hii na kushusha mizigo kwa urahisi zaidi na kupunguza gharama za usafirishaji wa mizigo kutoka meli awali ilipokua inaishia mpaka karibu na Gati," anasema Msese.

Anasema awali meli ilikua inasimama kwa umbali wa Kilomita 1.7 lakini kwa sasa mita 200 tu, hivyo kumefanya ufanisi wa kituo hicho na mapato kuongezeka kutokana na uchimbaji huo unatarajiwa kupunguza muda kupaisha mapato .

**MAPATO BANDARINI**

Msese anasema lengo kubwa ya kufanya miradi mbalimbali bandarini, ni kukusanya mapato itakayofanya bandari ya tanga na nchi kwa ujumla kuweza kutengeneza faida na kusukuma gurudumu la maendeleo katika bandari ya Tanga.

Anasema, wanaendelea vizuri katika suala la mapato licha ya kuwapo changamoto ya kushuka na kupanda, lakini katika miaka mitano iliyopita na miaka miwili ya nyuma walikuwa na mafanikio mazuri ya ukusanyaji wake.


Hata hivyo, kupungua kwa shehena katika miaka miwili iliyofata walishuka na kwa mwaka 2018 wameanza kupanda tena.

**BANDARI BUBU**

Msese anataja matatizo mengi yanayowakabili, ikiwamo bandari zisizo rasmi ambazo zimekuwa zikipitisha shehena ya mizigo mbalimbali na kufanya Serikali kushindwa kupata mapato kupitia bandari zilizo rasmi.

"Serikali kupitia TPA imeendelea kuzitambua bandari ambazo sio rasmi zinazopitisha mizingo mbalimbali na kuziwekea utaratibu wa kuzisimamia na bandari ya Tanga.

"Tayari wametambua bandari kadhaa zimeanza kuwekewa mkakati wa namna gani zinaenda kusimamiwa ili kuweza kuthibiti mapato yanayotoka na shehena zinazopita katika bandari hizo bila kuwa na utaratibu uliokubalika," anasema Msese.





Vijana wa Bajaj wakiendelea na harakati za kubeba abiria katika kituo walichotengewa cha Kabwe jijini Mbeya juzi, eneo ambalo hujaa maji nyakati za mvua. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Ajifungua watoto watano, mmoja afa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKAZI wa Kata ya Kibeta jijini Mbeya, Emelia Joram (21), amejifungua watoto watano katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, huku mmoja akiwa amekufa.

Emelia alijifungua Oktoba 31, mwaka huu kwa upasuaji, ambapo watatu kati yao ni wa kike na mmoja pekee ndiye wa kiume na wawili kati yao wapo kwenye chumba cha joto kutokana na kuzaliwa wakiwa na uzito pungufu.

Daktari Bingwa wa Watoto wa Hospitali hiyo, Dk. Ismail Macha, alisema walimpokea binti huyo mwezi Mei mwaka huu kwa ajili ya kutaka kupimwa kipimo kikubwa (Ultra Sound) na walipompima wakabaini ana ujauzito wa mapacha watano.

Alisema baada ya kubaini hali hiyo waliamua kubaki naye katika hospitali hiyo kwa ajili ya uangalizi wa kina mpaka alipojifungua mwishoni mwa Oktoba ambapo walilazimika kumfanyia upasuaji.

Dk. Macha alisema kabla ya Emelia hajaenda katika hospitali hiyo, alikuwa ameanzia katika moja ya vituo vya afya jijini humo ambako alishauriwa kwenda kwenye hospitali kubwa kwa ajili ya vipimo vikubwa.

"Asingeweza kujifungua kwa njia ya kawaida kutokana na kuwa na watoto zaidi ya wawili, hivyo tulimfanyia upasuaji na kwa sababu uzao huu sio wa kawaida tuliamua kumfutia gharama zote kama mchango wa hospitali," alisema Dk. Macha. Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Glory Mbwilo, alisema uzao wa aina hiyo ni wa kwanza kutokea katika hospitali hiyo. Alisema kutokana na mama huyo kutokuwa na uwezo wa kunyonyesha watoto wote wanne, waliamua wengine wanyonyeshwe na bibi yao (mama wa Emilia).

Distributed via ipnmedia

Alisema walimpima vipimo vya kiafya na baada ya kubaini kuwa ana afya njema walimruhusu aendelee kusaidiana na mtoto wake kuwanyonyesha wajukuu zake hao. "Nawapongeza madaktari wa kitengo cha mama na mtoto ambao wamehakikisha mama huyu anajifungua salama na watoto wake wanakuwa salama na naamini hii pia imechangiwa na serikali kuboresha huduma za afya," alisema Dk. Mbwilo.

Aliwataka wadau kumsaidia mama huyo kwa vitu mbalimbali ili vimsaidie kuwalea watoto hao kwa madai kuwa kwa sasa hana uwezo wa kufanya chochote cha kumwingizia kipato.

Mama mzazi wa Emilia, Cecilia Mbaza, aliushukuru uongozi wa hospitali hiyo kwa kumsaidia mtoto wake kuanzia siku ya kwanza walipompokea mpaka sasa ambapo bado yupo chini ya uangalizi wa madaktari pamoja na watoto wake. Aliwaomba Watanzania kuendelea kumsaidia mwanaye kwa vitu mbalimbali kwa ajili ya malezi ya watoto wake kwa maelezo kuwa familia yake haiko vizuri kiuchumi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji la Mbeya, James Kasusura, pamoja na wadau mbalimbali walifika katika hospitali hiyo juzi kwa ajili ya kumpatia misaada Emilia zikiwamo fedha taslimu.

Kasusura alimkabidhi Sh. milioni 1.61 ambapo alisema mchango wake binafsi ni Sh. 1,000,000 na zingine ni michango ya watumishi wa jiji hilo pamoja na wadau wengine.

# TIA kutumia utafiti kusaidia vijana kupambana soko ajira

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Uhasibu Tanzania nchini (TIA), imesema inakusudia kutumia utafiti na machapisho yaliyoandaliwa na taasisi hiyo kutoa elimu ambayo itawawezesha vijana kuwa na uwezo wa kupambana katika soko la ajira pamoja na kujiajiri.

Uongozi wa taasisi hiyo ulitoa maelezo hayo juzi wakati wa kongamano la kitaaluma lililofanyika katika chuo hicho Tawi la Mbeya, ambalo liliwakutanisha wasomi, wahadhiri wa chuo hicho, wahitimu wa chuo hicho na wanafunzi.

Mkuu wa Kitengo cha Machapisho wa Chuo hicho, Dk. Elimeleky Akyo, alisema wanawahamasisha wanafunzi pamoja na kusoma masomo yao ya kipaumbele pia wanatakiwa kusoma masomo ya biashara yatakayowawezesha kujiajiri.

"Tunataka vijana wetu wawe na uwezo wa kujiajiri ikiwamo kuanzisha biashara zao, wakijiajiri watakuwa na uwezo wa kuajiri watu wengine na hivyo kupunguza tatizo la ajira nchini, hatutaki kuwa na wahasibu ambao hawana biashara zao," alisema Dk. Akyo.

Alisisitiza kuwa katika kipindi hiki ambacho taifa linaingia kwenye uchumi wa kati kupitia viwanda, wanaandaa wahasibu waliobobea ili waweze kusaidia viwanda vitakavyoanzishwa kuendelea.

Alisema sekta ya uhasibu ni muhimu kwenye uchumi, hivyo ndio maana taasisi hiyo imeamua kuimarisha sekta hiyo ambayo ni muhimu katika shughuli yoyote.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa TIA, Luciana Steven, alisema utafiti mbalimbali unaofanywa na wasomi wa chuo hicho mbali na kuwasaidia wahadhiri na wanafunzi, pia zinasaidia pia kukitangaza chuo hicho kitaifa na kimataifa.

Alisema baadhi ya vyuo vimeajiri wataalamu mbalimbali hasa kwenye vitengo vya uhasibu kutoka katika taasisi hiyo, na kwamba watu hao wanafanya kazi vizuri ambayo pia inaipa sifa taasisi hiyo.

Naye Mkuu wa Idara ya Utafiti na Ushauri wa Taasisi hiyo, Gora Abdallah, alisema lengo la kongamano hilo ni kuwakutanisha wasomi wa taasisi hiyo kwa ajili ya kuwasilisha machapisho yao zinaingiliana na dhana ya taifa ya kuingia kwenye uchumi wa viwanda.

Alisema katika kongamano hilo wataalamu wengi waliwasilisha maandiko ambayo yanalenga masuala ya uchumi na biashara ambayo ndiyo sekta muhimu kwa taifa hasa kipindi hiki.

Alisema baadhi ya utafiti unalenga kubadili mitazamo ya vijana kutotegemea kuajiriwa na badala yake wawe wabunifu wa biashara zao na miradi ambayo itawafanya wajiajiri wenyewe.

# Tari yaanzisha teknolojia 55

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari) kituo cha Uyole kilichopo jijini Mbeya, imeanzisha teknolojia 55 kwa wakulima ambazo ni rafiki kwa mazingira ambazo zitaongeza kipato, kukuza ajira na kuwa na uhakika wa chakula. Hayo yalielezwa juzi na Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania, kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alipokuwa akiwaeleza waandishi wa habari mikakati wanayoifanya katika kuinua na kuboresha kilimo kupitia teknolojia mpya.

Dk. Bucheyeki alisema lengo kuanzisha teknolojia hizo ni kumsaidia mkulima kuondokana na kilimo cha mazoea kisichozingatia matumizi ya mbegu bora, zana duni za kulima na kutowatumia wataalamu.

Alisema teknolojia 55 zitafanya kazi kwenye mazao ya kimkakati yakiwamo mahindi, maharage, viazi mviringo na lishe, pareto, ngano, alizeti, parachichi ulezi na soya.


Aliongeza kuwa katika kufanikisha azma ya uanzishwaji wa teknolojia mpya kwenye sekta ya kilimo mwaka wa fedha 2019/2020 kituo cha Uyole wametenga kiasi cha shilingi bilioni moja.

Alisema wanakusudia kuwawezesha wakulima kuingia kwenye kilimo chenye manufaa ambacho kitasaidia kupunguza tatizo la udumavu na utapiamlo.

Mratibu Msaidizi wa Utafiti wa zao la Mahindi Taifa, Leonard Sabula, alisema asilimia 70 ya wakulima nchini wanajihusisha na kilimo cha mahindi na kwamba asilimia 46 ya ardhi yote nchini inalimwa zao hilo hivyo teknolojia mpya ambayo itahusisha matumizi ya mbegu bora, wataalamu na dhana bora za kilimo itasaidia kuongeza uzalishaji.

Sabula alisema mwaka huu wanaanzisha mashamba darasa 150 ya zao la mahindi ili wakulima wajifunze na kwamba katika kufanikisha hilo wanashirikiana na wadau wengine yakiwamo mashirika.

Mtafiti wa viazi lishe na mviringo Dk. Dorah Mende, alisema katika idara yake wanabuni aina 10 za mbegu bora za viazi hadi kufikia sasa wana aina nne ambazo ni tengeru, meru, ahsante na sherehekea.



# Jafo ataka Tarura iongezewe fedha

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amewaelekeza wataalamu wa Mfuko wa Barabara kuangalia namna ya kurekebisha kanuni ili kuongeza mgao kwa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (Tarura) kutoka asilimia 30 ili ifike 40.

Lengo la kuongeza kiwango ni kuongeza ufanisi katika utendaji kazi. Kwa mujibu wa kanuni zilizopo mgao wa fedha ni asilimia 30 kwenda Tarura na asilimia 70 kwenda kwa Wakala wa Taifa wa Barabara (Tanroads).

Jafo aliyasema hayo jijini hapa wakati akikabidhi magari 22, kwa Tarura yatakayohakikisha barabara zilizopo vijijini zinapitika wakati wote.

"Road Fund mnafanya kazi nzuri, hebu endeleeni kidogo kuangalia ile fomula au kanuni. Haiwezekani Tarura na kilomita inazohudumia hivi sasa tukaendelea na utaratibu wa zile za asilimia 30 kwa 70 haiwezekani," alisisitiza Jafo.

Alisema barabara za vijijini ndizo zinazounganisha sehemu ya masoko ya watu na sehemu za bidhaa zinapozalishwa hivyo ni vyema kanuni zikaangaliwa ili kuongeza fungu.

"Ukiangalia huko ndiko wananchi wanapoishi, wakulima wanapotaka kutoa mazao yao, hivyo wataalamu angalieni basi hata isipofika 50 kwa 50 angalau ifike 40 kwa 50 sababu tunachosema tuhakikishe wananchi wanapata fursa ya kuhudumiwa," alisema.

Akizungumzia kuhusu magari aliyokabidhi aliwataka madereva kuwa wa kwanza kutunza magari hayo kwa kuyafanyia matengenezo kwa muda unaotakiwa ili yaweze kudumu kwa muda mrefu. "Maeneo mengi nimeona hata kwa Mkuu wa Mkoa na Wilaya unakuta gari linapelekwa hata miaka mingapi haijafika. Unaambiwa gari limekufa, tena utaambiwa limeumia injini, kama injini imeharibika ina maana halikupata service iliyotakiwa. Hapo kuna uzembe umefanyika, kwa hiyo madereva mnaopewa magari haya hakikisheni mnayatunza," alisema waziri. Aidha, Jafo, alikemea tabia ya baadhi ya viongozi kunyanyasa madereva wao kwa kuchukua hela za mafuta na kukaa nazo, ilhali dereva ndiye anawajibu katika hilo.

"Niendelee kusema tabia ya kuwanyanyasa madereva siipendi. Kuna mabosi pesa ya mafuta anataka akae nayo kwenye semina anasaini hela ya mafuta ya dereva anachukua yeye hata hujui gari linaoshwaje na dereva akirudi ndio anafanya 'retirement' wakati pesa alikuwa nayo bosi wake. Jamani hii ni aibu. Naomba niwaambie viongozi mnaofanya hivi hii ni aibu," alisema Jafo.

Alisema kitendo hicho wakati mwingine kinamsababishia dereva kuwa na msongo wa mawazo na baadaye kusababisha ajali." Tunapotembea barabarani wakati mwingine sisi tumelala kwenye kiti dereva anahangaika na barabara tunawapa 'stresi' madereva. Tuache tabia hii tunawakatisha tamaa hata wakati mwingine ajali zinatokea kwa sababu yetu tuache," aliongeza Waziri Jafo.

Awali akitoa taarifa Mtendaji Mkuu wa Tarura, Mhandisi Victor Seff, alisema magari hayo yamenunuliwa na serikali kupitia mfuko wa barabara na ni sehemu ya juhudi zake katika kukabiliana na changamoto ya magari ya usimamizi.

Alisema ununuzi wa magari hayo 22 ni wa awamu ya pili, ambapo awamu ya kwanza walinunua magari 26 na yalishakabidhiwa na hivyo kufanya hadi sasa Tarura kuwa na magari 48 kwa gharama ya Sh. bilioni 4.3.

"Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kwa ajili ya magari ya usimamizi, tangu Tarura ianzishwe 2017, mwaka wa kwanza yalinunuliwa magari 26, mwaka wa pili yameletwa 22 ndiyo haya unayakabidhi na mwaka huu wa tatu tumeagiza magari 19 kutoka Road Fund Board," alisema Mhandisi Seff.



Mkazi wa Mtaa wa Osterbay, Kata ya Kiwanja cha Ndege, jijini Dodoma, Mzee Amani Ramadhani (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari waliomtembelea shambani kwake, wakati wakitekeleza kwa vitendo mafunzo ya uandishi wa habari za mazingira yaliyofanyika jijini hapo jana, na kuratibiwa na muungano wa vilabu vya waandishi wa habari Tanzania (UTPC). **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# TCRA yaonya Desemba 31

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Mawasiliano nchini (TCRA) kanda ya kati imewataka wakazi wa Dodoma kutumia kampeni ya uhamasishaji usajili wa simu inayoendelea jijini hapa kabla ya Desemba 31, mwaka huu.

Katika kampeni hiyo, TCRA imeunda timu ambazo zinazunguka kila mahali kuhamasisha jamii kusajili kadi zao za simu kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Akizungumza jijini hapa Meneja wa TCRA Kanda ya Kati, Antoni Manyanda, alisema lengo la kampeni hiyo ni kuwashawishi wananchi wote wafanye usajili wa kadi zao za simu mjini na vijijini kabla ya tarehe ya mwisho.

"Ninaomba wananchi wajitokeze kwa ajili ya kukamilisha usajili wa kadi za simu kwa sababu ikifika Desemba 31, hawatapata mawasilino," alisema Manyanda.

Katika kampeni hiyo wamekuwa wakitoa elimu ya umuhimu wa kusajili kadi za simu hasa ukizingatia teknolojia ya matumizi ya simu inakuwa kila wakati, alisema.

Aliongeza kuwa timu hiyo inazunguka katika wilaya zote kuhakikisha wakazi waliopo ndani na nje ya mji wanakamilisha usajili wa kadi zao za simu.

Alifafanua kuwa TCRA, inataka kuona kila mmoja amefanya usajili kwa vidole na kitambulisho cha taifa.

Alisema kampeni kwa kanda ya kati imeanzia mkoa wa Singida, na kufanikisha kwa asilimia nyingi kutokana na idadi kubwa ya watu wamejitokeza kushiriki katika kukamilisha usajili kupitia alama za vidole. Alisema wamekamilisha kampeni za uhamasishaji katika mikoa ya Singida, Tabora na hivi sasa wanaendelea jijini Dodoma na baadaye Kigoma.

Alisema jamii inapaswa kujua umuhimu wa kusajili kadi za simu kwa alama za vidole jambo litakalowaweka huru katika matumizi ya simu.

Alisema kwa upande wa Dodoma wanatarajia kuhitimisha kampeni hiyo wilayani Kondoa ambapo wataanza Novemba 27, kushawishi na kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kusajili kadi za simu kwa alama ya vidole na vitambulisho vya taifa.

Wakazi wa maeneo mbalimbali jijini hapa walisema kikwazo kikubwa katika kukamilisha usajili wa kadi za simu ni upatikanaji wa namba kutoka mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa Nida.

Akizungumza jijini hapa Ester Justine, alisema upatikanaji wa namba imekuwa tatizo ambalo linachangia msongamano wa watu katika baadhi ya maeneo ambayo wanakwenda kusajili.

# Wataka bajeti zaidi ili kudhibiti ukatili

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KITUO cha Sheria cha Haki za Binadamu (LHCR), kimeiomba serikali kila inapoongeza bajeti katika sekta nyingine, iongeze pia katika mahakama na taasisi zinazofanya kazi ya kutatua kesi za ukatili.

LHRC ilisema lengo ni kusaidia kupunguza vitendo hivyo kwa jamii hususani kwa wanawake na watoto.

Hayo yalibainishwa na Ofisa Dawati la Jinsia kutoka LHCR, Renatha Seleman, katika mdahalo uliojumuisha wadau kutoka mashirika mbalimbali yanayohusika kupinga ukatili dhidi ya wanawake, watoto na jamii kwa ujumla uliofanyika jijini hapa.

Renatha alisema kukosekana kwa bajeti ya kutosha, kunapelekea ukosefu wa rasilimali katika maeneo hayo na hiyo ni moja ya chanzo cha kuongezeka kwa matukio ya ukatili kwa sababu walengwa hawashughulikiwi ipasavyo na kwa wakati kwa sababu hawana vitendea kazi.

Kutokana na hilo serikali inapaswa kuangalia uwezekano wa kuongeza bajeti ya kutosha katika taasisi hizo ambazo wanaamini zikiboreshwa zitasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza matukio hayo yanayotokea kila kukicha kwa jamii inayotuzunguka.

"Unakuta mtu amefanyiwa ukatili anakwenda kuripoti Polisi au Ustawi wa Jamii akifika pale anaambiwa gari halina mafuta au maofisa ustawi wametoka, hivyo ni vema suala la bajeti katika taasisi hizo iongezwe," alisema Renatha.

"Wakati mwingine mwathirika wa tukio hilo analazimika kuchangia fedha ya mafuta ili mtuhumiwa afuatwe kwa ajili ya kukamatwa kujibu mashtaka," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali inapaswa kulitupia macho suala hilo, kwa sababu ambalo wanaamini ikifanyika hivyo matukio hayo yataongezeka.

Mbali na hilo alisema serikali pia inapaswa kuboresha vitengo hivyo ili kuwarahisishia utendaji kazi katika maeneo mbalimbali.

Alisema baadhi ya vitengo havina watumishi kuna mtu mmoja na ana matukio mengi kwa wakati moja jambo linalomkwamisha kufanyakazi kwa wakati na kuongeza kuwa serikali pia inapaswa kuongeza watu katika vitengo hivyo.

Pia Renatha alisisitiza suala la usikilizwaji wa haraka wa kesi za ukatili ikiwamo kutolewa adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine kutorudia makosa kama hayo.

Neema Bwaira, ambaye ni mtaalamu wa Haki za Watoto na Utawala kutoka Save the Children, alisema serikali inapaswa kuongeza bajeti katika maeneo hayo ili kuboresha mifumo ya utendaji kazi zinazohusiana na ukatili hapa nchini.



HABARI ZANZIBAR

## Balozi Iddi abainisha iliko nguvu ya CCM

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

NGUVU ya Chama Cha Mapinduzi, itaimarika maradufu iwapo wanachama wake watawashawishi vijana wenye nia na uzalendo kujiunga na CCM ili chama hicho kiendelee kuimarika.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, Balozi Seif Ali Iddi, alisema.

Aliwaambia viongozi wa ngazi mbalimbali wa chama hicho kuanzia mashina, matawi, mjimbo, wilaya hadi mkoa kuwa wanapaswa kusimamia kazi hiyo inayohitaji muda mwingi wa kujitolea ambayo ina faida.

Balozi Iddi alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na wanachama, viongozi na wananchi wa Kijiji cha Kipandoni baada ya kushiriki kazi za ujenzi wa taifa akiwa katika ziara ya kukagua shughuli za chama pamoja na kuelewa changamoto zinazowakabili ili kuzitafutia mbinu za utatuzi.

Alisema CCM inaendelea kukubalika na Watanzania mijini na vijijini kutokana na jitihada kubwa zinazochukuliwa na viongozi wake katika kuwaletea maendeleo na ustawi wao kupitia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2015 – 2020.

Alisema lengo la kujenga majengo ya kisasa ya chama hicho kama ilivyosisitizwa katika kanuni utawapa fursa wanachama hao kukutana au wakati mwingine kuendesha vikao vyao katika mazingira bora na salama. Balozi Iddi alisema wakati wa kuendesha vikao na mikutano ya wanachama chini ya miti au majengo mabovu umepitwa na wakati kutokana na mabadiliko makubwa yaliyopo ya mfumo wa kuendesha mambo kwa sayansi na teknolojia ambao CCM yenyewe imejikita kwenda nao.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa ofisi ya CCM, Katibu wa Tawi la Kipandoni Jadi Mtumwa Jadi, alisema tawi hilo likiwa miongoni mwa matawi 14 yaliyomo ndani ya Jimbo la Kiwengwa limeanza kujengwa Juni 28 mwaka 2009.

Jadi alisema tawi hilo lenye wanachama 150 hadi kukamilika kwake linatarajiwa kugharimu Sh. milioni 9.3 ambapo hadi sasa zimeshatumika zaidi ya Sh. milioni 7.7 zikiwamo nguvu za wanachama wenyewe.

Akitoa salamu za Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Kaskazini Unguja kwenye kikao cha majumuisho ya ziara hiyo, Mwenyekiti wa CCM mkoa huo, Iddi Ali Ame, aliiomba serikali itoe adhabu kali kulingana na uzito wa makosa ya udhalilishaji yanayoonekana kuongezeka kila kukicha.

Iddi alisema katika kupunguza makosa hayo umefika wakati sasa kuundwa kwa mahakama maalum itakayosikiliza kesi zinazowahusu wadhalilishaji wote wa vitendo vinavyowakosesha raha wananchi hasa wale wanaofanyiwa vitendo hivyo vya kudhalilishwa utu wao.

# Israel yatoa vifaa kudhibiti uhalifu

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

SHIRIKA la Ndege la Israel, limejitosa kudhibiti ugaidi na uhalifu kwa njia ya anga, visiwani Zanzibar baada ya kukabidhi mashine mbili za ugunduzi wa chembechembe na mabaki ya milipuko kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege vya Zanzibar.

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano ya mashine hizo aina ya ETD, yaliyofanyika mjini Zanzibar, Mkurugenzi Mipango na Miradi wa Mamlaka, Seif Abdallah Juma, alisema vifaa hivyo vitasaidia kudhibiti uingiaji wa vitu vinavyoweza kusababisha milipuko. Alisema, Zanzibar ni miongoni mwa nchi zinazotegemea sekta ya utalii hivyo kunahitajika kuimarishwa usalama zaidi katika uingiaji na utokaji wa wageni na vifaa.

Aidha, alisema kuwa mamlaka inalishukuru shirika hilo kwa kuwapatia mashine hizo, ambazo aliahidi kuzifanyia kazi kama ilivyokusudiwa.

Meneja wa Shirika la El Al Security ya Israil, Hardof Jacoby, alisema mashine hizo za kisasa zina uwezo wa kutambua na kugundua matukio ya kihalifu yenye ukubwa wa aina yoyote.

Alisema uwepo wa mashine hizo zitaweza kusaidia kutoingia uhalifu kwani ukizingatia kuwa nchi ya Zanzibar inategemea sekta ya utalii.

Akitoa shukurani kwa niaba ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Naibu Katibu wa Wizara hiyo, Shomari Omar Shomari, alisema, mashine hizo zitaweza kulinda uharibifu na uharamia unaoweza kutokea katika uwanja wa ndege.

Aidha, alisema kuwa Zanzibar ni kituo cha utalii ambacho wageni wake wanatoka katika mataifa mbalimbali, hivyo kupatiwa mashine hiyo kutaweza kuwalinda zaidi ikiwa ni jitihada za kutokomeza uhalifu unaoleta madhura.

Hivyo, aliwataka wafanyakazi wa mamlaka hiyo, kuzitunza mashine hizo ili kuweza kuimarisha huduma zaidi katika viwanja vyao.


Distributed via ippmedia

Mwekezaji mzawa ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Al- Zara Agriculture, Ahmed Saleh Mbarouk (katikati), akitoa maelezo kwa Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, kuhusu mradi wao wa Kilimo cha Biashara katika shamba lao, liliopo Kilombero Kaskazini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Unahitajika mwongozo kutoa elimu ya awali

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Idara ya Maandalizi na Elimu ya Msingi Zanzibar, Safia Ali Rijaal, amesema ni lazima kuwapo mwongozo madhubuti wa elimu ya maandalizi na msingi ili mafunzo yanayotolewa yawe rafiki kwa wanafunzi.

Alisema elimu ya maandalizi ni muhimu katika mazingira ya kumjenga mtoto kwenye kukua kiakili na ufahamu bora wa masomo.

Akifungua warsha kwa walimu wa maandalizi na msingi pamoja na kamati za shule kuhusu kutoa maoni ya marekebisho ya mtaala wa elimu hiyo iliyofanyika katika ukumbi wa kituo cha Walimu Kiembesamaki nje ya Mji wa Zanzibar.

Alieleza kuwa kubadilisha mtaala wa elimu ya maandalizi na msingi ni suala muhimu na linasaidia katika kutoa elimu bora itakayokidhi mahitaji ya watoto.

Aidha, alisema bila ya kuwalinda na kuwatunza dhidi ya vitendo viovu vikiwamo vya udhalilishaji hawatoweza kusoma kikamilifu na hivyo mwelekeo wao mzima wa masomo utaharibika.

Mkurugenzi huyo aliwataka wazazi, walimu na jamii kwa ujumla kushirikiana kuwasaidia watoto kwa kuwakinga na vitendo viovu, pamoja na walimu kuwa karibu na wanafunzi kwani kumeonekana baadhi ya watoto wa shule za msingi wamekuwa wakiwaharibu wenzao wanapokuwa darasani.

Pia aliwaomba walimu kusimamia watoto kuwa wasafi wanapokwenda shuleni na kuwasaidia kwa wale wanaoishi katika mazingira magumu hasa katika shule za vijijini kwa kuangalia uwezekano wa kuwapa msaada wa sare ili nao waweze kusoma kwa utulivu zaidi.

Akizungumzia suala la michango mkurugenzi huyo alisema suala hilo halikubaliki na limepigwa marufuku hivyo mwalimu atakayebainika kuendeleza suala hilo ajijue kuwa anajitia katika matatizo.

Alieleza kuwa suala la kuchangia michango ya maendeleo haliepukiki lakini siyo ndani ya shule au kuwafukuza wanafunzi shuleni kwa wasiochangia, suala la michango kama hiyo ni ya kamati za shule tena si kwa kumlazimisha mzazi bali ni hiari yake.

Washirika waliwashauri masheha pamoja na wenyeviti wa kamati za mitaaa, kuweka kanuni ndogo na kuwachukulia hatua hasa kwa wanaofanya biashara za kuchezesha 'game' wakati wa shule kwani watoto wengi, wamekimbilia maeneo hayo kuwa maficho yao wanapokimbia kusoma.

Mapema wakiwasilisha mada wawezeshaji kutoka Taasisi ya Elimu Zanzibar walisema mfumo wa marekebisho wa mtaala wa elimu ya maandalizi na msingi umewashirikisha wadau mbali mbali ambao ndiyo wahusika wakuu na hivyo ili kufikia malengo hayo ni vyema kupitia kwa makini na kutoa mapendekezo yao ili kufanikisha kupata mtaala ulio bora.

# Naibu sheha afungwa jela miaka 10 kubaka mtoto

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

NAIBU Sheha wa shehia ya Mgogoni Wilaya ya Chakechake, Mwadini Ali Mwadini, amehukumiwa kwenda jela kwa miaka 10, kulipi fidia ya Sh. milioni 2 pamoja na faini ya Sh. milioni moja, baada ya kupatikana na kosa la kumtorosha na kumbaka mtoto wa miaka 13.

Mshtakiwa huyo ambaye alikuwa rumande tokea Septemba 9, mwaka huu, akikabiliwa na makosa hayo Novemba 11, mwaka huu alipandishwa kizimbani Mahakama ya Mkoa wa Chakechake 'A' mbele ya Hakimu Abdul-Razak Abdul-Kadir Ali.

Katika hukumu hiyo, hakimu akisema atatumikia jela kwa miaka saba kwa kosa la ubakaji na atatumikia miaka mitatu kwa kosa la utoroshaji wa mtoto huyo.

Hakimu alimweleza mshtakiwa kuwa kutokana na ushahidi uliotolewa mahakamani na mashahidi mbalimbali akiwamo polisi mpelelezi, mtoto mwenyewe, mama mzazi, daktari umeitosheleza mahakama kumtia hatiani.

Awali mshtakiwa huyo alifikishwa mahakamani hapo, Septemba 9 mwaka huu, kwa kosa la utoroshaji na ubakaji wa mtoto wa miaka 13.

Mwendesha Mashtaka kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kisiwani Pemba, Mohamed Ali Juma, alidai mshakiwa alitenda kosa hilo Agosti 19, mwaka huu.

Alidai, kosa hilo lilifanyika saa 2:35 usiku wakati mtoto huyo akiwa katika eneo akiangalia televisheni, na baada ya kufanikiwa kurubuni, alimpeleka kichakani (migombani) na kumbaka.

Baada ya kusomewa shtaka lake, mshtakiwa kwa wakati huo alikana.

Kumtorosha mtoto aliyechini ya uangalizi wa wazazi wake ni kosa kinyume na kifungu cha 113 (1) (a) cha Sheria ya Adhabu Na. 6 ya Mwaka 2018, sambamba na kubaka, kuwa ni kosa kinyume na kifungu cha 108 (1) (2) (i) na kifungu cha 109 (1) cha sheri hiyo ya Zanzibar.



Ujenzi wa barabara ya mwendokasi kutoka Gerezani kwenda Mbagala, jijini Dar es Salaam, inayojengwa na mkandarasi kutoka China ukiendelea katika Barabara ya Kilwa, eneo la Jitegemee, juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Watendaji watakiwa usimamizi wa lishe

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MKUU wa Wilaya ya Buhigwe Mkoa wa Kigoma, Kanali Michael Ngayanali, amewataka watendaji wa kata na vijiji pamoja na wasimamizi wa afya wa wilaya hiyo, kuhakikisha wanajua umuhimu wa lishe katika ukuaji wa kimwili na kiakili.

Ngayanali alitoa rai hiyo wakati akizungumza na watendaji wa kata na vijiji pamoja na wasimamizi wa afya wa wilaya hiyo kwenye kikao cha kupitia viashiria vya utekelezaji wa mkataba wa lishe.

Ninyi ni wakurugenzi wa masuala ya maendeleo na suala la lishe ni sehemu ya maendeleo, hivyo utekelezaji wa mkataba wa lishe ni wajibu wenu sisi tutafuatilia utekelezaji wake, alisema.

Aidha, alisema katika utekelezaji wa mkataba wa lishe, majukumu yao ni kuhakikisha lishe ni ajenda ya kudumu katika vikao vya kisheria vya kamati ya maendeleo ya kata na kijiji ili kuchochea na kuibua fursa za lishe, matatizo na kutatua matatizo ya lishe yaliyopo kwenye jamii na kuhakikisha mpango kazi wa lishe unajumuisha afua za chakula na lishe, afya, majisafi na usafi wa mazingira na uchangamshi kwa watoto wadogo.

Mwakilishi wa Shirika la IMA World Health, Zidikheri Mziray, alisema kuwa aina za utapiamlo ni kula chakula kingi kuliko mahitaji ya mwili na kuwa watu wa aina hii wanakuwa na uzito uliozidi na vitambi.

Alisema watu wengi wanaona kuwa na kitambi ndiyo dalili ya afya bora au ufahari.

Ofisa lishe wa Mkoa wa Kigoma, Naomi Rumenyela, aliwataka watendaji wa kata na vijiji pamoja na wasimamizi wa afya wa Wilaya ya Buhigwe kuhakikisha wanatatua matatizo ya utapiamlo yaliyoko kwenye jamii.

# NEMC yataka sheria mipango miji ifuatwe kulinda mazingira

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamzi wa Mazingira (NEMC), limetoa wito kwa wafanyabiashara na wawekezaji hapa nchini kufuata sheria na taratibu za mipango miji ili kuepuka ujenzi holela wa viwanda katika makazi ya watu na kusababisha kero kwa wananchi.

Akizungumza jijini Mwanza katika ziara ya kukagua uzalishaji wa mifuko mbadala na kubaini iliyochini ya kiwango,

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema sheria zikizingatiwa katika ujenzi wa viwanda na shughuli nyingine, itasaidia kulinda mazingira.

"Ujenzi wa viwanda katika makazi ya watu unasababisha kero kwa wananchi kutokana na kelele, harufu au vumbi, ili kuepukana na hilo ni lazima wawekezaji kwenye viwanda wakafuata taratibu za mipango miji ili kuepusha adha kwa wananchi," alisema Dk. Gwamaka.

Alisema ujenzi unaofuata utaratibu wa mipango miji unasaidia kuyafanya mazingira kuwa salama na kupelekea huduma nyingine kufanyika kwa urahisi kama vile kuainisha idadi ya viwanda na mahali vilipo inakuwa

rahisi tofauti na hali ilivyo kwa baadhi ya maeneo nchini.

"Ushirikiano kati ya taasisi za serikali na wafanyabiashara,

wajasiriamali na wawekezaji unahitajika ili hatua anayofanya mwekezaji katika uwekezaji wake iendane na taratibu za serikali hali itakayosaidia kukuza uwekezaji wa viwanda unaofata utaratibu nchini," alisema.

Alisema shughuli zote za uendelezaji wa makazi na upangaji wa mautumizi ya ardhi zinasimamiwa na halmashauri za wilaya, miji, manispaa na majiji kwa niaba ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, hivyo NEMC tunashirikiana nao katika kuhakikisha mazingira yanatunza kupitia mwongozo wa mipango miji.

"Jukumu letu kubwa ni kuhakikisha shughuli za binadamu nchini hazileti athari katika mazingira ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya athari kwa mazingira kutokana na shughuli husika hali inayosaidia mazingira kuwa salama kwa kizazi cha sasa na baadaye," alisema.

Aidha, Dk. Gwamaka aliwataka wajasiriamali waliojenga viwanda vyao katika makazi ya watu kuwasiliana na mamlaka husika ili waweze kupatiwa mwongozo wa kuhamisha viwanda hivyo kwenda kwenye maeneo maalum ya viwanda ili kuepusha uchafu wa mazingira katika makazi ya watu.

"Mipango madhubuti ya ujenzi wa miundombinu, ulinzi wa mazingira ya asili, kuboresha mazingira ya kuishi na utunzaji wa mazingira hufanya mji ukue kwa urahisi na kwa ufanisi pasipo kuathiri mazingira hali itakayopelekea kuzidisha thamani ya ardhi na kuvutia wawekezaji zaidi," alisema Dk. Gwamaka. Mmiliki wa kiwanda cha Chilya's Tubing kilichopo Mwanza mjini, Spenas Masatu, alisema ushauri wa NEMC ameupokea na ataufanyia kazi kwanza kwa kuhamisha kiwanda chake kukipeleka katika maeneo ya viwanda.

"Nipo kuunga mkono azma ya serikali ya kujenga viwanda hivyo taratibu zote ni lazima nizifuate ikiwa ni pamoja na kukiweka kiwanda changu katika eneo linalotakiwa," alisema Masatu.

## HABARI KIMATAIFA

# Watu 68 washtakiwa mapinduzi Amhara

**ADDIS ABABA,** Ethiopia

UCHUNGUZI wa mauaji ya kisiasa yaliyotokea mwishoni mwa mwezi Juni umekamilika baada ya Waziri wa Sheria wa Ethiopia kutangaza. Mwendesha Mashtaka Mkuu Berhanu Tsegayé, alibaini kwamba tukio lililotokea Juni 22 ilikuwa ni jaribio la mapinduzi.

Juni 22, Rais wa Jimbo la Amhara, aliuawa pamoja na viongozi wengine waandamizi wawili. Saa, chache baadaye, Mkuu wa Jeshi la Ethiopia, pia aliuawa Addis Ababa, baada ya kupigwa risasi na mmoja wa walinzi wake. Baada ya zaidi ya miezi mitano ya uchunguzi, viongozi wa Ethiopia wanadai kwamba Naibu Mkuu wa Jeshi ndiye alikuwa anatarajiwa kuuawa.

Kwa mujibu wa Mwendesha Mashitaka Mkuu, watu 110 walipewa mafunzo maalum kwa kuandaa mashambulizi haya. Berhanu Tsegayé alisema kuwa watu hao ni kutoka Jimbo la Amhara lakini pia kutoka mji mkuu wa Ethiopia, Addis Ababa, na sehemu za kusini au magharibi mwa nchi hiyo.

Polisi ilikamata silaha, simu za mkononi, sarafu za ndani na nje na magari. Akaunti 22 za benki zilifungwa. Kwa jumla, watu 78 watashitakiwa mwishoni mwa wiki hii kwa mujibu wa televisheni ya serikali Fana.

Februari mwa huu, Mkoa wa Amhara nchini Ethiopia ulitangazwa kuwa unakabiliwa na hali ya sintofahamu. Hiyo ilitokea baada ya vifo vya watu zaidi ya 20 kati ya mwishoni mwa Septemba na mapema mwezi Oktoba, wakuu wa mkoa huo walitishia kuomba jeshi la nchi hiyo kuingilia kati ili kurejesha utulivu.

Machafuko katika eneo hilo la kaskazini mwa nchi yaliendelea kushuhudiwa kwa karibu miaka mitano. Mamlaka ziliripoti kutokea vifo vya watu 22 tangu mwishoni mwa mwezi Septemba mwaka huu. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Baraza la Usalama la Mkoa wa Amhara.

Baraza hilo lilizungumzia machafuko hayo kama makubwa katika ngazi ya kitaifa, vifo, nyumba zilichomwa, mali zilizoharibiwa na uchumi ambao ulivurugwa kwa kiasi kikubwa. Mzozo wenye vyanzo mbalimbali, ambao unaweza kuongezeka.

Baraza la Usalama la Mkoa wa Amhara lilibaini na kutangaza kuchukua hatua kadhaa. Wananchi wa kawaida walipigwa marufuku kumiliki silaha, makundi ya usalama yasiyojulikana rasmi yalipigwa marufuku na raia walitakiwa kuwafichua wahalifu. **RADIO UFARANSA**

# Israel, wanamgambo wasitisha mapigano

**GAZA,** Palestina

ISRAELI na wanamgambo wa itikadi kali wa Kiislamu wa Islamic Jihad wameafikiana kusitisha mapigano kati yao ambayo yamesababisha vifo vya Wapalestina 34 na kusimamisha shughuli mbalimbali katika maeneo kadhaa ya Israel.

Inaelezwa kuna afueni kwa raia wa kawaida katika ukanda wa Gaza na maeneo ya Israel baada ya Israel na wanamgambo wa Islamic Jihad kuafikiana kuweka silaha chini na kusitisha mapigano hayo.

Msemaji wa wanamgambo hao Musab al-Berim, alisema kuwa maafikiano hayo yalianza kutekelezwa kuanzia jana alfajiri huku naye msemaji wa jeshi la Israel Luteni Kanali Avichay Adraee akiandika katika mtandao wa kijamii wa twitter kuwa oparesheni yao Gaza imekamilika.

**Baada ya kuuawa kwa Bahaa Abu el-Atta, wanamgambo hao walijibu mashambulizi hayo ya angani kwa kurusha makombora 400 yaliyofika hadi eneo la Tel Aviv kama njia ya kulipiza kisasi.**

Alisema yamkini Misri imekuwa na mchango mkubwa katika upatanishi huo, baada ya maafikiano hayo, sasa baadhi ya vikwazo vilivyowekwa kwa baadhi ya wakazi wa kusini mwa Israel vimeondolewa huku hali ya kawaida ikirudi katika barabara za eneo la pwani ya Palestina.

Hali hiyo iliathiri masomo Israel baada ya shule kufungwa na watu kulazimika kusalia nyumbani, kwa mujibu wa Mkazi wa Gaza aliyekuwa akieleza kuhusu athari ya mapigano hayo.

"Mimi nafanya kazi, na kwa sababu ya vita kwa wakati huu sifanyi kazi."

Al-Berim aliongeza kuwa kusitishwa kwa mapigano hayo kulitokana na mahitaji yaliotolewa na wanamgambo hao ikiwamo kuitaka Israel kukomesha mashambulizi yao yaliyolenga viongozi wakuu wa kundi hilo.

Msemaji wa jeshi la Israel hakuthibitisha moja kwa moja iwapo mahitaji ya wanamgambo wa Islamic Jihad yalizingatiwa katika maelewano yao ya kusitisha mapigano.

Hata hivyo, katika hali iliyotilia shaka maelewano hayo, Waziri wa Mambo ya Nje wa Israel Yisrael Katz, alisema kuwa wataendelea kuwashambulia wanamgambo ambao amewataja kama hatari kwa usalama licha ya maafikiano hayo ya kusitisha mapigano.

Mapigano hayo yalizuka upya baada ya Israel kufanya shambulizi la anga mapema wiki hii lililomuua kiongozi wa wanamgambo wa Islamic Jihad Bahaa Abu el-Atta, mkewe na kuwajeruhi watoto wake wawili.

Baada ya kuuawa kwa Bahaa Abu el-Atta, wanamgambo hao walijibu mashambulizi hayo ya angani kwa kurusha makombora 400 yaliyofika hadi eneo la Tel Aviv kama njia ya kulipiza kisasi.

Jeshi la Israel lilisema kuwa Abu el-Atta ndiye aliyeongoza mashambulizi dhidi ya Israel na amekuwa kiungo muhimu katika kupanga mashambulizi ya makombora na yale ya ndege zisizokuwa na rubani dhidi ya Israel.

Aidha, kujitenga kwa kundi la wanamgambo la Hamas ambalo ni kubwa na lenye nguvu zaidi kuliko kundi la Islamic Jihad katika maafikiano hayo ya kusitisha mapigano, kumetafsiriwa kuwa sio mwisho wa vita kati ya Israel na makundi ya wanamgambo. **DW**


Distributed via ippmedia

Moja ya makombora yaliyotikisa Ukanda wa Ghaza . **PICHA: DW**

# Mawaziri wapata kashfa, wajiuzulu

**WINDHOEK,** Namibia

MAWAZIRI wa uvuvi na sheria nchini Namibia wamejiuzulu baada ya kufichuliwa kwa madai ya kuhusika kwao katika kashfa ya rushwa inayohusisha kampuni kubwa ya uvuvi ya Iceland iitwayo Samherji.

Waziri wa Uvuvi Bernhard Esau na Sheria Sacky Shanghala, wanadaiwa walitumia vibaya nyadhifa zao kujipatia fedha ili kutoa leseni za uvuvi, ikiwa ni pamoja na kuipatia kampuni ya Samherji, kwa mujibu wa gazeti moja la nchi hiyo, The Namibian.

Samherji imekana madai hayo kuwa ililipa kiasi kikubwa cha fedha kwa maofisa hao katika taifa hilo la kusini mwa Afrika ili kuweza kukwepa kipengele cha kudhibiti kiasi cha samaki inachostahili kuvua.

Madai hayo yalitolewa Jumanne wiki hii katika kipindi cha uchunguzi kilichotangazwa katika televisheni nchini Iceland cha Kveikur. Kipindi hicho cha taarifa za uchunguzi kimenukuu nyaraka, zilizovujishwa katika tovuti ya WikiLeaks zikidai kuwa kampuni ya Samherji ililipa mamia ya mamilioni ya krona sarafu ya Iceland kwa wanasiasa na wafanyakazi wa serikali nchini Namibia katika muda wa miaka 10 iliyopita. **DW**

# Miradi uwekezaji yaingiza Dola mil. 15.7 kwa miaka 4

Na Romana Mallya

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kimesema katika kipindi cha miaka minne kimetoa usajili wa miradi mipya ya uwekezaji 1,174 inayohusisha Dola za Marekani bilioni 15.7.

Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Geoffrey Mwambe, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza kuhusu miaka minne ya Rais John Magufuli na mambo waliyotekeleza kama kituo.

Alisema katika kipindi hicho, TIC imesajili miradi hiyo ambayo inatengeneza jumla ya ajira 159,833.

"Kati ya miradi hii, zaidi ya nusu ya miradi iliyosajiliwa, 626 sawa na asilimia 53 ya miradi yote iliwekezwa kwenye sekta ya viwanda.

"Sekta nyingine zilizokuwa na uwekezaji mkubwa ni pamoja na majengo ya biashara asilimia 10, ikifuatiwa na usafirishaji asilimia 9, utalii asilimia 8, kilimo asilimia 7, huduma asilimia 6 na sekta nyingine zimeweza kuvutia uwekezaji chini ya asilimia tano."

Alisema ajira zitokanazo na miradi ya uwekezaji katika kipindi tajwa unatarajiwa kutoa ajira za moja kwa moja zipatazo 159,833.

"Sekta zilizoongoza kwa utoaji wa ajira zitokanazo na uwekezaji huu ni pamoja na uzalishaji viwandani (60,465), kilimo (53,689), majengo ya biashara (14,127), Usafirishaji (11,482), Utalii (7,867) na Huduma (5,376)," alisema.

Mwambe alisema baadhi ya miradi mikubwa ambayo imeandikishwa na TIC kwa kipindi hicho ni kiwanda cha KEDA (Twyford) Tanzania Ceramic ambacho kipo kijiji cha Pingo, Chalinze Mkoani Pwani.

"Kiwanda hiki kimewekeza jumla ya Dola za Marekani milioni 56 kwa ajili ya kutengeneza vigae na kimeweza kutoa ajira za moja kwa moja kwa wazawa wapatao 2,000 na ajira zisizo za moja kwa moja zaidi ya 4,000.

Alisema kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha jumla ya mita tatu za mraba 50,000 za marumaru kwa mwaka na kwamba zaidi ya asilimia 90 ya mali ghafi zinazotumika, hupatikana Tanzania.

Alisema kiwanda cha sharubati cha Sayona ambacho kipo katika kijiji cha Mboga wilaya ya Bagamoyo Mkoa wa Pwani uwekezaji wake ni Dola za Marekani milioni 55 ambapo kwa siku kinazalisha tani 36,000 na kimeweza kutoa ajira kwa wazawa wapatao 800 na nyingine ni zaidi ya 30,000.

Alitaja kiwanda kingine ni cha Keds cha kutengeneza sabuni za unga za kufulia na vipodozi kilichopo Wilaya ya Kibaha, Mkoa wa Pwani ambacho ni cha pili kwa ukubwa barani Afrika baada ya kile cha Ghana.

Alisema mradi huo umewekeza jumla ya dola za Kimarekani milioni 11.8 na umetoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa wazawa zaidi ya 2,000.

Mwambe alitaja kingine kuwa kiwanda cha Kiluwa Steel Group kinachozalisha chuma katika mji mdogo wa Mlandizi ambacho kilianza uzalishaji mwaka 2017.

"Jumla ya dola za Kimarekani milioni 130 zimewekezwa katika awamu ya kwanza ya mradi huu ambao unatarajiwa kukamilishwa katika awamu tatu, kinazalisha jumla ya tani 200 za nondo kwa siku na ukikamilika uwezo wake ni kuzalisha tani 10,000 kwa siku," alisema.

Alisema mradi mwingine ni kiwanda cha vigae cha Goodwill Ceramics chenye uwekezaji wa Dola za Marekani milioni 53.




Meneja wa Benki ya NMB, Kanda ya Ziwa, Abraham Augustino (katikati), akikabidhi matofali kwa Mkuu wa Wilaya ya Chato, Mhandisi Charles Kabeho (wa pili kulia), kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu wa Chato, mkoani Geita hivi karibuni. Kulia ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Batholomeo Manunga. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Aahidi huduma bora ya mafuta

Na Enock Charles

WATANZANIA wamehakikishiwa kuendelea kupata huduma bora ya mafuta ya pertoli na dizeli.

Ahadi hiyo ilitolewa jijini Dar es Salaam jana na Kampuni ya Mafuta ya Total Tanzania kupitia Mkurugenzi mpya wa Kampuni hiyo, Jean-Francois Schoepp, wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Huduma kwa Wateja, iliyozinduliwa jijini Dar es Salaam.

Schoepp alisema kampuni ya Total huwa inafanya Wiki ya Huduma kwa Wateja kila mwaka, kwa sababu kuu tatu; ya kwanza ni kuwa karibu na wateja kwa kuwasikiliza kujua mahitaji na matarajiyo yao kutoka Total.

Sababu ya pili ni kuwaelimisha wateja kuhusu ubora wa mafuta ya Total yenye kiambata cha excellium, ubora wa vilainishi vya Total na ubora wa huduma mbalimbali zinazotolewa kwenye vituo vya Total.

"Sababu ya tatu, kwetu mteja kwanza. Hivyo Wiki ya Huduma kwa Wateja inatoa fursa kwa watumishi wote wa Total wakiwamo menejimenti, kutembelea vituo vyetu ili kuweza kuwahudumia wateja na kuweza kufahamu changamoto zao ili tuweze kuwahudumia kwa usahihi," alisema.

Mkurugenzi wa vituo vya Total, Marieme Sow, alisema wiki hii, kampuni hiyo inaonyesha kwa vitendo jinsi inavyowathamini wateja wake na namna bora ya kuwahudumia, ikiwamo kuwasikiliza na kupokea mrejesho kutoka kwa wateja kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa.

Marieme ameongeza wiki hii pia inatoa fursa kwa kampuni kuwa wabunifu zaidi kwa kukidhi mahitaji ya wateja wao mbalimbali kwa kadri wanavyopokea maoni, hivyo wateja kupata kilicho bora.

# Sheria ardhi zilizopitwa na wakati kubadilishwa

Na Mary Geofrey

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imesema ipo tayari kuzifanyia marekebisho sheria zote za ardhi zilizopItwa na wakati kwa lengo la kuendana na kasi ya ukuaji wa teknonolojia.

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Nicholas Mkapa, kwa niaba ya Waziri wa wizara hiyo, Wiliam Lukuvi, wakati akifungua kongamano la wapimaji ardhi Tanzania na Mkutano Mkuu wa mwaka Chama cha Wapimaji Ardhi ( IST) jana jijini Dar es Salaam.

Mkapa aliwataka wadau wa ardhi nchini, kuwasilisha mapendekezo ya sheria zinazotakiwa kufanyiwa marekebisho ili zibadilishwe.

Alisema taaluma ya upimaji na teknolojia ya uandaaji wa ramani inabadilika kwa kiwango kikubwa na kusababisha sheria hizo kuwa kikwazo cha maendeleo ya taaluma hiyo.

"Nimeshamuagiza Mkurugenzi wa Upimaji Ramani kuwashirikisha wadau wote kutoa maoni ili kupata sheria itakayokidhi mahitaji. Matumaini yangu mchakato huu utaharakishwa ili marekebisho yafanyike mapema na kuendana na kasi ya Serikali katika utekelezaji wa majukumu yenu," alisema Mkapa.

Alisema taaluma ya upimaji wa ramani nchini inaongozwa na sheria mbili ambazo ni CAP324 Ordinance Law na Sheria namba mbili ya mwaka 1977 ambazo zimeshapitwa na wakati.

Sambamba na hilo, Mkapa alisema wizara hiyo kwa kushirikiana na wataalamu wa kimataifa imeshakamilisha kazi ya kuunda mfumo mpya wa upimaji ardhi utakaotumika kwa ajili ya kazi zote za upimaji.

Mkapa alisema mfumo huo unaotumika kimataifa, umekamilika na unatarajiwa kuchapishwa kwenye gazeti la serikali mwishoni mwa mwaka huu.

Aliitaka IST kuweka mkakati maalumu wa kujenga utaratibu wa kudhibiti maovu kwa taaluma hiyo ili kutoa ushirikiano wa kutosha kwa serikali na msaada wa ufafanuzi wa mwenendo wa taaluma na wataalamu ya upimaji.

Naye Makamu wa Rais wa IST, Bille Mussa, alisema mkutano huo umewakutanisha wataalamu wa upimaji ardhi 130 na kampuni tano ambazo mbili zimefadhili mkutano na tatu zimeshiriki maonyesho.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/VIWANJA

**NYUMBA 2 ENEO MOJA ZINAUZWA** Zipo Ukonga Mombasa. Ya mbele njengo wa kisasa vyumba 4 nyingine chumba na sebule 4 kiwanja robo eka. Za kupaua. Bei maelewano. Piga simu: 0719 619444 / 0782 574669.

**VIWANJA VITATU VINAUZWA,** NO.1-341-1890 SQM NO. 2-1342- 1391 SQM NO.3 1343- 1556 SQM BLOCK A KISUKURU-TABATA. SIMU. 0754 857523/0786 857523

## NAFASI ZA KAZI

**Wanahitajika wanaume wenye umri kuanzia miaka 30 hadi 45** kwa nafasi za udereva (Ikiwemo Class C, C1, C2 na C3). Wanahitajika wanawake wenye umri kuanzia miaka 25 hadi 35 kwa nafasi za mauzo (sales za bidhaa). Mshahara wa kuvutia utatolewa. Mawasiliano piga 0714 634 046. Piga simu kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi jioni tu.

**2 ACRE YARD FOR RENT**

Facing New Julius Nyerere International Airport. Call: +255 754 375 967. Email: **gold@goldtz.net**

## MCHANGANYIKO

**MONKAL I INSULIN**:Inawasaidia wagonjwa waliogua kisukari kwa muda mrefu,inarejesha kongosho ktk utoaji ute mchungu na sukari kuwa normal balance 4- 5- 6, iko katika mfumo wa maji na vidonge,husaidia mmengenyo wa chakula,tiba lishe,gout,uzazi,tumbo la vidonda na kuunguruma na kujaa gesi n.k :0713293988/0758078280.

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI SHAHIDI**
**(MCA/84)**
**MAHAKAMA YA MWANZO YA MIKONGENI WILAYA YA MOROGORO**
**MADAI NAMBARI: 20B...2018**

**Mdai:** DOROTEA ALBERT ANAMDAI
**Mdaiwa:** JOHN MARTIN CHAMZILA
**Kwa:** JOHN MARTIN CHAMZILA, MKAZI WA KISAKI, IFAKARA MOROGORO

**Ombi la Mdai:** DOROTEA ALBERT
Madai ya: PESA SHILINGI 2,956,000/= **PIA KWA AJILI YA UTEKELEZAJI.**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani Siku ya JUMANNE ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 19 mwezi 11 mwaka 2019 saa 02:30Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa. Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 29 mwezi 10 mwaka 2019.

115519202

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**
**SHAURI LA MADAI NAMBA 37 YA MWAKA 2019**

**JACKSON ELIAS MASHAMBO ..............MDAI**

**DHIDI YA**

**JOSEPH JUMA BUJIMILE...........................MDAIWA**

**KWA: JOSEPH JUMA BUJIMILE**
**POPOTE ULIPO**

Mahakama hii inakufahamisha kwamba mdai amefungua madai dhidi yako. Nakala yake inapatikana katika Mahakama hii.

Shauri limepangwa kusikilizwa mnao tarehe 20/11/2019 saa 2:30 asubuhi na unatakiwa kuwepo, au kuwakilishwa kisheria pamoja na kuleta utetezi wako dhidi ya madai haya.

Zingatia kwamba kutokufika kwako tarehe hiyo, shauri litaanza kusikilizwa bila ya wewe kutaarifiwa tena, na maamuzi kutolewa.

Imetolewa kwa mkono wangu na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 13/11/2019.

115519002

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**NANZOKE THEOBALD MVUNGI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T. 141 DPT TOYOTA IST.

Chassis namba NCP60-0123371.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: KW/BJ/WL.201.

115519102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/63)**
**Mahakama ya mwanzo ya MJINI – TANGA**
**Wilaya ya TANGA**
**MADAI NAMBARI: 112 ya 2019.**
**Mdai: JUMA SALIMU WARYOBA**
**Mdaiwa: SAIDI IDD ATHUMANI**
**Kwa: C/O MW/KITI WA MWAKIDILA B KATA YA TANGASISI - TANGA**

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba MADAI YA 1,200,000/-

Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya Jumanne tarehe 21/11/2019 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku hiyo iliyotajwa hapo juu mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea wito wa kuitwa shaurini mahakama hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa. Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 31/10/2019.

Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
TANGA MJINI

115518602

---

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP/HATI YA MATOKEO



**PROTEXTATUS DEODATUS WAIJAHA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.4014/0064** iliyotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika Shule ya Sekondari Winning Spirit. Yeyote atakaeion atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa:**UD/B.I/1/10/24/62/19**

1155177802

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **IJUMAA** tarehe **15/11/2019** kampuni ya **TRANSCARGO LTD** itasafirisha Mzigo wako wenye vipimo vikubwa kutoka **GEITA** kuelekea **DAR ES SALAAM,** gari hilo lenye namba za usajili:

   **T 631 CFU/ T 348 ACY**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

   Urefu - mita 21
   Upana - mita 4.3
   Kimo - mita 5.3

3. Njia itakayotumika: **GEITA hadi DAR ES SALAAM kupitia DODOMA,**

   Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**KAGERA LILILOPO BUKOBA**

**MAOMBI MADOGO NA: 128/2019**

**JOVESTUS NESTORY ........................... MDAI**

**DHIDI YA**

1. **MADUHU KATANI**
2. **GEOPHREY SOSPTER ............ WADAIWA**
3. **GODWIN PANTALEO**

**KWA: MADUHU KATANI NA GODWIN PANTALEO (POPOTE PALE MLIPO)**

Mnaarifiwa/ unaarifiwa kuwa Maombi Madogo Na: 128/2019 yamepangwa kutajwa tarehe 28.11.2019 mbele ya mwenyekiti wa baraza , R.Mtei saa 2:00 asubuhi.

Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/ mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa baraza hili leo tarehe 29.10.2019.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

115518502

---

Distributed via ippmedia

**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa**

**Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0767 223311**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

Nipashe
MWANGA WA JAMII

---

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# IBRAHIMOVIC AMALIZANA RASMI NA LA GALAXY




**NEW YORK,** Marekani

KLABU ya LA Galaxy ya nchini Marekani imethibitisha kuachana na mshambuliaji Zlatan Ibrahimovic, kwa kusema, hatokuwa sehemu ya kikosi kwa msimu ujao wa Ligi ya Marekani.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 38, anaondoka mjini Los Angles, Marekani huku akiacha historia ya kupachika mabao 52, katika michezo 17 aliyocheza na kutoa pasi za mwisho 53.

Zlatan alijiunga na klabu hiyo maarufu duniani, mwezi Machi mwaka 2018 akitokea Manchester United ya England.

"Tunatoa taarifa kuwa, Zlatan hatokuwa nasi kwa msimu ujao wa Ligi ya MLS, tunamshukuru kwa mchango alioutoa klabuni hapa tangu alipojiunga nasi, tunamtakia kila la kheri katika maisha yake ya soka," alisema Rais wa LA Galaxy Chris Klein.

"Tangu mwaka 2018, Zlatan amekuwa msaada mkubwa katika kikosi chetu, ametoa mchango wa kutosha ambao umeisaidia klabu yetu kufikia malengo yake, japo kwa uchache. Tunajivunia kufanya kazi na mchezaji huyu, na tunaamini ipo siku atarejea hapa katika nafasi tofauti. Tunamshukuru sana Zlatan kwa kazi nzuri aliyoifanya."

Taarifa za kuondoka rasmi LA Galaxy, zinaendelea kukoleza tetesi za mshambuliaji huyo kurejea barani Ulaya kujiunga na moja ya klabu nguli zinazotajwa kuiwania saini yake, kupitia dirisha dogo la usajili, litakalofunguliwa hapo Januari 2020.

Kabla ya kujiunga na LA Galaxy, Zlatan aliwahi kuzitumikia klabu kubwa barani Ulaya kama FC Barcelona, Juventus, Paris St Germain, Inter Milan na AC Milan.

Distributed via ippmedia

# Silva afungiwa, apigwa faini kumbagua Mendy

**LONDON,** England

KIUNGO wa Manchester City, Bernardo Silva amefungiwa mchezo mmoja na kupigwa faini ya pauni 50,000 na Chama cha Soka cha England kwa kile kilichoonekana kama kumbagua Benjamin Mendy kwenye Twitter.

Silva alikutwa na hatia hiyo baada ya kuweka kibonzo cha 'chokuleti' maarufu nchini Ureno ya Conguitos, huku akiandia "kisia ni nani huyo?" Ambapo aliiweka Septemba 22, mwaka huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, aliifuta posti hiyo na akahoji: "Siku hizi huwezi hata kumtania rafiki yako..."

Katika taarifa ya FA ya juzi Jumatano ilisema: "Bernardo Silva amefungiwa kwa mchezo mmoja na amepigwa faini ya pauni 50,000 kwa kuvunja Kanuni ya FA kifungu E3.

Kocha wa Silva, Pep Guardiola alimtetea mchezaji wake huyo kwa kitendo hicho, huku mchezaji mwenzake, Raheem Sterling akisema "Bernardo alifanya utani kwa rafiki yake."

Mchezaji wa zamani wa England, John Barnes pia aliiambia Sky Sports News kwamba tuhuma za ubaguzi za Silva hazikuwa na maana.

Silva na Mendy wote waliichezea AS Monaco na wote walitua pale kwenye Uwanja wa Etihad mwaka 2017.

Kiungo huyo wa Ureno amefunga mabao matano katika mechi 17 alizoichezea City katika mashindano yote msimu huu na alifunga wakati kikosi hicho cha Guardiola kikichezea kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Liverpool Jumapili.

Silva ataukosa mchezo wa Man City dhidi ya Chelsea Novemba 23, mwaka huu.






# Barca vs Madrid sasa Desemba 18

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA itaikaribisha Real Madrid Desemba 18, mwaka huu kwenye mchezo wa kwanza wa Clasico msimu huu wa 2019-20.

Barca na Real Madrid awali mchezo wao ulitakiwa kupigwa Oktoba 26, mwaka huu, lakini ukaahirishwa kutokana na maandamano yaliyokuwa yakiendelea kule kwenye Jimbo la Catalunya.

Shirikisho la Soka la Hispania (RFEF), lilikubali maombi ya pamoja ya klabu hizo kwamba mchezo huo upigwe Desemba 18, mwaka huu.

Taarifa ya RFEF kupitia ukurasa wake wa Twitter Jumatano ilisema kuwa, tarehe ya pili ya Desemba 7 kwa ajili ya mchezo huo, ilionekana kuwa itavuruga ratiba nyingine.

Barcelona na Real Madrid zina pointi sawa kileleni mwa msimamo wa LaLiga, 25 baada ya mechi 12, huku Barca ikiongoza kwa tofauti ya mabao.

# Bayern wamnyatia Sane kimyakimya

**MUNICH,** Ujerumani

LEROY Sane anaweza tena kuwa kwenye rada za Bayern Munich wakati wa dirisha dogo la usajili Januari.

Winga huyo wa Manchester City, Sane alikuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, lakini aliumia Agosti wakati wa mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Liverpool.

Sane alifanyiwa upasuaji na anatarajia kurudi uwanjani mwakani, wakati ambao pia Bayern wanaweza kuanzisha mpango wa kumuwania tena.

"Kulikuwa na majadiliano juu ya Sane," mjumbe wa bodi ya Bayern, Edmund Stoiber ameiambia Sport Bild.

"Bahati mbaya majeraha na operesheni yakasababisha mazungumzo kuvunjika.

"Tutaona jinsi mambo yatakavyokuwa. Nikiwa kama mjumbe wa bodi ya ushauri na mjumbe ya bodi ya usimamizi, nina imani kubwa na uongozi wangu wa soka.

"Kama watatoa tena ofa kipindi cha usajili wa dirisha dogo, hilo ni jambo la kusubiri."

Sane alijiunga na City




# STERLING ARUDISHWA ENGLAND VS KOSOVO


Distributed via ippmedia

**LONDON,** England

GARETH Southgate atamuita Raheem Sterling kwenye mchezo wa England nchini Kosovo baada ya kuachwa katika mechi ya kufuzu michuano ya Euro 2020 dhidi ya Montenegro.

Pointi moja tu ilikuwa inahitajika kwa vinara hao wa Kundi A dhidi ya Montenegro kuweza kufuzu kwenye fainali hizo katika mchezo huo uliopigwa jana Alhamisi.

Sterling alitemwa kwenye kikosi cha England baada ya kukwaruzana na mchezaji mwenzake, Joe Gomez, ambapo ilikuwa chini ya saa 24 baada ya mchezo uliozikutanisha klabu zao Manchester City na Liverpool.

Kwenye mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Anfield, Man City walifungwa mabao 3-1 na Sterling na Gomez ugomvi wao ulianzia huko.

Hali hiyo hiyo ikamfanya kocha, Southgate kumtema kwenye kikosi hicho kuelekea mchezo wa jana dhidi ya Montenegro.

# *Wenger alamba bonge la dili Fifa*

**GENEVA,** Uswisi

ARSENE Wenger ameteuliwa kuwa Ofisa Mkuu wa Maendeleo ya Soka Duniani na Shirikisho la Soka la Kimataifa, Fifa.

Wenger mwenye umri wa miaka 70, alitumia muda wa miaka 22 akiwa kocha pale Arsenal hadi mwaka 2018 na wiki za hivi karibuni alikuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa kuinoa klabu ya Bayern Munich, lakini sasa amepata dili mpya huko Fifa.

Wakati wake akiwa pale kwa 'Washika Bunduki' hao, Wenger alikuwa akitajwa kama mmoja wa makocha bora duniani na ameshinda mataji matatu ya Ligi Kuu ya England pamoja na mataji saba ya FA.

Kwa mujibu wa Fifa, Wenger pia atakuwa akiongoza pia kwenye "masuala ya kiufundi" akiwa mjumbe wa kamati ya ushauri wa ufundi, pia akiwa sehemu ya mabadiliko ya sheria za michezo.

Wenger atahusika zaidi na masuala ya elimu ya ukocha na programu ya kuwahamasisha wachezaji wa zamani kuwa makocha. Baada ya kuteuliwa, Wenger amesema: "Nina hamasa kubwa ya kufanya kazi katika nafasi yangu hii mpya na ni changamoto mpya kwangu."

Rais wa Fifa, Gianni Infantino katika taarifa yake amebainisha kwamba ana imani kubwa na uzoefu wa Wenger kwenye maendeleo ya soka dunia.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



Distributed via ippmedia

# SUAREZ SASA AOMBA STRAIKA MPYA BARCA

●●● Ni bora maana kutaleta ushindani, lakini utafika wakati ambao umri wangu hautaniruhusu...

**BARCELONA,** Hispania

LUIS Suarez ameitaka Barcelona kutafuta straika mpya licha ya kwamba kunaweza kuwa tishio kwake katika nafasi ya kuanza kikosi cha kwanza.

**Vinara hao wa LaLiga, Barca wamekuwa wakihusishwa na kumsajili Lautaro Martinez, Erling Haaland na Carlos Vela wakati huu wakisaka mbadala wa kuiimarisha safu hiyo ya ushambuliaji ya Ernesto Valverde.**

Klabu hiyo ilishindwa kumrejesha Neymar kutoka Paris Saint-Germain wakati dirisha la majira ya joto likikaribia kufungwa, ikikiacha kikosi hicho kuwa na ushindani hafifu katika nafasi ya mshambuliaji asili wa kati anayocheza Suarez.

Suarez, 32, amefunga mabao sita katika mechi nane za LaLiga alizoanza msimu huu, lakini anajua hataweza kuonyesha kiwango cha juu mara zote.

"Utafika wakati ambao umri wangu hautaniruhusu kuishi hadi kile ambacho Barcelona inahitaji kushindana," Suarez aliliambia gazeti moja la Uruguay. "Lakini kwa kadri niwezavyo, maadamu nina nguvu, kunipa ushindani ni bora zaidi.

"Kwamba wanatazama ama wanataka kuleta namba tisa mwingine hakuna lililo geni, ni ukweli wa soka.

"Itakuwa bora kwangu na bora kwa klabu, kwa sababu kutaleta ushindani, na itakuwa bora kwa baadaye kwa sababu klabu inaweza kuandaa mchezaji kwa msaada wa wachezaji wote wakubwa pale Barcelona."

Suarez alijiunga na Barca akitokea Liverpool mwaka 2014 na sasa yupo katika msimu wake wa sita hapo Camp Nou.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Ajax, amepanga kuendeleza wasifu wake kisoka hadi angalau Kombe la Dunia mwaka 2022, ambalo litakuwa mara ya nne kwake kucheza kwenye michuano hiyo.

"Natumai hivyo," alisema. "Ukweli ninashawishika kwa hilo, ndiyo."

Suarez ni sehemu ya kikosi cha Uruguay kwa mechi zijazo za kirafiki za kimataifa dhidi ya Hungary leo na kisha Argentina hapo Novemba 18, na ni mara ya kwanza kwake kujumuishwa katika kikosi cha timu ya taifa tangu michuano ya Copa America Juni mwaka huu.

## ZISIKUPITE

### LIVERPOOL NAYO KWA SANCHO

WINGA wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, anataka kuondoka kwa miamba hiyo ya Ujerumani, na vinara wa Ligi Kuu England, Liverpool wakiwa miongoni mwa klabu zilizoonyesha nia ya kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 19. ***(Mail)***

### BECKHAM AMGEUKIA CAVANI

NAHODHA wa zamani wa England, David Beckham, amekuwa akiwapigia simu wachezaji anaowataka Inter Miami. Mshambuliaji, Luis Suárez, 32, kiungo wa Real Madrid, Mcolombia James Rodriguez, 28, na straika wa Paris St-Germain na Uruguay, Edinson Cavani, 32, wote wamekuwa wakihusishwa na kutimkia timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu ya Marekani, MLS. ***(Sun)***

### ERIKSEN, TOBY KUONDOKA

SPURS inahofia kiungo Mdenmark Christian Eriksen, 27, na mabeki Wabelgiji Jan Vertonghen, 32 pamoja na Toby Alderweireld, 30, watafuata njia moja na Danny Rose na kuondoka wakiwa huru mwishoni mwa mikataba yao majira ya joto yajayo. ***(Star)***

### GUARDIOLA ATAJWA BAYERN

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola anadhaniwa kutokuwa na furaha hapo Kaskazini-Magharibi mwa England na Mhispania huyo amekuwa akihusishwa na kurudi kwa mabingwa wa Bundesliga, Bayern Munich. ***(Bild - in German)***

### WILLIAN AWINDWA BARCA, JUVE

WINGA wa Chelsea, Mbrazil Willian, 31, ambaye mkataba wake hapo Stamford Bridge unatarajiwa kumalizika majira ya joto yajayo, anawindwa na Juventus pamoja na Barcelona, na zitajaribu kumsajili kwa mkataba wa awali hapo Januari mwakani. ***(Mirror)***

### CONTE AMTAKA GIROUD INTER

KOCHA wa Inter Milan, Antonio Conte yupo tayari kumsajili mshambuliaji wa Chelsea, Olivier Giroud katika dirisha la usajili la Januari. Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 33, mkataba wake na 'Blues' unamalizika majira ya joto yajayo. ***(Gazzetta dello Sport, via Express)***

### KOEMAN AJITANGAZA BARCA

KOCHA wa Uholanzi, Ronald Koeman amesema kuna uwezekano wa yeye kwenda kuinoa Barcelona baada ya michuano ya Euro 2020. ***(Marca)***

### MALCOLM LULU ARSENAL, LIVER

ARSENAL, Liverpool na Manchester United zote zinamfuatilia mshambuliaji wa West Brom, Jovan Malcolm, 16. ***(Mirror)***

### SILVA KUMFUATA INIESTA

KIUNGO wa Manchester City, David Silva, 33, yupo njiani kujiunga na Mhispania mwenzake Andres Iniesta, 35, katika klabu ya Vissel Kobe ya Japan mara mkataba wake hapo Etihad utakapomalizika mwishoni mwa msimu wa Ligi Kuu England. ***(Mail)***

### KOULIBALY, MERTENS SOKONI

NAPOLI inaweza kulazimika kumuuza Kalidou Koulibaly, 28, ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester United na mshambuliaji Mbelgiji Dries Mertens, 32, anayedhaniwa kuwindwa na Arsenal, kwa ada punguzo baada ya kuanza msimu vibaya. ***(Ilmattino - in Italian)***

## HABARI MICHEZO

### MSIMAMO LIGI KUU BARA



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Simba | 9 | 7 | 1 | 1 | 16 | 3 | 22 |
| 2. Kagera Sugar | 10 | 6 | 2 | 2 | 14 | 8 | 20 |
| 3. Lipuli | 10 | 5 | 3 | 2 | 18 | 10 | 18 |
| 4. Prisons | 10 | 3 | 7 | 0 | 11 | 7 | 16 |
| 5. Namungo | 10 | 5 | 1 | 4 | 9 | 8 | 16 |
| 6. JKT Tanzania | 10 | 4 | 3 | 3 | 8 | 8 | 15 |
| 7. Mtibwa Sugar | 11 | 4 | 3 | 4 | 10 | 11 | 15 |
| 8. Ruvu Shooting | 11 | 4 | 3 | 4 | 9 | 10 | 15 |
| 9. Alliance | 10 | 3 | 5 | 2 | 8 | 7 | 14 |
| 10. Mbao | 11 | 3 | 5 | 3 | 9 | 9 | 14 |
| 11. Azam | 7 | 4 | 1 | 2 | 7 | 4 | 13 |
| 12. Polisi TZ | 9 | 4 | 1 | 4 | 9 | 10 | 13 |
| 13. Coastal Union | 10 | 3 | 2 | 5 | 8 | 9 | 11 |
| 14. Mwadui | 11 | 2 | 5 | 4 | 7 | 10 | 11 |
| 15. Yanga | 5 | 3 | 1 | 1 | 6 | 4 | 10 |
| 16. KMC | 8 | 2 | 2 | 4 | 5 | 8 | 8 |
| 17. Biashara Utd | 10 | 2 | 2 | 6 | 6 | 11 | 8 |
| 18. Mbeya City | 10 | 1 | 5 | 4 | 7 | 16 | 8 |
| 19. Ndanda | 9 | 1 | 4 | 4 | 6 | 9 | 7 |
| 20. Singida Utd | 11 | 0 | 4 | 7 | 4 | 15 | 4 |

# KIBADENI, MWAISABULA WAMCHAMBUA CHAMA

**Na Focus Nicus**

KOCHA na mchezaji wa zamani wa Simba, Abdallah "King" Kibadeni pamoja na mdau na nguli wa soka nchini, Kenny Mwaisabula wametofautiana kimtazamo katika maoni yao kuhusu madai ya kuporomoka kiwango kwa kiungo wa Wekundu wa Msimbazi, Mzambia Clatous Chama.

**Chama ameingia katika mjadala mzito kupitia mitandao ya kijamii na vyombo mbalimbali vya habari kuhusu kinacho tafuna kiwango chake kwa sasa ukilinganisha na ubora wa hali ya juu aliokuwa nao msimu uliopita.**

Hata hivyo, wakati Kibadeni akisema kinachomtesa zaidi Chama ni kutokana



Kibadeni



Mwaisabula

na ushindani mkubwa wa namba uliopo Simba kwa sasa, Mwaisabula yeye amefunguka kuwa starehe nyingi huenda kikawa chanzo cha kiungo huyo raia wa Zambia kuporomoka kisoka.

"Pale Simba kwa sasa kuna ushindani mkubwa katika nafasi ya kiungo anayocheza Chama, kuna wachezaji kama Kahata [Francis] ambaye anakuja juu kwa sasa na pia Ajibu [Ibrahimu] na wengine, hivyo anajikuta hapati namba mara kwa mara, jambo ambalo inakuwa vigumu kuonekana kuwa katika kiwango bora," alisema Kibadeni.

Lakini Mwaisabula alisema Chama amekuwa miongoni mwa nyota wanaoelekea kuporomoka kwa kasi kiwango chake ukilinganisha na wakati anatua Simba akitokea Power Dynamos ya Zambia.

"Inaonekana starehe zinamgharimu Chama na sasa hana tena ule ubora wake dimbani. Huyu si yule Chama ninayemfahamu, si yule wa Simba wa mwaka jana, wachezaji wengi wa nje wakija Tanzania hawamalizi mwaka mmoja wanapotea dimbani, wanaendekeza starehe zaidi kuliko kazi," alisema.

Mbali na Ajibu na Kahata, lakini pia nafasi hiyo ya Chama anaweza kuicheza vizuri Mtanzania Hassan Dilunga pamoja Sharaf Eldin Shiboub aliyesajiliwa msimu huu akitokea kwao Sudan, ambaye pia ameanza kunyooshewa kidole kuwa uwezo wake umeanza kushuka mapema.


Distributed via ippmedia

Shabiki wa Taifa Stars, Bongo Zozo, (kulia) akimkabidhi pesa Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wilfred Kidao, za kuwanunulia tiketi mashabiki wa kike 100, kwa ajili ya kuingia Uwanja wa Taifa kuishangilia Taifa Stars kwenye mechi ya kuwania kufuzu Afcon 2021 dhidi ya Equatorial Guinea kesho. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Shime apania ubingwa Cecafa Wanawake*

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Wanawake 'Kilimanjaro Queens', Bakari Shime, ambaye anakiandaa kikosi hicho kwa mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa Challenge) kwa upande wa wanawake, amesema anataka kuweka historia nyumbani ya kubaki na kombe la michuano hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Shime alisema amejipanga vizuri kuhakikisha anapata matokeo mazuri huku akiwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi uwanjani.

"Tutashuka uwanjani tukiwa na tahadhari kubwa kwa kujua tupo nyumbani tunaangaliwa na Watanzania wote, kikubwa ni kuzidi kumwomba Mungu," alisema Shime.

Aliongeza kuwa, anaendelea kukinoa kikosi chake kwa ajili ya kukiweka fiti tayari kwa kutoa ushindani mkubwa katika mashindano hayo ambayo yatafanyika katika Uwanja wa Chamazi, Mbagala jijini Dar es Salaam kuanzia kesho.

"Kikosi changu kinaendelea vizuri na mazoezi mpaka sasa sina majeruhi hata mmoja na wote wapo vizuri tayari kwa mashindano," alisema.

Alisema anaheshimu kila timu ambayo ipo katika mashindano hayo kwa kudai zote zina ubora mzuri.

"Naziheshimu timu zote kwa kuamini zina ubora ndio maana zikapata nafasi ya kushiriki michuano mikubwa kama hii, alisema kocha huyo.

## Mtifuano Ligi Kuu Z'bar kesho

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MTIFUANO wa Ligi Kuu Zanzibar mzunguko wa 10 unatarajiwa kuanza kutimua vumbi kesho, Jumamosi kwa kupigwa michezo nane katika viwanja tofauti visiwani hapa.

Mwenge ya Pemba yenye alama tisa ikiwa nafasi ya 10 kwenye msimamo wa ligi hiyo, itakuwa na kibarua kigumu katika Uwanja wa Gombani dhidi ya timu ya Chuoni ambayo ipo nafasi ya tano na pointi 15.

Kesho pia mashabiki wataishuhudia timu ya Polisi yenye alama tisa ikiwa nafasi ya 12, ikivaana na Jamhuri ya Pemba ambayo ipo nafasi ya 11 na alama zake tisa.

Mzunguko huo wa 10, utaendelea tena keshokutwa, Jumapili katika Uwanja wa Amaan ambapo Mlandege yenye alama 18 ikiwa nafasi ya nne, itashuka dimbani hapo kuumana na Maafande wa Kipanga waliopo nafasi ya 14 wakiwa na alama saba.

Katika dimba la Mao siku hiyo Jang'ombe Boys ikiwa nafasi ya sita na alama zake 13 watavaana na Maafande wa Mafunzo wenye pointi 12 wakishikilia nafasi ya saba.

Michezo
Ijumaa Novemba 15, 2019
Nipashe



Suarez aomba straika mpya Barca UKURASA 30

TUTAWANYOOSHA...



Distributed via ippmedia

Nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta na mchezaji mwenza wa kikosi hicho, Abdulazizi Makame (jezi namba 21), wakiwa mazoezini katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana, kujiandaa na mechi dhidi ya Equatorial Guinea ya kuwania kufuzu Afcon nchini Cameroon 2021 itakayopigwa uwanjani hapo leo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mkwasa aandaa panga kali Yanga

**Na Somoe Ng'itu**

KUELEKEA dirisha dogo la usajili wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, Boniface Mkwasa, amesema atatoa tathmini ya wachezaji wapya anaowahitaji ikiwa ni pamoja na wakukatwa ili kuimarisha kikosi chake kwa ajili ya kuwania ubingwa wa ligi hiyo mapema wiki ijayo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkwasa, alisema ameshaanza kuufanyia kazi mchakato huo na atatoa tathmini ya wachezaji wanaopaswa kuongezwa na kuachwa kwenye kikosi hicho kwa ajili ya kuanza mchakato mpya wa kusajili wachezaji atakaowahitaji.

Mkwasa alisema baada ya kukutana na Kamati ya Ufundi, watashauriana na kufanya uamuzi wa pamoja kabla ya kutoa uamuzi wa mwisho wa kikosi wanachokihitaji kuendelea nacho katika vita ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA nchini.

"Kwa muda ambao nimekaa na timu, tayari nimeshaanza kuifanyia kazi ripoti ya kiufundi, hadi wiki ijayo nitakuwa nimekamilisha ripoti yangu ya kiufundi kuhusu usajili wa dirisha dogo, ila nitawasiliana na Kamati ya Ufundi kwa ajili ya ushauri zaidi," alisema Mkwasa.

Kocha huyo aliongeza kuwa anaamini baada ya usajili huo mdogo kufanyika, kikosi cha Yanga kitarejea kwenye upinzani na kwa sasa ni mapema mno kutabiri timu itakayochukua ubingwa kutokana na ushindani na changamoto iliyopo katika ligi.

"Bado ligi haijakolea, mechi tulizocheza ni chache na kama tutatulia, au timu nyingine zitajipanga vizuri, lolote linaweza kutokea kwenye vita ya ubingwa," alisema kocha huyo wa zamani wa Twiga Stars na Taifa Stars.

# Stars: Njooni, E' Guinea hawatoki

**Na Shufaa Lyimo**

## ●●● Ndayiragije aanika mkakati wake akiwaita mashabiki Taifa, Boli Zozo shabiki kindakindaki awalipia wanawake...

LENGO ni ushindi nyumbani! Hiyo ndiyo kauli ya Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa Tanzania, 'Taifa Stars', Etienne Ndayiragije kuelekea mechi yao ya leo dhidi ya Equatorial Guinea kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2021 nchini Cameroon.

**Taifa Stars itaikaribisha Equatorial Guinea katika mechi hiyo ya kwanza ya hatua ya makundi itakayopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam majira saa moja usiku leo.**

Akizungumza na Nipashe jana, Ndayiragije alisema maandalizi kuelekea mchezo huo yamekamilika na mpaka sasa hana majeruhi yeyote katika kikosi chake huku akifurahia morali ya wachezaji kuwa juu.

"Kikosi changu kinaendelea vizuri na mazoezi, kila mchezaji morali yake ipo juu kuhakikisha ushindi unabaki nyumbani kabla ya kuelekea Libya,"alisema kocha huyo raia wa Burundi aliyerithi mikoba ya Mnigeria Emmanuel Amunike aliyetimuliwa.

Alisema tayari ameifuatilia timu hiyo na kubaini aina ya uchezaji wake huku akibainisha kuwapo kwa wachezaji wengi wazuri wanaounda kikosi hicho cha Equatorial Guinea.

"Tutaingia uwanjani tukiwa na tahadhari kubwa, lakini lengo kubwa likiwa ni kubakisha ushindi nyumbani," alisema kocha huyo wa zamani wa Azam huku akibainisha kufurahishwa na ushirikiano mzuri uliopo kwa wachezaji wa timu hiyo ndani na nje ya uwanja.

### TFF YAFUNGUKA

Kwa upande wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), limewataka wachezaji wa kikosi hicho kulipa deni kwa Watanzania kwa kuhakikisha wanapata matokeo mazuri nyumbani.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao alisema maandalizi kwa ajili ya mchezo huo yamekamilika na waamuzi watakaochezesha mchezo huo tayari wameshawasili.

"Maandalizi kwa ajili ya mchezo wetu wa kesho (leo), yamekamilika kwa asilimia 100 tunaomba wachezaji wetu wasituangushe katika mchezo huo.

"Sisi kama TFF tumejipanga kuhakikisha usalama wa kutosha unakuwapo na tunaomba Mungu atupe matokeo yenye kuridhisha," alisema Katibu huyo huku akiweka wazi wamepanga viingilio rafiki ili kila Mtanzania apate nafasi ya kuingia uwanjani kuwapa sapoti mashujaa hao wa Tanzania.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa kamati ya hamasa ya timu hiyo ambaye pia ni msemaji wa Klabu ya Simba, Haji Manara, aliwataka mashabiki wa Simba kuachana na ushabiki wa timu na badala yake wawe kitu kimoja kuiunga mkono timu ya taifa.

"Mimi niwaombe mashabiki wetu wa Simba tuachane na tabia ya kwenda uwanjani kushangilia wachezaji kwa mapenzi ya timu bali tuwe kitu kimoja kushangilia timu ya nchi," alisema Manara.

Naye Boli Zozo, ambaye pia yupo ndani ya Kamati ya Uhamasishaji ya Stars, alimkabidhi Kidao fedha kwa ajili kununua tiketi 100 maalumu kwa wanawake ili wajitokeze kwa wingi uwanjani kuishangilia Taifa Stars.

"Nimejitolea kununua tiketi 100 kuwapa wanawake ili wapate nafasi ya kwenda uwanjani kushuhudia mchezo huo, yote ninaonyesha jinsi nilivyo na moyo na timu yangu ya Taifa," alisema Boli Zozo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >